# Nipashe

Ijumaa Februari 15, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579842

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Mvua mafuriko yaja, taasisi sita kuathirika

UKURASA 3


BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Mkutano wa Marekani Poland wasusiwa
Umaskini hadi kulemazwa; sasa atekeleza nadhiri kuhudumia maskini, wanaoteswa
UCHUMI
Habari katika picha
KIUCHUMI ZAIDI
Takwimu za Biashara

UKURASA 13

# Chadema wamjia juu Waziri Lugola

UKURASA 2


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**MICHAEL WAMBURA AKWAA KISIKI**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imesema haina...

UKURASA WA 22

**DIWANI KORTINI KISA TUHUMA KUGHUSHI**

WATUHUMIWA wa kesi ya kughushi hati ya kiwanja cha Waziri Mkuu wa...

UKURASA WA 26

**EKARI 42 ZA POLISI ZAGAWIWA WANANCHI**

SERIKALI imekonga nyoyo za wananchi baada ya kuwapatia ekari...




Makamu wa Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Michael Wambura, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kutupilia mbali hoja ya mawakili wake ya kutaka hati ya mashtaka dhidi yake ifanyiwe marekebisho. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Mpangaji anayeishi maisha ya ajabu Dar

UKURASA 2



## Sababu 3 mauaji ya watoto Njombe

UKURASA 2

**MICHEZO** **AUSSEMS, ZAHERA WATAMBIANA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mpangaji aishi maisha ya ajabu

Na Beatrice Shayo

MKAZI wa Buguruni Madenge jijini Dar es Salaam, amewaacha watu midomo wazi kutokana na aina ya maisha anayoishi kwenye chumba chake cha kupanga ambacho kimejaa uchafu wa kupindukia.

Akizungumzia tukio hilo, Diwani wa Buguruni, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Madenge, Adam Fugame, alisema amemfahamu mtu huyo kwa zaidi ya miaka 25 na kwamba amekuwa na tabia ya usiri sana.

"Kwanza kuyapata majina yake mawili ni vigumu kutokana na usiri wa maisha yake. Yeye huwa hakai na watu karibu na kuzungumza nao mara kadhaa anapita na kusalimia tu na kuondoka zake," alisema.

"Ukimwangalia ni mtu mstaarabu sana, huwezi kuamini kama anaishi katika haya matakataka tuliyoyakuta chumbani kwake, yaani imetushangaza sana kwa kweli hatuamini tuliyoyaona,"alisema.

Alisema chanzo cha kugundua kwamba mpangaji huyo anaishi kwenye chumba kilichojaa taka ni Februari 11, mwaka huu. Walikuja watu nyumbani kwake majira ya saa 11 jioni na kumjulisha kuwa kuna nyumba inawaka moto na ndipo walipokwenda katika hilo tukio.

Fugame alisema wakati huo mwenye chumba hicho alikuwa safarini mkoani Morogoro, hivyo walijadiliana na kukubaliana kuwa mlango uvunjwe.

"Kwa sababu mwenyewe hayupo ikaamuliwa mlango uvunjwe ili wazime moto tulipovunja mlango tukawa tukashangaa kuona taka nyingi sana kule ndani na kilichokuwa kinaungua ni kigodoro kidogo sana ambacho alikuwa akilalia," alisema.

Alisema siku iliyofuata, askari walifika eneo la tukio na kuchukua maelezo yao huku akisema kwa mwonekano wake mitaani wameshangazwa kukuta hali kama hiyo.

Fugame alisema dada wa mtu huyo alimweleza kuwa kaka yake alikuwa akifanya kazi katika benki mmoja katika nafasi ya mhasibu na alistaafu miaka miwili iliyopita.

Alisema jana alimkabidhi dada yake jukumu la kutafuta

INAENDELEA UK. 8

# Chadema wamjia juu Lugola

Na Romana Mallya

SIKU moja baada ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, kumtaka Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, arejee nchini kuendelea na kesi, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimemjia juu na kuhoji kama uchunguzi dhidi ya tukio hilo hauwezi kufanyika bila yeye kuwapo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Mafunzo na Operesheni wa Chadema, Benson Kigaila, alisema inashangaza kuona waziri huyo akiwaaminisha Watanzania kwamba uchunguzi wa tukio hilo hauwezi kufanyika bila Lissu kuwapo nchini.

Septemba 7, 2017 Lissu alishambuliwa kwa kupigwa zaidi ya risasi 30 na watu wasiojulikana nje ya nyumba aliyokuwa akiishi Area C, jijini Dodoma.

Juzi, Waziri Lugola, akiwa jijini Arusha, alimtaka mbunge huyo kurejea Tanzania akidai kuwa yeye na dereva wake ni mashahidi muhimu wa tukio hilo.

Hata hivyo, Kigaila, alihoji kama kigezo ni Lissu kurejea, mbona wako waliorudi lakini hadi sasa hawajaambiwa majibu ya uchunguzi matukio yao.

"Waziri jana (juzi) alisema Lissu ametelekeza kesi yake, maana yake mpaka Lissu awepo ndipo uchunguzi ufanyike, ndicho anachotaka kutuambia bila Lissu uchunguzi haupo," alisema.

"Ni kazi ya Jeshi la Polisi kuchunguza tukio bila kujali aliyeathirika au kuumia yupo au hayupo, amekufa au yuko hai na Lissu hahusiki kwenye uchunguzi kama ambavyo waathirika wengi hawahusiki kwenye uchunguzi," aliongeza.

Kigaila alitolea mfano wa tukio lililotokea siku chache kabla ya Lissu ambalo Meja Jenerali wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), alipigwa risasi na watuhumiwa walikamatwa siku iliyofuata.

"Wanataka kutwambia kwamba Meja Jenerali ndiye aliyewaeleza ni kina nani walimpiga risasi? Meja Jenerali Kombe miaka ya 1990 alipigwa risasi na kufariki dunia, hakusubiriwa hadi afufuke mbona watuhumiwa walikamatwa wakapelekwa mahakamani na kuhukumiwa?" Alihoji.

Kigaila alitolea mfano tukio lingine la aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Abdallah Zombe, aliyetuhumiwa na wenzake kuhusika kwenye mauaji ya wafanyabiashara wa madini Morogoro, ambao walikamatwa na wengine wakahukumiwa bila wafanyabiashara hao kufufuka.

"Kama Kangi Lugola anataka kutwambia hii kesi ni ya Lissu kwa hiyo ameitelekeza, kwa maana hiyo polisi haiwezi kuchunguza, sasa Lissu angekufa maana yake uchunguzi usingefanyika," alisema.

Kigaila alihoji kwa nini kesi hiyo mpaka Lissu awepo wakati kesi zingine zinachunguzwa bila wahusika kuwapo.

"Ndiyo maana tunataka haya majibu wayatoe, kadiri wanavyofanya propaganda za kufanya

INAENDELEA UK. 8



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akishirikiana na Balozi wa Italia nchini, Roberto Mengoni (kulia) na Mwenyekiti wa Shirika la Communita Solidal nel Mondo la Italia, Michelangelo ChiurChiu, kukata utepe kuzindua kituo kipya cha utengamano wa watoto wenye ulemavu cha Kila Siku Community Based Rehabilitation kilichoko Kawe jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Sababu 3 mauaji ya watoto Njombe

Na Mwandishi Wetu, NJOMBE

TIMU ya Wataalamu kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imesema imebaini sababu tatu zilizochangia kuwapo kwa mauaji ya watoto mkoani Njombe.

Pia timu hiyo imeutaka uongozi wa Mkoa wa Njombe kuhakikisha ajenda ya ulinzi na usalama wa mtoto inakuwa ya kudumu mkoani humo.

Kiongozi wa timu hiyo, Hanisa Selengu, akizungumza mjini Njombe jana, alizitaja sababu zilizochangia kuwapo kwa mauaji dhidi ya watoto kuwa ni tabia ya kukumbatia mila potofu na zisizofaa zinazochangia kuwa na mifarakano katika jamii.

Alisema sababu zingine ambazo timu yake imebaini ni migogoro ya kifamilia ambayo imekuwa ikisababishwa na visasi vya wazazi na ndugu pamoja na desturi ya ukimya na ugumu wa kueleza uhalifu unaotokea.

Selengu alisema katika siku 10 walizokaa mkoani humo, timu yake imejifunza masuala mbalimbali kutoka kwa jamii na kubaini na changamoto hizo tatu.

Alisema ajenda ya ulinzi wa mtoto isifanyike tu panapotokea matukio ya utekaji na mauaji ya watoto, bali iendelee kupewa mkazo na kusisitizwa na viongozi mkoani humo.

Aliutaka uongozi wa Mkoa wa Njombe kuifanya ajenda hiyo kuwa ya kudumu na kupewa nguvu na viongozi katika mikutano mbalimbali wanayofanya na wananchi.

Aliongeza kuwa, ili kuhakikisha ulinzi na usalama kwa mtoto, Kamati za Ulinzi na Usalama wa wanawake na watoto zina jukumu kubwa la kuhakikisha mtoto anakuwa salama na kuhakikisha agenda ya usalama kwa watoto inapewa kipaumbele zaidi ili kuhakikishia mtoto huyo ulinzi na usalama.

Alisema timu yake inapendekeza mkoa kuhakikisha mipango ya kamati za ulinzi wa wanawake na watoto zinatengewa bajeti na kutekeleza majukumu yake.

"Huduma za kisaikolojia na kijamii ziendelee kutolewa kwa familia zilizopoteza watoto na makundi maalum," alisema kiongozi huyo na kubainisha kuwa mapendekezo mengine ya timu yake kuwa ni kuendelea kuelimisha na kuhimiza mazingira salama kwa watoto nyumbani, shuleni na mazingira yanayowazunguka.

Selengu pia alisema kuna haja kuendelea kufanya mikutano ya mara kwa mara kwa familia, makundi maalum na wanajamii kuhusu mila na desturi potofu.

Mwezi uliopita, kuliripotiwa matukio ya utekaji na mauaji dhidi ya watoto mkoani Njombe, huku wanaotekeleza ukatili huo wakidaiwa kunyofoa baadhi ya viungo kwenye miili ya watoto wanaowaua.

Tayari watu watatu wamefikishwa mahakamani na kushtakiwa huku wengine 27 wakiendelea kushikiliwa na Jeshi la Polisi kutokana na matukio hayo.

HABARI KITAIFA

# Wambura akwaa kisiki

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imesema haina mamlaka ya kusikiliza hoja yoyote katika kesi inayomkabili Makamu wa Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Michael Wambura (52), dhidi mashtaka 17 ya uhujumu uchumi.

Pia imesema haina mamlaka hayo mpaka itakapopokea kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) cha mahakama hiyo kusikiliza tuhuma hizo ikiwamo kughushi, kuwasilisha nyaraka ya kughushi, kujipatia zaidi ya Sh. milioni 95 kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha zaidi ya Sh. milioni 100.

Uamuzi huo mdogo ulitolewa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi Kelvin Mhina.

Hakimu alisema hati ya mashtaka dhidi ya mshtakiwa imefunguliwa chini ya kanuni ya adhabu na sheria ya kutakatisha fedha.

Hata hivyo, alisema kwa mujibu wa sheria, mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza wala kutolea maamuzi hoja zilizotolewa na pande zote mbili kwa sababu DPP hajatoa kibali kuisikiliza kesi hiyo.

"Mahakama hii haina mamlaka ya kusikiliza wala kutengua kasoro za hati ya mashtaka mpaka pale DPP atakapoipa kibali, haya ndiyo maamuzi yetu ya kisheria, haki ya kukata rufani iko wazi," alisema Hakimu Mhina.

Alisema mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu na kesi hiyo itatajwa Februari 28, mwaka huu.

Februari 11, mwaka huu, Wambura alipandishwa kizimbani kwa mara ya kwanza na kusomewa hati ya mashtaka ya uhujumu uchumi chini ya kifungu cha Kanuni ya Adhabu na Sheria ya Kutakatisha Fedha.

Upande wa utetezi ukiongozwa na mawakili Majura Magafu na Nehemia Nkoko, ulipinga hati ya mashtaka dhidi mshtakiwa kwamba vifungu vya sheria vilivyotumika si vya uhujumu uchumi ni vya kanuni ya adhabu.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na

INAENDELEA UK. 8



Mawaziri wanane, wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi; TAMISEMI, Suleiman Jaffo; Maji na Umwagiliaji, Prof Makame Mbarawa; Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla; Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina; Ulinzi na Kujenga Taifa (JKT), Hussen Mwinyi; Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Musa Sima, wakiwa katika kikao jana mkoani Morogoro, walikokwenda kusitisha zoezi la kuhamisha wakazi wanaozungukwa na Bwawa la Mindu. **PICHA: FRANK MONYO**

# Tahadhari yatolewa mvua kubwa

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA) imetoa tahadhari ya kuwapo kwa mvua kubwa (juu ya wastani) kwa baadhi ya mikoa ya Kanda ya Ziwa, Dar es Salaam na Kilimanjaro.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu utabiri wa mvua za masika kwa mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka, Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, alisema kuwa, kutokana na mifumo ya hali ya hewa ilivyo kwa sasa na inavyotarajiwa kuwa kwa kipindi chote kuanzia Machi mpaka Mei mwaka huu, maeneo mengi yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka yanarajia kuwa na mvua za wastani.

Hata hivyo, Dk. Kijazi alisema baadhi ya maeneo katika mikoa ya Dar es Salaam, Zanzibar, Arusha, Kilimanjaro, Kagera, Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Shinyanga kuna uwezekano mkubwa wa kupata mvua kubwa (juu ya wastani).

"Kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa, tunategemea mvua hizi zitaanza wiki ya mwisho ya mwezi huu, ikianzia mikoa ya Kagera na baadaye kusambaa kwenye mikoa mingine ya ukanda huo," alisema.

Mkurugenzi huyo aliongeza: "Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani kwa maeneo mengi ya mikoa ya hii ya Kanda ya Ziwa, hata hivyo kwa baadhi ya maeneo machache ya Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Kibondo kutakuwa na upungufu wa mvua."

Alisema mikoa ya Dar es Salaam, Tanga,

INAENDELEA UK. 8

# Mawaziri wanusuru wakazi 133 kuhamishwa bwawani

**Na Frank Monyo,** MOROGORO

TAKRIBANI Kaya 60 zenye watu 133 wanaozunguka bwawa la Mindu Manispaa ya Morogoro, wamenusurika kuhamishwa kwa muda, baada ya serikali kuingilia kati na kusimamisha zoezi hilo lililotakiwa kuanza Jumatatu.

Wananchi ambao wanatakiwa kuhama ni kutoka Kijiji cha Mindu na Kasanga.

Uamuzi wa kusitisha zoezi hilo ulitolewa jana mkoani Morogoro baada ya mawaziri kutoka wizara nane kutembelea bwawa hilo kwa lengo la kuangalia changamoto ya sheria ya maji na mazingira zinavyoingiliana na kuleta mkanganyiko.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kikosi kazi hicho kilichoteuliwa na Rais John Magufuli kwa ajili ya kutembelea maeneo mbalimbali nchini yanayoingiliana katika mazingira na makazi ya watu, alisema Rais ameagiza timu hiyo kutembelea sehemu zenye changamoto na kumkabidhi ripoti kwa lengo la kumaliza changamoto hizo.

Mawaziri wengine ni Suleiman Jafo (Tamisemi); Maji na Umwagiliaji, Profesa Makame Mbarawa; Maliasili na Utalii Dk. Hamis Kigwangalla; Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina; Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT),, Hussen Mwinyi; Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba na Naibu Waziri Mazingira, Musa Sima.

Wakiwa kijiji cha Mindu lililopo bwawa hilo, Lukuvi, aliiomba Bodi ya Maji Bonde

INAENDELEA UK. 8




# Manufaa ya mfumo mpya wa BoT utumaji wa fedha

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imezindua mfumo mpya wa malipo ya fedha kwa njia ya kielektroniki utakaowezesha utumaji wa huduma za kifedha kutoka katika taasisi moja kwenda nyingine.

Pamoja na kurahisisha utumaji wa fedha, pia utaondoa urasimu na udanganyifu kwa taasisi za fedha.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuzindua mfumo huo, Mkurugenzi wa Mifumo ya Malipo ya Taifa wa BoT, Benard Dadi, alisema mfumo huo pamoja na kurahisisha utumaji wa fedha, pia utasaidia benki hiyo kupata taarifa za kifedha katika kila benki badala ya kusubiri kupelekewa taarifa hizo na taasisi za benki.

Kwa mujibu wa Dadi, pia utasaidia kuonyesha kiwango cha mapato ambacho serikali inapaswa kupata kupitia taasisi za fedha.

Kadhalika, alisema pia utapunguza matumizi ya fedha taslimu na kuondoa usumbufu ambao umekuwa ukitokea wa kukosea taarifa za kifedha ikiwamo majina na taarifa nyingine muhimu.

"Mfumo huo utasaidia kuonyesha kila muamala unaofanyika katika kila kampuni nyingine, kwa hiyo kutusaidia kujua miamala ni mingapi kwa siku, kwa mwezi, kwa mwaka, kuleta udhibiti ndani ya BoT, badala ya kwenda kwenye kampuni kwenda kuomba taarifa, hizo taarifa tutakuwa nazo, tutajua serikali inapata ushuru kwa kiasi gani kwa usahihi zaidi bila kutegemea mpaka ifike mwisho wa mwezi ndio tupewe taarifa kujua serikali imepata ushuru kiasi gani," alisema Dadi na kuongeza:

"Vyote hivyo vitarahisishwa sana kupitia mfumo huu na kufanyika miamala utakuwa unachukua muda mfupi ndani ya sekunde mbili au tatu kumfikia mteja na pia itasaidia kupunguza gharama. Mfumo huu unajengwa ndani ya miezi 18 na utatumia wataalamu kutoka BoT," alisema Dadi. Sosteness Kewe, Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania (FSDT), alisema mfumo huo mpya utakuwa na manufaa makubwa kwenye uchumi wa nchi, wananchi wa kawaida, wafanyabiashara na wakulima kwa sababu utakapoanza kufanya kazi utasaidia kupunguza gharama za utumaji wa fedha pamoja na kutoa taarifa za watu wote wanaotumia huduma za kifedha.

Alisema taarifa hizo pia zitasaidia taasisi za fedha kuongeza ufanisi namna ya kuboresha huduma kwa wateja.

"Tunajua wengi tunatumia mfumo wa fedha taslimu ambao ni gharama kubwa, lakini mfumo huu wa kutuma pesa kwa haraka utaepusha mengi, kwa mfumo wa sasa unatakiwa uende benki ukachukue pesa au umtume mtu au umtume boda boda, lakini kwa mfumo huu ambao BoT umezindua utarahisisha miamala mbalimbali kulipa au kupokea pesa kiurahisi hasa wafanyabiashara, wakulima kufanya miamala kwa urahisi zaidi, hawatakuwa na haja ya kulipa fedha taslimu,"alisema Kewe.

# Mbowe, Matiko warejea mahabusu hadi Jumatatu

**Na Hellen Mwango**

KESI ya jinai inayomkabili Mwenyekiti Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na wenzake wanane wanaokabiliwa na mashtaka ya uchochezi, imepigwa kalenda mpaka Februari 18, mwaka huu.

Kesi hiyo yenye usajili namba 112/2018 itaendelea kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Kelvin Mhina, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam mpaka Mahakama ya Rufani itakapotoa uamuzi wa rufani ya Jamhuri.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba wanasubiri rufani iliyopo Mahakama ya Rufani.

Hakimu Mhina alisema kwa sababu mahakama yake haina jalada halisi la kesi hiyo bado haijapangiwa hakimu wa kuisikiliza.

Alisema kesi hiyo imepangwa kutajwa mahakamani hapo, washtakiwa waliopo nje kwa dhamana wataendelea na dhamana na Mbowe na Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, wataendelea kukaa rumande hadi uamuzi wa rufani utakapotolewa.

Awali kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama hiyo, Wilbard Mashauri (sasa ni Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania).

Rufani ya Jamhuri dhidi ya Mbowe na wenzake imepangwa kusikilizwa Februari 18, mwaka huu.

Mbali na Mbowe na Matiko, washtakiwa wengine wanaokabiliwa na kesi hiyo ni Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Zanzibar, Salum Mwalimu na Naibu Katibu Mkuu Bara, John Mnyika, ambaye pia ni Mbunge wa Kibamba.

Wengine ni Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee; Mbunge wa Bunda, Esther Bulaya; Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vincent Mashinji na Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 13, ikiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia, kuhamasisha hisia za chuki, kushawishi hali ya kutoridhika, uchochezi na kushawishi utendaji wa kosa la jinai kati ya Februari 1 na 16, 2018, jijini Dar es Salaam.




Balozi wa Uingereza hapa nchini, Sarah Cooke (katikati), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa awamu ya pili ya mpango kabambe wa miaka mitano wa kusaidia asasi za kiraia nchini, uitwao 'Uwajibikaji Tanzania-ACT2', utakaogharimu shilingi bilioni 126, uliochini ya serikali ya nchi hiyo, kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa (DFID). Kulia ni Mkuu wa Ofisi wa DFID hapa nchini, Beth Arthy na Mkurugenzi Mtendaji wa Foundation for Civil Society (FCS), Francis Kiwanga. **PICHA: JOHN BADI**

# Utafiti takwimu mapato, matumizi kaya wakamilika

**Na Beatrice Moses**

Kazi ya kuorodhesha utafiti wa takwimu zinazohusisha mapato na matumizi ya kaya binafsi Tanzania Bara wa Mwaka 2017/18 imekamilika.

Akizungumzia kazi hiyo iliyogharimu Sh. bilioni 10 zilizotolewa na Benki ya Dunia, Meneja wa Takwimu za Jamii na Watu, Sylvia Meku wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), alisema hatua hiyo imekamilika licha ya wadadisi kukumbana na changamoto kadhaa.

"Changamoto hazikutukwamisha, tumekamilisha na tunarajia matokeo ya awali tutayatangaza kuanzia mwezi Machi mwaka huu, ikiwa yana takwimu za nchi nzima," alisema Meku wakati akizungumza na gazeti hili jana.

Alisema katika kazi hiyo ya uorodheshaji wa kaya ambayo imefanyika mikoa yote ya Tanzania Bara, wadadisi walikumbana na watu wakaidi ambao waligoma kutoa ushirikiano wa kutoa maelezo yaliyohitajika.

"Tulipokumba nao tulilazimika kutumia mbinu za ziada ili kufanikisha, ikiwamo kuwashirikisha viongozi wa vijiji au mitaa," alisema Meku.

Alisema kukamilika kwa kazi hiyo kutatoa nafasi nzuri ya kupata viashiria vya kupima hali ya umaskini nchini kuanzia katika ngazi ya kaya.

Utafiti kama huu mara ya mwisho ulifanyika mwaka 2011/12 ambao ulionyesha kuwa asilimia 28.2 ya Watanzania wanaishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya Msingi.

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania Bara wa Mwaka 2017/18, unafanywa na NBS kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na baadhi ya wadau wa maendeleo.

Utafiti huo ulihusisha kupata takwimu zinazohusu shughuli za kijamii na kiuchumi, mapato na matumizi, hali ya makazi na umiliki wa rasilimali katika ngazi ya kaya.

Kazi hiyo ilizinduliwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, Novemba 2017 ambako alibainisha kuwa utafiti huo utaiwezesha serikali kupima kiwango cha hali ya umaskini wa chakula, kipato na pengo baina ya matajiri na maskini kuanzia kipindi cha mwaka 2013 hadi sasa. Awali ilibainishwa kuwa utafiti huu utakusanya takwimu katika kaya binafsi 10,460 kwa Tanzania Bara kuanzia Novemba 2017 hadi Novemba 2018.

Mkurugenzi Mkuu wa NBS, Dkt. Albina Chuwa, awali alibainisha kuwa utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi utafanyika katika maeneo 754 yaliyochaguliwa kutokana na takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012.

# Raia 13 wa Ethiopia wanaswa shambani

**Na Rose Jacob,** MWANZA.

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linawashikilia raia 13 wa Ethiopia wakiwa wamejificha kwenye shamba la mkazi mmoja wa mtaa wa Nyaburogoya Kata ya Nyegezi jijini hapa.

Miongoni mwao, watano wamekutwa na hati za kusafiria zilizotolewa na Ethiopia zilizogongwa muhuri na Idara ya Uhamiaji ya Kenya, lakini bila kugongwa mhuri na idara hiyo nchini.

Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Jumanne Muliro, alisema watu hao walikamtwa Februari 13, mwaka huu asubuhi, kufuatia taarifa za kiintelijensia kutoka kwa raia wema, na kwamba walipofuatilia walikuta ni kweli kisha kuwakamata13, ambao walitambulika kuwa ni raia wa nchi hiyo.

"Tunachoendelea nacho kwa sasa ni kutaka kujua hawa watu wamefikaje hapa nchini, wamesafirije hadi kupita mpakani na ni nani mwenyeji," alisema Kamanda Muloro na kuongeza:

"Watakapobainika wanaowapatia mbinu za kuingia nchini bila vibali watachukuliwa hatua sitahiki za kisheria, ikiwamo kufikishwa kwenye vyombo husika."

Aidha, alisema kutokana na watu hao kutokuelewa lugha ya Kiswahili wala Kiingereza, utaratibu unafanyika wa kumtumia mkalimani ili kubaini sehemu wanayotoka na wanapokwenda.

"Tunawashikilia katika kituo kikuu cha Nyamagana, taratibu zinafanyika za kuwafikisha katika idara ya Uhamiaji kwa ajili ya hatua nyingine za kisheria," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, baada ya mkuu huyo wa mkoa kuzungumza katika hafla ya wateja wa CRDB wa mkoa huo, iliyoandaliwa na benki hiyo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yakubali kufanyia kazi mapendekezo kuboresha kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imesema itafanyia kazi matokeo ya utafiti na mapendekezo mbalimbali yatakayokwenda kusaidia kuboresha sekta ya kilimo ili kuendana na mabadiliko makubwa yanayoendelea katika sekta hiyo kwa sasa nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Tano la Sera za Kilimo jijini Dodoma, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, amesema kilimo kinakabiliwa na changamoto nyingi za kisera ambazo zinasababisha sekta hiyo kutopiga hatua na kufanya wakulima kubaki katika hali ya umaskini.

"Utafiti huu utasaidia kuboresha sera mbalimbali katika sekta hii na kupelekea hamasa kwa wadau wa kilimo na wakulima kukuza uzalishaji wa mazao wenye tija nchini," alisema Waziri Kairuki.

Alisema Serikali itaendelea kujenga mazingira wezeshi na endelevu ili kukuza sekta ya kilimo kwa kuboresha miundombinu ya barabara , reli na maji ili kuimarisha uzalishaji na ushindani wa mauzo ya bidhaa, yakiwamo mazao ya kilimo.

"Tutaweza kufikia malengo endapo tutakuwa na sera imara na zenye kutekeleza katika kukuza sekta ya kilimo ambayo ndio msingi wa uanzishwaji wa viwanda nchini," alisema.

Aliongezea kuwa Serikali inatambua jitihada za wadau wa kilimo kama

ASPIRES Tanzania katika kufanya mageuzi kwenye sekta ya kilimo kwa kuleta mapendekezo yatakayoboresha sera za sekta hii na kukifanya kilimo kupiga hatua.

"Nchi yetu imebarikiwa kuwa na maeneo mazuri ya uzalishaji wa mazao kwa uwapo wa ardhi, mvua za kutosha kwa ajili ya kilimo, hivyo ni kuboresha sera zetu ili tuzalishe kwa tija kwa matumizi ya ndani na nje ya nchi," alisema.

Waziri Kairuki pia alizitaja changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo ni pamoja na sheria zinazoongoza masuala ya kilimo na ambazo siyo rafiki kwa kilimo cha kibiashara, kuwapo kwa taasisi nyingi zinazodhibiti masuala ya kilimo na ambazo zinakinzana, na utitiri wa kodi na tozo mbalimbali kwenye biashara ya kilimo.

"Kupitia mpango wa kuboresha mazingira ya biashara utaondoa changamoto zilizopo na kuchochea mageuzi katika sekta ya kilimo na kumfanya mkulima kijijini kuwa na maendeleo na kupelekea nchini kupiga hatua kiuchumi," alisema Kairuki.

Alisema katika kutekeleza wa Mpango wa Kuendeleza Kilimo Awamu ya Pili (ASDP-2,) matokeo ya utafiti mbalimbali katika sekta ya kilimo yanahitajika ili kujua changamoto na namna ya kuzikabili ili kufanya mpango huu kutekeleza kwa vitendo.

Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alisema Wizara ya Kilimo inaendelea na utekelezaji wa ASDP-2 ili kukuza mnyororo wa thamani. "Matokeo ya utafiti tuliyapokea, tutakwenda kuyafanyia kazi kwa ngazi ya Wizara ili kufanya maboresho yatakayopelekea tija katika uzalishaji kuongeza na kuchochea viwanda kuanzishwa," alisema Mgumba

Alisema viwanda vinahitaji malighafi, hivyo kwa kuwa na mazingira mazuri ya uzalishaji mazao, kutapelekea kuwa na mazao yakutosha yatakayotumika kama malighafi katika viwanda vya ndani.

Naye Mshauri wa Sera za kilimo kutoka ASPIRES Tanzania, Prof. David Nyange, amesema utafiti mbalimbali wanaofanya una mchango mkubwa katika kukuza na kuendeleza kilimo nchini, hivyo ni jukumu la Serikali kuyafanyia kazi matokeo ya utafiti.

Wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo walikutana jijini Dodoma katika kongamano la siku tatu la kujadili maendeleo ya kilimo ili kukabiliana na changamoto inayodidimiza sekta hiyo.

# Watumishi wahukumiwa kutumia madaraka vibaya

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma, imewahukumu watumishi watatu wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji kwenda jela miaka 2 au kulipa faini ya Sh. milioni 3 kila mmoja kwa kosa la kutumia mamlaka vibaya kinyume cha kifungu 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11/2007.

Waliohukumiwa ni Hussein Rashidi (ofisa manunuzi); Ramadhani Nyamtema (mhasibu ukaguzi wa ndani) na Michaeli Sonyo (mweka hazina msitaafu) .

Hata hivyo, wote kwa pamoja walilipa faini na kuachiwa.

Hukumu hiyo ilotolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Flora Mtarania, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo.

Hakimu Mtarania alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali kwa washtakiwa hao ili liwe fundisho kwao na kwa watumishi wengine wenye tabia kama hiyo. Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi wanne na vielelezo sita ambavyo vilionyesha kuwa washtakiwa hao walitumia madaraka yao vibaya. Hakimu huyo alisema washtakiwa hao walitumia mamlaka yao vibaya kwa kuwezesha malipo kwa ajili ya kununua vipuri vya greda la Manispaa ya Kigoma/Ujiji lenye namba za usajili SM 8695, kabla ya vipuri hivyo kukaguliwa na kupokelewa kwa mujibu wa kanuni ya 242 (1) ya kanuni za manunuzi namba 446 ya mwaka 2013 ikisomwa pamoja na kanuni ya fedha ya 71 (1) ya kanuni ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

Aidha, Hakimu Mtarania alisema upande wa mashtaka uliwashtaki watu watano ambao ni Hemed Major, mfanyabiashara wa vipuri vya magari ambaye manispaa ilimpa kazi ya kuwapelekea vifaa vya greda kwa thamani ya Sh. 15,840,000, Wilfred Shimba, Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi, Hussein Rashidi, Ofisa Manunuzi, Ramadhani Nyamtema, Mhasibu Ukaguzi wa Ndani na Michael Sonyo, mweka hazina mstaafu wa manispaa.

Alisema katika hukumu yake upande wa mashtaka haukuthibitisha makosa dhidi ya Major na Shimba, na kuwa mahakama imewaona hawana hatia, hivyo imewaachia huru.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kigoma, Boniface Kamwesigile, aliomba mahakama hiyo itoe adhabu kali kwa washtakiwa hao kwa sababu kosa walilolifanya ni kushindwa kusimamia sheria na kanuni za fedha na manunuzi ya umma, hivyo kuisababishia serikali hasara.

Upande wa utetezi ukiongozwa na wakili wa kujitegemea Ignatus Kagashe na Sylvester Damasi, waliomba mahakama iwapunguzie wateja wao adhabu kwa sababu wana familia zinazowategemea.

Hakimu Mtarania alitupilia mbali utetezi huo na kuwataka washtakiwa wote watatu mtakwenda jela miaka miwili au kulipa faini ya Sh. milioni 3 kwa kila mmoja.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mapendekezo uboreshaji wa kilimo yafanyiwe kazi

**KIPINDI** hiki ambacho mkakati wa Tanzania kujenga viwanda kama njia ya kuelekeza kwenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, kumekuwapo na msisitizo wa kuboresha sekta ya kilimo.

Kimsingi, lengo ni kuhakikisha kuwa maendeleo ya sekta hiyo muhimu yatatoa sapoti kubwa kwa viwanda, kwa kuzingatia kuwa uwapo wa viwanda unategemea kilimo kwa ajili ya kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda hivyo.

Katika kuonyesha kwamba kilimo kina umuhimu mkubwa na wa kipeee kwa sasa, wataalamu wa sekta mbalimbali wakiwamo wachumi, watafiti na wa makundi mengine, wamekuwa wakihimiza serikali kuwekeza katika kilimo.

Wengi wao mbali na kutoa mapendekezo hayo, pia wamefanya utafiti mbalimbali na kuja na mapendekezo mengi yanayoonyesha vikwazo vya kukua kwa sekta hiyo na nini kifanyike kwa ajili ya maendeleo yake.

Kwa upande wake, serikali nayo imekuwa ikichukua hatua kadhaa za kuboresha sekta hiyo ikiwamo kuandaa majukwaa ya kujadiliana, kuongeza ajira kwa wataalamu wa kilimo husussan maofisa ugani, kuongeza bajeti ya wizara pamoja na kuwavutia wawekezaji wa nje kuja nchini kuwekeza katika sekta hiyo.

Wakati jitihada mbalimbali zikiendelea kufanyika, serikali imesema itafanyia kazi matokeo ya utafiti na mapendekezo mbalimbali yatayosaidia kuboresha sekta ya kilimo ili kuendana na mabadiliko makubwa yanayoendelea katika sekta hiyo kwa sasa nchini. Akizungumza kwa niaba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Tano la Sera za Kilimo jijini Dodoma, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, amesema kilimo kinakabiliwa na changamoto nyingi za kisera ambazo zinasababisha sekta hiyo kutopiga hatua na kufanya wakulima kubaki katika hali ya umaskini.

Katika kongamano hilo lililofanyika jijini Dodoma, Waziri Kairuki, alieleza kwamba utafiti huu utasaidia kuboresha sera mbalimbali katika sekta hiyo na kuleta hamasa kwa wadau wa kilimo na wakulima kukuza uzalishaji wa mazao wenye tija. Alisema serikali itaendelea kujenga mazingira wezeshi na endelevu ili kukuza sekta ya kilimo kwa kuboresha miundombinu ya barabara , reli na maji ili kuimarisha uzalishaji na ushindani wa mauzo ya bidhaa, yakiwamo mazao ya kilimo.

Aliongezea kuwa serikali inatambua jitihada za wadau wa kilimo katika kufanya mageuzi kwenye sekta ya kilimo kwa kuleta mapendekezo yatakayoboresha sera za sekta hii na kukifanya kilimo kupiga hatua.

Ni jambo jema kuwapo mijadala ya aina hii kwa sababu inakutanisha serikali na wadau kubadilishana mawazo pamoja na uzoefu. Aidha, inakuwa rahisi kwa wadau kutoa mapendekezo, ushauri, kukosoa na maoni yao yenye lengo la kuboresha.

Kinachotia moyo ni kuwa serikali imekubali kufanyia kazi maoni hayo ya wadau, hivyo tunaamini kuwa kwa kufanya hivyo changamoto mbalimbali zitatafutiwa ufumbuzi na kuwezesha kuboreshwa kwa sekta ya kilimo nchini.

Tunakubali kuwa changamoto haziwezi kukosekana mahali popote, isipokuwa katika suala la kilimo, Tanzania kuna mazingira bora ikiwamo kuwa na maeneo mazuri ya uzalishaji wa mazao kutokana na uwapo wa ardhi, mvua za kutosha kwa ajili ya kilimo.

Kwa kuwa serikali imeahidi kufanyia kazi mapendekezo hayo pamoja na utayari wa kuboresha sera zetu ili kuzalisha kwa tija, tunatarajia kuwa kilimo kitaboreshwa na kutoa mchango stahiki katika uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tuungane katika vita ya lishe

Na Mary Geofrey

**LISHE** duni hudumaza ukuaji wa watoto kimwili na kiakili. Pia, inamuathiri ukuaji wa akili yake, hivyo kupunguza uwezo wa kufanya vizuri shuleni na pia hupunguza ufanisi katika maisha ya utu uzima.

Takwimu zilizotolewa na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), nchini kuna tatizo kubwa la utapiamlo na udumavu kwa watoto wachanga na wadogo, licha ya kuwapo juhudi za kupambana.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa inadumaza uwezo wa watoto kufikiri vyema na mwisho kuzalisha taifa la wenye uelewa mdogo, serikali imetekeleza mikakati kadhaa.

Mosi ni kuimarisha huduma za lishe kupitia nyanja kadhaa: Matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto chini ya miaka mitano, kwa kutumia vyakula dawa ikiwamo matumizi ya maziwa maalumu ya kopo(F.75 na F.100).

Pia, serikali inaendesha kampeni za kutoaji vidonge vya nyongeza ya vitamini A na dawa za kutibu minyoo kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5, mara mbili kwa mwaka katika, mwezi Juni na Desemba, ili kuwakinga na upofu na upungufu wa kinga mwilini.

Hadi Juni mwaka jana, asilimia 96 ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano walipatiwa na serikali vidonge hivyo, pia wazalishaji chumvi zinazoongeza madini joto, ili kutokomeza upungufu wa madini joto mwilini kwa watoto wanaozaliwa, wakiwa na matatizo ya akili na ulemavu wa viungo.

Serikali inaviwezesha viwanda vinavyosindika vyakula kuongeza virutubishi vya vitamin na madini katika vyakula vinavyosindikwa viwandani, ikiwamo mafuta ya kula, unga wa mahindi na ngano.

Jingine, inaimarisha huduma ya ufuatiliaji wa ukuaji maendeleo ya watoto kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya ya mama na mtoto nchini, ikiwamo kupima uzito, kuanzisha vitabu vipya vya ufuatiliaji vinavyobaini utapiamlo mapema zaidi, tofauti na awali.

> **Pia, serikali inaendesha kampeni za kutoaji vidonge vya nyongeza ya vitamini A na dawa za kutibu minyoo kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5, mara mbili kwa mwaka katika, mwezi Juni na Desemba, ili kuwakinga na upofu na upungufu wa kinga mwilini.**

Serikali imeimarisha utoaji elimu ya lishe kwa umma kwenye jamii, kwa kutumia kitendea kazi cha 'Mkoba wa Siku 1,000' unaohamasisha matunzo bora ya mjamzito na mtoto tangu anapozaliwa, hadi kutimiza miaka miwili.

Aidha, inawezesha vituo vya utafiti wa kilimo kurutubisha mazao kibaiolojia, vikiwamo viazi lishe na mahindi lishe, kuongeza kiwango cha virutubisi madini na vitamini.

Serikali pia, imeongeza bajeti ya lishe kwa kuziagiza halmashauri nchini kutenga Shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano, ili zigharamie lishe. Mwaka 2018 jumla ya bilioni 11 zilitengwa.

Wakuu wa Mikoa, ndiyo wanaoratibu na kusimamia kwa ukaribu utoaji uduma za lishe katika mikoa wanayoiongoza.

Katika juhudi hizo zinazofanywa na serikali, jamii bado ina mwamko mdogo wa uzingatiaji lishe kwa watoto na wajawazito.

Wajawazito wengi wako katika imani potofu, mfano wanasema mjamzito akila mayai, atazaa mtoto asiye na nywele kichwani. Hiyo inamkosesha virutubishi vilivyopo kwenye mayai.

Pia, kuna imani ya wazazi wa watoto, kuwa miaka ya nyuma, hawakula vyakula vizuri, lakini walikuwa na afya njema hadi sasa, kumpa imani mjamzito au mzazi kutojali lishe ya mtoto.

Ni jukumu letu sote kuwa makini kuzingatia kanuni za afya hasa suala la lishe ili kujenga taifa imara lisilo na 'mambumbumbu.'

Ni vyema kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali chini ya TFNC katika kuhakikisha wanatoa elimu kwa jamii.

Afya ya mama na mtoto, ni jukumu letu sote kuwa na wajibu wa kumuelimisha mzazi, kumpa mtoto wake vyakula vinavyoendana na umri na kuzingatia ratiba.

Wazazi na walezi, ni muhimu kuachana na imani na tabia za asili zinazokinzana na zama hizi zenye kila aina ya teknolojia ikiwamo maziwa yenye virutubishi, vidonge lishe na vinavyomfanya kukua katika mfumo ulio salama.

BARUA/MJADALA

# Tunaitumiaje Valentine?

**Mhariri,**

*JANA ilikuwa Siku ya Wapendanao, maarufu kama Valentine. Kupitia ushuhuda nina shaka juu ya namna gani sote tunabeba tafsiri sahihi ya suala hilo katika usahihi unaotakiwa.*

*Nikirejea maadhimisho ya jana na huko tunakoenda, kwa miaka mingi umma umekuwa ukiamini tafsiri ya dhana hiyo, inatokana na mapenzi ya uhusiano wa mwanamume na mwanamke na si nje ya hapo.*

*Nasikitika kubaini kuanzia vyombo vya habari, hadi mitandao ya kijamii, wote walijikuta katika dhana hiyo ya mapenzi ya bwana na bibi. Niushirikishe umma kuhoji, je hilo ni sahihi?*

*Ukweli ni zaidi ya hapo. Tafsiri yake halisi iko pana zaidi, kwa maana ya upendo uko kuanzia nyumba za ibada, kwenye familia na maeneo kama hayo.*


*Mapenzi ya uhusiano huo yanaonekana katika wiki nzima ndio yaliyotawala Valentine hata watu kusahau tafsiri ya msingi. Hii binafsi ninaiona ni kasoro kubwa inayopaswa kufanyiwa kazi.*

*Nini kifanyike kulirekebisha hilo. Naamini kila sehemu ambayo imeumbika kuwa ya jumuiya. Hapo nimaanisha katika mjumuiko wa sehemu za kazi, nyumba za ibada, mikusanyiko ya burudani, jumuiya za kimasomo; shule na vyuoni.*

*Tukihubiri upendo na kupendana katika maeneo hayo, inakuwa tumepiga hatua kubwa sana kijamii na kusonga mbali tena kwa hatua ndefu zaidi.*

**Mzangeli Juma,**
**Pugu,**
**Kinyamwezi,**
**Dar es Salaam.**

# Vilio vya ushuru serikali za mitaa visikilizwe




**Na Yasmine Protace**

**MWONGOZO** unapoandaliwa na ukasimamiwa vizuri utaleta matunda katika sehemu husika.

Kuleta matunda ni pale sheria inayofuatwa ipo katika mwongozo na haitakiwi kupindishwa na kusababisha kuleta malalamiko kwa jamii.

Umuhimu wa ulipaji kodi, ni moja ya sehemu ya kuchangia kuwapo maendeleo kwa sehemu husika.

Hata Rais, Dk.John Magufuli, amekuwa akisisitiza kodi zilipwe, ili kuliongezea taifa mapato na ukwepaji kodi, unavyodidimiza maendeleo si kwetu, bali katika nchi yoyote ile duniani .

Anasizitiza kwamba, kila anayeyafanya ununuzi, lazima awajibike kuchukua risiti yake, ili mfanyabiashara aonekane anachokizalisha katika biashara yake na awajibike na kodi.

Rais Magufuli aliwakumbusha wafanyabiashara wadogo, kwamba wasirubuniwe na wenye maduka ya biashara kubwa, kwa kuchukua bidhaa katika maduka yao, ili waziuze nje kinyemela.

Anasema, kufanya hivyo ni kumsaidia mwenye duka kukwepa kulipa kodi, kwani alisamehe kodi katika baadhi ya maeneo, lengo ni kuhakikisha huduma hizo zinanusurika na mizigo kiuchumi.

Pamoja na kuzungumzia kodi, kumekuwapo tozo na ushuru, ambazo zinasimamiwa na halmashauri mbalimbali katika ngazi ya serikali za mitaa na zimeonyesha kumbebesha mzigo mwananchi wa kipato cha chini.

Ukiangalia sehemu kubwa ya wanaofanya biashara ndogo ni wanawake na hao hao ndio wamejikuta wanaobeba mzigo wa kodi, kutokana na uhalisia wa biashara zao, ingawa tunajua nia ya mamlaka daima imekuwa nzuri.

Kinamama hao wa aina ya biashara kama vile soda, wanauza hata kwa siku hawamalizi kreti mbili, lakini wanatakiwa kulipa Sh. 5,090 za ushuru wa taka.

Hivi karibuni asasi ya TGNP Mtandao, iliandaa semina za Jinsia na Maendeleo( GDSS), ambazo wananchi kutoka wilaya za Temeke, Ilala, Kinondoni na Ubungo, walishiriki kujadili uhalisia wa kodi, tozo na ushuru, jinsi zinavyochangia kuleta maendeleo.

Katika ushuru wa taka, ilionekana kuwapo tofauti kubwa na wananchi wamedai ushuru wa taka umekuwa kero kwao, kutoka eneo moja hadi jingine.

Jamii inalalamika kuwa ushuru unatozwa bila ya kujali vipato vya wananchi na katika kaya, ushuru wa taka umekuwa ukiwachanganya wengi katika ulipaji.

Imeelezwa kuwa, katika mikutano ambayo wananchi wameshirikishwa, wanaambiwa kila nyumba italipa ushuru wa Sh.3,000 za taka kila gari linapoondoa taka.

Wananchi wanasema kwa nyakati tofauti, kuwa gari linapita mara mmoja kwa wiki, lakini cha kushangaza taka wanadaiwa Sh. 5,000 au zaidi.

Kibaya zaidi, wanasema pamoja na kutoa risiti, kuna nyumba ambazo wapangaji wanafunzi na vyumba vingine hawazalishi taka, lakini wanatozwa kila chumba Sh. 3000 hadi Sh.5000 na asiyelipa anatozwa faini, hata kufikishwa mbele ya sheria.

Ni malalamiko yanayofika mbali, kwamba wakazi sasa wanadai mwongozo uandaliwe na mamlaka husika, wapunguziwe ushuru uliopo.

Kuna swali linaloenda mbali, kwamba hata wanaouza CD nao wanalipishwa ushuru wa Sh. 5000, wakati wao hawazalishi taka nyingi kamwe.

Dai kuu ni mwongozo uandaliwe kudaiwa ushuru unaoendana na taka zinazozalishwa. Pia, mbali na wauza CD, kuna wauzaji soda katika maduka ya vinywaji, wanalia kutozwa Sh. 5000 kwa kila gari la taka linapopita, wakati hawazalishi taka zaidi ya vizibo.

Wanasema vizibo wanavyowafungulia wateja haviendani na ushuru wanaoulipa. Ni kilio kinachoangukia katika mamlaka husika kurekebisha miongozo, ili kuwaondolea kero ya kulipa ushuru mkubwa.

Ni kilio kinachosema mtu akikataa kulipa kiasi hicho cha fedha katika baadhi ya sehemu, anaangukia faini ya fedha nyingi.

Biashara nyingi ndogo zimekuwa zikifanywa na kinamama wanaojikuta wanabebeshwa mizigo mikubwa ya ushuru, wakati kipato chao cha ujasiriamali kiko chini zaidi.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**




**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Tahadhari yatolewa mvua kubwa

INATOKA UK. 3

Zanzibar, Arusha, Manyara, Kilimanjaro na baadhi ya maeneo ya kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro, mvua za masika zinatarajiwa kuanza katikati ya wiki ya mwisho ya mwezi huu.

Alisema ni vyema kwa mamlaka husika hasa katika sekta za kilimo, uvuvi, ujenzi na afya kuchukua tahadhari kutokana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mvua.

"Kwa sekta ya kilimo, mikoa itakayopata mvua juu ya wastani ni vyema wakaangalia kulima mazao yanayostahimili unyevu nyevu mwingi kutokana mvua nyingi.

Lakini pia kwa mamlaka ya miji, huduma za majisafi na majitaka zinaweza zikaathiriwa, ni vyema mifumo ya njia za kupitisha maji ikaimilishwa kuepuka mafuriko na athari nyingine," alisema.

Alisema tahadhari ya magonjwa ya mlipuko kutokana na matarajio ya uwapo kwa mvua nyingi, inapaswa kuchukuliwa katika sekta ya afya.

"Upande wa wenzetu wachimbaji wa madini, wanapaswa kuchukua tahadhari ya maporomoko ya ardhi kwenye migodi," alisema.

Alisema TMA itaendelea kutoa mrejesho wa mvua katika utabiri wa siku 10 na siku tano watakaokuwa wakiutoa na kuwataka wananchi kufuatilia taarifa kwenye vyombo vya habari.

Mvua za masika zimekuwa zikisababisha mafuriko karibu kila mwaka kwenye maeneo ya mabondeni ambayo licha ya serikali kupiga marufuku watu kuweka makazi, bado yanaendelea kuwa na ujenzi holela.

# Mawaziri wanusuru wakazi 133 kuhamishwa bwawani

INATOKA UK. 3

la Wami/Ruvu kusitisha zoezi hilo mpaka Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Mbarawa) atakapotoa muongozo wa utaratibu gani utatumika kuwahamisha wananchi hao. Aliongeza maeneo waliochagua kutembelea na kujifunza ni yenye changamoto kubwa ya migogoro ya mgongano ya sheria za ardhi, maji na makazi ya wananchi.

"Timu hii aliyoituma Rais Magufuli ni timu bora ambayo itakuja na majibu ambayo itamkabidhi ripoti yetu wiki ijayo na ataangalia kama sheria hizi zinahitaji maboresho," alisema.

Alisema baada ya kutembelea bwawa hilo, wanatarajia kutembelea Bonde la Kilombero, Mbarari, Uvinza, Serengeti, Ilemela, Bwanga na pori la akiba Maswa.

Alisema serikali ya mkoa wa Morogoro ihakikishe inadhibiti na kusitisha utoaji wa vibali vya makazi kwa wakazi ambao wanazunguka bwawa hilo, huku wakisubiri hatua zaidi ambazo serikali itaamua juu ya wakazi hao.

"Mkuu wa mkoa wa Morogoro hakikisha unasitisha kutoa vibali vya makazi katika eneo hili na maeneo mengine yenye mgogoro mpaka hapo Waziri wa Maji atakapotoa agizo lake juu suala hili," alisema Lukuvi.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Stephen Kebwe, alihakikishia kamati hiyo kuwa imetenga maeneo ya kuwahamishia wakazi wa vijiji hivyo, hivyo hakuna tatizo juu ya sehemu ya makazi mapya.

Alisema kuwa wakazi wa eneo hilo walikuwa wamesimamisha shughuli za ujenzi na serikali huwa hailipi watu mara mbili kwasababu wakazi hao walishalipwa kupisha uendelezaji wa bwawa hilo.

"Tumewataarishia sehemu ambayo watalipia pesa kidogo kwa kuwa serikali haiwezi kulipa fedha mara mbili kwa sababu tulishawalipa ila kuna baadhi yao waliuza maeneo yao kwa watu wengine," alisema.

Kwa upande wa wananchi wanaokaa kuzunguka bwawa hilo waliishukuru serikali kwa kusitisha zoezi hilo kwa kuwa hapakuwa na pa kwenda kutokana na kutokupewa eneo mbadala la kwenda.

Ismail Juma, alisema walipewa notisi ya kuhama eneo hilo miezi miwili iliyopita, lakini hawakuelezwa wapi watahamia.

Naye Ally Lugendo, alisema yeye ameishi eneo hilo kwa miaka 45 sasa hajawahi kusikia suala la kulipwa fidia wananchi wa kijiji hicho ili wahame. Mwajuma Mbega, alisema madhara yatakayotokea wakati bwawa likipasuka ni mabaya, hivyo aliiomba serikali kuwahamisha eneo hilo na kuwapatia lingine ambalo lina huduma zote za kijamii.

# Mpangaji aishi maisha ya ajabu

INATOKA UK. 2

gari la kubeba taka hizo na kuzipeleka dampo kwa kuwa hawawezi kuvumilia hali hiyo.

Kwa mujibu wa Fugame walifanikiwa kupata gari na kuzoa taka hizo awamu ya kwanza na wamebakiza uchafu mwingine ambao utamaliziwa leo.

Naye Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Madenge, Hamis Digega, alisema mpangaji huyo ana umri unaokadiriwa miaka 68 na hana dalili za kuonyesha kwamba ana ugonjwa wa akili.

Digega alisema anashindwa kufahamu kilichompata mwanamume huyo ambaye ana elimu ya uhasibu hadi akaamua kuishi katika taka hizo. "Si kwamba ana shida ya fedha kwa sababu huwa anawasaidia wazee wa hapa. Ni mtu mwenye uwezo wake lakini ndugu zake wakija kumtembelea anawaambia nisubirini hapo nje hivyo hawaingii ndani," alisema Digega

Omary Said ambaye ni jirani wa mpangaji huyo alisema mara kwa mara huwa anamwona nyumbani hapo ingawa hajawahi kuingia ndani ni kwake na kwamba ameshangaa kumwona mpangaji huyo akishi katika mazingira hayo yenye jalala ndani.

"Baba mwenye nyumba amethibitisha kwamba huwa anamwona akizoa takataka na kutoa nje lakini tunashangaa kuzikuta humu ndani," alisema.

Alisema mpangaji huyo kwa mwonekano na tabia zake ni mtu mwenye busara zake , hekima na hana kawaida ya kugombana na watu na huwa anatoa msaada kwa majirani pale inapotokea.

"Si kwamba ni mtu mhuni mhuni useme kuwa anakuja na takataka chumbani kwake hapana.. Huwa anakuja na mifuko yake ya chakula anaingia ndani anakula," alisema.

Alisema anamfahamu mpangaji huyo tangu akiwa kijana na kwamba ni mtanashati na mtu ambaye hajakiona chumba hicho hawezi kuamini kwamba anatoka mtu ambaye huwa anajipenda na kuvaa vizuri. Mmoja wa majirani alisema mtu huyo amepanga katika nyumba ya Omary Said kwa takriban miaka 25 na anaishi peke yake na kwa sasa ni mstaafu anayefanya shughuli ndogo ndogo za kuondoka alfajiri na kurudi jioni.

# Chadema wamjia juu Lugola

INATOKA UK. 2

Watanzania wawaamini. Lazima wajue Watanzania wanaowaambia haya wana akili timamu," alisema.

Kigaila alisema Lugola anachotaka kuwaeleza Watanzania ni kwamba hawajachunguza kupotea kwa Ben Saanan, Azory Gwanda na miili iliyokuwa ikiokotwa ikielea Bahari ya Hindi kwa sababu wanawasubiri wahusika warudi.

"Kama huo ndio msimamo wa serikali wanataka hadi waathirika warudi ndipo wachunguze, wako waliorudi mbona hawachunguzi, MO Dewji na Roma Mkatoliki si walitekwa wakarudi? Kama kurudi ndiyo kufanya uchunguzi, je, wameshachunguza na kujua waliowateka?" Alihoji. Alisema haiwezekani serikali yenye wajibu wa kulinda raia na mali zake, ikakwepa wajibu wake wa kuchunguza uhalifu.

Alisema walitakiwa kuchunguza maganda yaliyookotwa eneo la tukio ni ya gani ya bunduki, imetengenezwa wapi na kama inamilikiwa na mtu binafsi au serikali. Pia chama hicho kimemtaka Waziri Lugola aeleze wamechukua hatua gani kwa kampuni ya ulinzi iliyokuwa ikilinda kwenye eneo la nyumba alikopigwa risasi Lissu.

Kadhalika, walimtaka waziri huyo aeleze mpaka sasa wameshakamata watu wangapi na kuwahoji kuhusika na tukio hilo.

**ALICHOKISEMA WAZIRI LUGOLA ARUSHA**

Akizungumza katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha juzi, Lugola, alisema uchunguzi wa shambulio dhidi ya mbunge huyo umefanyika, lakini hawawezi kufungua kesi mahakamani bila kumhoji mlalamikaji (Lissu) na dereva wake ambao alisema ni mashahidi muhimu. "Hakuna hata siku moja polisi wakashindwa kuchunguza kesi ya Lissu, lakini ili kesi ifike katika hatua ya kwenda mahakamani, ni lazima yeye na dereva wake waje. "Upande wa mashtaka ndiyo wenye dhamana ya kuthibitisha ushahidi, hivyo lazima wajiridhishe kabla ya kufungua kesi mahakamani ambapo wanatakiwa kuthibitisha kesi hiyo pasipo kuwa na shaka.

"Kupeleka hii kesi bila kuwahoji walalamikaji (Lissu na dereva wake), tutaonekana kituko mahakamani," Lugola alisema.

Waziri huyo pia alihoji maswali kadhaa ambayo alidai kuwa ni muhimu yakapata majibu kutoka kwa walalamikaji.

Lugola alihoji kwa nini dereva wa Lissu hakwenda moja kwa moja sehemu yenye usalama kama eneo la Bunge au kituo cha polisi, ilhali kabla ya shambulio hilo, alidai kuona gari likiwa linawafuatilia kwa nyuma. "Wakati shambulio likifanyika, kama wanavyodai risasi zilirushwa ovyo ovyo, iweje zipekeche mguu wa kulia wa Lissu pekee bila kumgusa dereva na hata kiboksi kinachokuwapo katikati ya siti ya abiria na dereva kisitobolewe kwa risasi?

"Kwa nini risasi ziende mguu wa kulia tu na siyo kwenye miguu yote na kale kaboksi hakajapigwa kwa risasi isipokuwa mguu wa kulia wa Lissu?" Lugola alihoji.

Waziri huyo pia alisema kama Lissu na dereva wake waliowaona washambulizi wao, wanapaswa kueleza kama walikuwa ni wanawake au wa kiume, wafupi au warefu, maji ya kunde au weusi.

Lugola pia alidai majengo yote ya Wakala wa Majengo (TBA) Dodoma, likiwamo alimokuwa akikaa Lissu 'Site One', hakuna hata moja lililofungwa kamera za usalama (CCTV), hivyo madai ya Lissu kuwa kamera hizo ziliondolewa siku moja baada ya shambulio hilo ni uongo.

# Wambura akwaa kisiki

INATOKA UK. 3

Mawakili wa Serikali George Barasa, Moza Kasubi na Imani Mitumezizi, uliomba mahakama kutupilia mbali hoja za utetezi kwamba hazina mashiko.

Katika kesi ya msingi, shtaka la kwanza ilidaiwa kuwa Julai 6, 2004 mahali pasipojulikana jijini Dar es Salaam, mshtakiwa akiwa na nia ya kutapeli alighushi barua yenye jina la E. Maganga Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Jeck System Ltd.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alighushi barua hiyo akidai TFF irejeshe mkopo wa Dola za Marekani 30,000 kwamba alilikopesha shirikisho hilo, huku akijua ni uongo.

Shtaka la pili, Julai 6, 2004, Wambura aliwasilisha TFF nyaraka ya kughushi akionyesha kwamba barua hiyo imeandikwa na E.Maganga, Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Jeck System Ltd kuwa alilikopesha shirikisho hilo Dola za Marekani 30,000.

Katika shtaka la tatu mpaka la tano, Juni 17, Agosti 19 na Julai 31, 2015, ofisi za TFF zilizoko Ilala, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alijipatia Sh. milioni 14 kama malipo ya mkopo na riba ya Dola za Marekani 30,000, huku akijua ni uongo.

Kasubi alidai katika shtaka la sita mpaka la 10, katika tarehe tofauti ofisi za TFF, mshtakiwa alijipatia Sh. 61,902,200 kama malipo ya mkopo na riba ya Dola za Marekani 30,000, huku akijua ni uongo.

Jamhuri uliendelea kudai kuwa katika shtaka la 11 mpaka la 15, katika tarehe tofauti ofisi za TFF, mshtakiwa alijipatia Sh. 35,095,424 kama malipo ya mkopo na riba ya Dola za Marekani 30,000, huku akijua ni uongo.

Shtaka la 16, ilidaiwa kati ya Agosti 15 na Oktoba 21, 2014 katika ofisi TFF, mshtakiwa alitakatisha Sh. 25,050,000 kutoka katika shirikisho hilo, wakati akijua fedha hizo ni zao la kughushi.

Shtaka la 17, ilidaiwa kati ya Mei 16 na Oktoba 21, 2015 katika ofisi za TFF, mshtakiwa alitakatisha Sh. 75,947,924 kutoka katika shirikisho hilo, wakati akijua fedha hizo ni zao la kughushi.

Barasa alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

**HABARI KITAIFA**

# Sifa za mwanamke kiongozi bora zatajwa

**Na Yasmine Protace**

IMEELEZWA kuwa sifa za mwanamke kuwa kiongozi ni lazima ajifunze na kupata utaalamu, ili awe kiongozi bora.

Hayo yalisemwa na Katibu wa Ubalozi wa Finland, nchini Elina Kalkku, katika mjadala uliokuwa ukizungumzia wanawake na uongozi, ulioandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) jijini Dar es Salaam.

Katika mada iliyoandaliwa na TGNP Mtandao juu ya wanawake na uongozi, klabu za shule za msingi na sekondari za jijini Dar es Salaam walishiriki katika mjadala huo.

Mbali na wanafunzi, pia baadhi ya wabunge na madiwani wa viti maalum wa Mkoa wa Dar es Salaam walishiriki kuchangia mada juu ya wanawake na uongozi.

"Sifa za kuwa mwanamke kiongozi lazima kujifunza na kupata utaalamu ili uweze kuwa kiongozi bora," alisema Kalkku.

Akizungumzia Finland, alisema masuala ya usawa wa kijinsia nchini humo yalianza mwaka 1906, na kwamba ushirikiano wa wanawake ulileta mabadiliko makubwa, hali iliyosababisha nchi hiyo kuwa ya kwanza duniani na kuwa na wabunge wanawake 19.

Alisema haikuwa rahisi wanawake kukubalika kushika madaraka miaka ya nyuma na kwamba wazazi nao walichekwa kutokana na watoto wao wa kike kugombea nafasi za uongozi, lakini baadaye walifanikiwa kuleta mabadiliko. Aliongeza kuwa masuala ya jinsia bado ni changamoto katika baadhi ya nchi, lakini hawakukata tamaa kugombea nafasi za uongozi.

Alisema kipindi walipoingia bungeni wanawake waliyafanyia kazi maeneo ya afya ya mama na mtoto, ikiwamo suala la elimu.

Aliongeza kuwa umoja na mshikamano wa wanawake ulisaidia kuleta mchango mkubwa katika nchi yao na kuwa wanaume walipokwenda kupigana vitani, wanawake walifanya kazi za viwandani na kufanikisha kuchangia pato la taifa.

Alisema wanawake walisaidia mambo mengi katika maendeleo ya nchi ikiwamo suala la elimu.

Kalkku alieleza kuwa Wizara ya Mambo Nje ilipoanzishwa, mabalozi wa kuiwakilisha nchi hiyo nje wote walikuwa wanaume, lakini kwa sasa mabalozi ni asilimia 50 kwa 50.

Alisema umoja wao uliwawezesha kupatikana rais mwanamke, spika wa bunge mwanamke na waziri mkuu alikuwa mwanamke.

Alisema Finland hakuna wabunge viti maalum, lakini katika kamati zilizopo wanahakikisha wanawake wapo kwa asilimia 40.

Kalkku katika ziara yake ya kutembelea ofisi za TGNP Mtandao na kushiriki katika mjadala wa wanawake na uongozi aliongozana na balozi wa Finland nchini, mratibu mkuu wa balozi, mwakilishi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa- Kitengo cha Wanawake (UN Women) na maofisa ubalozi wa Finland nchini.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu wenye Ulemavu), Stella Ikupa (kulia), akipata maelezo kwa lugha ya alama kutoka kwa mwanafunzi mwenye uziwi wa darasa la saba katika Shule Maalumu ya Viziwi Dodoma, Eliabi Chilongola, kuhusu teknolojia aliyoivumbua ya umwagiliaji, alipokuwa katika ziara kukagua utekelezaji wa masuala ya watu wenye ulemavu mkoani humo jana. **PICHA: OWM**

# Kilimo cha migomba, mananasi chapata msukumo

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA iko katika nafasi nzuri ya kuzalisha kwa wingi mimea ya migomba na mananasi endapo wakulima watatumia miche asilia inayozalishwa kwa njia ya maabara na Kampuni ya Kilimo Organo nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Ammar Mussaji, alisema miche inayotengenezwa na kampuni yake ni asili na inakidhi vigezo vya soko la ndani na nje, kwa kuwa haina magonjwa.

"Ni nafasi pekee kwa wakulima wa ndani kutumia miche hii ambayo haiwezi kuharibiwa na magonjwa na mkulima hatapaswa kutumia mbolea ya aina yoyote na ubora na uhakika mazao ni mkubwa," alisema Mussaji.

Mussaji alisema maabara yake ni ya kisasa na pia ina uwezo wa kuzalisha miche zaidi ya milioni saba kwa mwaka na kuweza kuchochea uzalishaji na kuchangia kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo nchini.

## Tarime, Rorya waelimishwa bidhaa ubora

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limeendelea kutoa elimu kwa wananchi katika wilaya za Tarime na Rorya juu ya umuhimu wa kununua bidhaa zilizothibitishwa ubora wake na shirika hilo na jinsi gani wajasiriamali wanaweza kupata leseni ya TBS bila gharama yoyote.

Kampeni hiyo ya elimu kwa umma imefanyika maeneo ya Soko jipya la REBU, Stendi ya Tarime Mjini, mnada wa Mtana na maeneo mengine ya Halmashauri ya Mji na Wilaya, ambapo wananchi walijitokeza kupata elimu sambamba na ufahamu wa masuala mbalimbali yahusuyo ubora wa bidhaa.

Kwa upande wake Ofisa Udhibiti Ubora, Mhandisi Paul Ndege, aliwakumbusha wananchi kuwa vita dhidi ya bidhaa hafifu sio ya TBS pekee bali ya kila mtu, hivyo, wasisite kutoa taarifa kupitia mawasiliano waliyopewa pale wanapogundua uwapo wa bidhaa hafifu katika soko lao na kuhakikisha wananunua bidhaa zilizothibitishwa na TBS.

Pia, shirika lilitoa semina kwa wajasiriamali wanaojihusisha na bidhaa mbalimbali kama nafaka, sabuni, maziwa, asali na unga wa lishe, kuhusiana na utaratibu wa kupata leseni ya kutumia alama ya ubora ya TBS na kuweleza kwamba huduma hiyo itatolewa bure kwa wajasiriamali wadogo.

Wajasiriamali wengi walieleza kuwa wamefurahishwa na elimu waliyoipata na kulishukuru shirika hilo, wakisema elimu hiyo itawapa matokeo yenye tija kwenye shughuli zao za uzalishaji.

# Halmashauri 22 zakwama makusanyo kodi ya ardhi

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

KAIMU Kamishna Msaidizi wa Ardhi Kanda ya Ziwa, Biswalo Makwasa, amesema serikali haijafikia malengo ya ukusanyaji wa kodi za ardhi na pango katika halmashauri 22 za mikoa ya kanda ya ziwa kama iliyokuwa imekusudia kukusanya kiasi cha Sh. 11,200,000,000.

Biswalo Makwasa alisema hayo katika uzinduzi wa mpango mkakati wa ukusanyaji kodi za pango la ardhi uliofanyika jijini hapa.

Alisema hadi kufikia Januari 31, mwaka huu halmashauri hizo zilifikia lengo la serikali la ukusanyaji wa kodi hizo ambazo mpaka sasa zimekusanya Sh. bilioni 5,191,511,136.45 sawa na asilimia 46 ya lengo la ukusanyaji huo.

"Serikali tulivyokuwa tumekusudia malengo yetu ya ukusanyaji kodi za ardhi na pango ni kukusanya kiasi hicho cha fedha kutoka halmashauri hizo, lakini tumeshindwa kufukia malengo kwa wakati mpaka sasa," alisema Makwasa.

Alisema kuwa Mkoa wa Mwanza lengo la ukusanyaji kodi katika halmashauri za wilaya ilikuwa kukusanya Sh. 7,441,400,000, lakini hadi kufikia Januari 31, mwaka huu, makusanyo yalikuwa ni Sh. 3,849,393,590.87 na hivyo kushindwa kufikia malengo yake.

Alisema katika sekta ya ardhi bado inakabiliwa na changamoto nyingi zikiwamo za migogoro ya ardhi kwa wananchi pamoja na wataalamu kushindwa kupimia wananchi viwanja kwa wakati kutokana na ukosefu wa fedha za kutolea huduma hiyo.

Hata hivyo, alisema serikali ina mpango kabambe wa kuhakikisha migogoro ya ardhi kwa wananchi inatoweka, ikiwamo kuwapimia viwanja vyao na kuvirasimisha ili kuondoa kero hiyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kilimo Organo, Ammar Mussaji, akitoa maelezo kwa waandishi wa habari kuhusu wanavyotunza miche kwenye moja ya eneo la kuhifadhia miche ya migomba na mananasi ndani ya maabara ya kisasa iliyoko Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Kijiji chapata ukombozi wa maji miaka 40

**Na Lilian Lugakingira,** MISSENYI

WANANCHI wa vitongoji vya Bitulage, Mtakuja na Kigarama katika kijiji cha Nyankere, Kata ya Mabare wilayani Missenyi mkoani Kagera, ambao wameishi takribani miaka 40 wakitumia maji ya bwawa, sasa wameondokana na adha hiyo baada ya kukabidhiwa mradi wa maji.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya kukabidhiwa mradi huo wa maji kijijini hapo, uliofadhiliwa na wadau wa maendeleo kutoka Shirika la World Vision Tanzania Kanda ya Kagera, kupitia mradi wa Missenyi, walieleza baadhi ya changamoto zilizokuwa zikiwakabili ikiwamo kutembea umbali mrefu kufuata maji ya bwawa.

Wananchi hao akiwamo Nusura Mudrikati, mkazi wa kijiji hicho alisema kuwa, changamoto ya upatikanaji majisafi na salama kwa miaka yote imekuwa ikiwatesa kwa kuwa wananchi wa vitongoji vyote vitatu walitegemea kupata huduma hiyo kutoka katika bwawa moja pekee. Mudrikati alisema kuwa kinamama na watoto ndiyo waliteseka zaidi maana walilazimika kutembea umbali wa takribani kilomita 25 kutafuta maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, huku akidai kuwa afya zao ziliathirika kutokana na matumizi ya maji yasiyo safi na salama.

"Ukitembea kila kaya utakuta wengi wakilalamika kuumwa matumbo ya kuhara, magonjwa ya ngozi, na tatizo ni maji tunayotumia maana hata mifugo wanakunywa humo na sisi tunakunywa," alisema.

Mabelina Yunusu, alisema kuwa kabla ya mradi huo wa majisafi na salama kupelekwa katika zahanati ya kijiji hicho, wajawazito walilazimika kwenda na maji yao kwa ajili ya kufanyia usafi baada ya kujifungua. Yunusu alisema kuwa, maji yaliyohitajika ni kuanzia madumu mawili yenye ujazo wa lita 20 ambayo yalifuatwa katika bwawa hilo, kutokana na zahanati hiyo kutokuwa na maji.

"Kama ukiwa na mama anayesubiri kujifungua au ambaye tayari kajifungua na hukwenda na maji, ulilazimika kumwacha na kutembea kwa muda wa zaidi ya saa moja kufuata maji, tunafurahi sasa kijiji tumepata maji na zahanati yetu na shule pia wamepata maji," alisema.

Awali, akisoma taarifa kwa niaba ya kamati ya watumiaji maji kijijini hapo, Ezekia Kazaula alisema, kijiji hicho kina wakazi wapatao 2,646, na kuwa kutokana na tatizo la ukosefu wa maji lililokuwapo, kaya 200 zimehama kijiji na kwenda kuishi maeneo ya vijiji vingine ambavyo vinaupatikanaji wa huduma hiyo.

Mratibu wa mradi kutoka Shirika la World Vision wilayani Missenyi, Renatus Rugakingira, alisema mradi huo umegharimu zaidi ya Shilingi milioni 156 na utekelezaji wake ulianza Machi mwaka jana na kuzinduliwa Februari 13, mwaka huu.

## Ofa punguzo bei mafuta yachangamkiwa Dar es Salaam

**Na Mwandishi Wetu**

WAMILIKI kadhaa wa vyombo vya moto katika Jiji la Dar es Salaam, jana walichangamkia fursa ya ofa ya kupunguziwa bei ya mafuta.

Ofa ya kupunguza bei ya mafuta kwa Shilingi 70 kwa kila lita ilitangazwa juzi na Kampuni ya mafuta ya Total kwa wateja wake kama zawadi ya siku ya wapendanao duniani (Valentine) iliyoadhimishwa jana na ingetolewa kwa siku tatu kuanzia jana.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkurugenzi wa Sheria na Uhusiano wa Total, Marsha Msuya Kileo, jumla ya vituo 16 vya mafuta vya Total ndivyo vimeteuliwa kutoa ofa hiyo katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Moshi, Mwanza Mbeya na Morogoro.

Nipashe jana ilitembelea baadhi ya vituo vya kampuni hiyo vikitoa ofa hiyo kwa wateja wake.

Meneja wa Total Bagamoyo Road, Michael Kipingu, alisema kuwa wamepunguza bei ya mafuta kwa siku tatu ambapo petroli ilikuwa inauzwa kwa Shilingi 2,050 badala ya Shilingi 2,120.


Alisema dizeli ilikuwa inauzwa kwa Shilingi 2,050 badala ya Shilingi 2,010.

Alisema kutokana na punguzo hilo, wateja wameitikia wito kufika kituoni kwao kununua mafuta.

Alisema mbali na punguzo la bei ya mafuta, pia upendo umekuwapo hata kwa wateja wengine ambao wananunua bidhaa katika maduka yao kutokana na kuwapo zawadi za maua.

Mussa Bakari mmoja wa madereva wa bodaboda Morocco, alisema amefurahishwa na ofa hiyo katika kituo kilichopo eneo hilo na kueleza kuwa kama ofa hiyo ingeendelea zaidi ya wiki, watu wengi zaidi wangepata taarifa na kuwenda kununua.

Mmiliki wa kituo cha Total Oyesterbay, alisema maandalizi yalitakiwa yafanyike mapema ili watu wengi wajue uwapo wa ofa ya punguzo la bei.



# Tanzania mbioni kupata umeme wa uhakika

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MWENYEKITI wa Bodi ya Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), Dk. Alexander Kyaruzi, amesema Tanzania iko karibu kupata umeme wa uhakika na bei nafuu, ambao utaiwezesha kuuza na kununua kwa nchi za Afrika, baada ya kukamilika kwa mradi wa Kimataifa wa Eastern

Africa Power Pool mwakani. Akizungumza juzi katika Kijiji cha Lemunguru, Arumeru mkoani Arusha, ambako kunajengwa kituo kikubwa cha kupooza na kusambaza umeme, msongo mkubwa wa KV 400, wakati wa ziara ya bodi yake yenye lengo la kujionea hatua za ujenzi wa mradi huo, Dk. Kyaruzi alimpongeza mratibu wa mradi huo na wenzake kwa hatua kubwa waliyofikia.

Dk. Kyaruzi alisema hana shaka na mradi huo ambao utakamilika mwakani kutokana na jitihada zinazofanyika na amejiridhisha.

"Mradi huu ukikamilika utatuwezesha Tanzania kuondokana na umeme usio na uhakika kwa sababu tutakuwa tumeshaunganishwa na njia nyingi za umeme za nchi zingine za Afrika na kutuwezesha kuuza na kununua umeme kwa bei nafuu, hivyo baada ya mwakani shida ya umeme nchini itakuwa historia," alisema.

Alisema kupitia mradi huo wa kimataifa nchi za Afrika zitauziana umeme mwingi wa uhakika na wa bei nafuu, hatua ambayo ni kubwa na ya kujivunia kama nchi.

Pia alisema njia mbalimbali za kuunganisha umeme huo na kupoozea zimeanza kujengwa kote kunakotakiwa kupita Babati hadi Arusha ambako kituo kikubwa kitakuwapo na umeme utasafirishwa hadi mpakani

Namanga na kupokewa na nchi jirani ya Kenya ambao nao watajiunga na Ethiopia ambao wako katika hatua nzuri. Naye Mratibu wa mradi huo wa njia za kusafirisha umeme msongo wa KV 400 Kenya, Tanzania na Zambia, Mhandisi Peter Kigadye, alisema mradi huo umeanza kujengwa kwa kasi Novemba, mwaka jana Tanzania na upande wa Kenya nao wameanza kujenga.

Alisema mradi mzima una sehemu kubwa tatu za ujenzi wa njia za umeme, kupoozea umeme na usafirishaji kwenye vijiji na njia hizo ni Singida hadi Babati, Babati hadi Arusha na Arusha hadi Namanga mpakani na njia zote tatu zimeshaanza ujenzi.

Kigadye alisema gharama za mradi huo ni dola za Kimarekani milioni 258 ambazo zimechangwa na serikali, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo Japan (Jica). Alisema awamu nyingine ya mradi huo inaendelea kujengwa kutoka Mbeya hadi Zambia na kusisitiza kuwa watakapokamilisha hatua hizo, nchi itapata wawekezaji wengi kwa sababu nishati ya umeme itakuwa ya uhakika.

Nao baadhi ya wananchi waliopitiwa na mradi huo katika eneo la Lemunguru, Julius Laizer na Lameck Mollel, waliishukuru serikali kwa kuwapa fidia baadhi yao, huku wakiomba kujengewa barabara ili kupitika wakati wa masika na kiangazi.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Mhandisi Zephania Chaula (kulia), akiwapungia wananchi wa Kata ya Loiborsiret, baada ya kumaliza mkutano wa kuhamasisha maendeleo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanaotafuna mali za ushirika waonywa

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

MWENYEKITI wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini, Dk. Titus Kamani, amesema dhana iliyokuwapo ya kutafuna mali za ushirika, sasa itabaki kuwa historia na atakayethubutu kufanya ubadhirifu huo, atakuwa anakitafuta kifungo.

Dk. Kamani alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na viongozi mbalimbali wa vyama vya ushirika vilivyoko mkoani Manyara, katika ziara yake iliyolenga kusikiliza kero za wanaushirika, ili kuzitatua kwa maslahi ya wakulima waliojiunga na ushirika. "Yeyote ambaye anafikiria mali za ushirika ni mali za kupiga dili, kama walivyokuwa wanafanya huko nyuma mtu wa namna hiyo ni mfungwa mtarajiwa, hivyo mali za ushirika tuziheshimu na kuziogopa kama unavyoweza kuogopa kushika paja la mama mkwe," alisema Dk. Kamani.

Alizitaja baadhi ya mali za ushirika ambazo zimeshaokolewa toka serikali ya awamu hii ianze ni Nyanza mkoani Mwanza, Shirecu mkoani Shinyanga, mali za chama cha ushirika Moshi na mali za vyama vya KCU na KDCU vilivyopo mkoani Kagera, hivyo aliwataka kujifunza kwa wenzao kilichowatokea na wengine wanasota rumande hadi sasa.

Pia aliwaonya kuacha kumwita kutaja kutatua migogoro, badala yake wamwombe kuwatafutia viongozi wakubwa kama Waziri Mkuu au Rais kuja kuzindua miradi ya ushirika.

"Manyara mnatakiwa kuwa matajiri wa kutosha maana hali ya hewa inaridhisha. Hebu jivunie kuzaliwa hapa, sumbueni akiri zenu na mkitumie chuo hiki cha ushirika Moshi ili mnufaike na fursa zilizoko kwenu, kwa kuwa wako watu wanafikiria ubinafsi ambao hauwasaidii," alisisitiza. Aliwataka viongozi kuvaa ngozi ngumu ili kupambana na wabadhirifu wa mali za ushirika, ambao bado wanafikiria kupiga dili kupitia vyama vya ushirika. Naye Mrajisi Msaidizi wa Ushirika mkoani Manyara, Venance Msafiri, akisoma taarifa ya ushirika, alisema mkoa huo una vyama vya ushirika 267 na wanachama 27,043.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Rift Valley (Rivacu), Michael Tsaxara, alisema ushirika unahitaji uwazi na kitu kinachosababisha uchukiwe na watu ni ubinafsi na wengine wananunuliwa na wanasiasa.

## Vijana wafundwa ubunifu teknolojia

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

VIJANA nchini wametakiwa kubuni teknolojia zitakazowasaidia wajasiriamali walioko kwenye viwanda vidogo kuongeza tija katika uzalishaji wa bidhaa na kuhimili ushindani wa soko.

Meneja wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) Mkoa wa Arusha, Nina Nchimbi, alisema hayo alipotembelewa na vijana kutoka mabaraza ya vijana yaliyoandaliwa na shirika la INFOY.

Aliwataka vijana kubuni teknolojia badala ya kuwa tegemezi kwa kutumia zile za kutoka mataifa ya nje, jambo ambalo haliwanufaishi.

Nchimbi alisema Sido inatoa fursa kwa vijana kufika na kutumia ubunifu wao ambao unaweza kubadilishwa na kuingia kwenye mfumo wa kibiashara hivyo kuwanufaisha.

"Ninachowaomba vijana wa Tanzania badilikeni kwa kujituma na kuwa wabunifu, ili kunufaika zaidi badala ya kutegemea vitu vilivyobuniwa na wenzenu nchi zingine," alisema.

Mratibu wa INFOY, Laurent Sabuni, aliyekuwa ameambatana na vijana hao, alisema vijana wanapaswa kuwa wabunifu na kubuni teknolojia ambazo zitasaidia taifa kusonga mbele kuelekea uchumi wa viwanda.

Sabuni alisema ziara hiyo inalenga kuhamasisha vijana kuongeza hamasa ya kushiriki katika uchumi wa viwanda, kwa kutumia ubunifu na fursa zinazowazunguka.

"Nchi yoyote haiwezi kuendelea kama hakuna ubunifu wa teknolojia na bidhaa mbalimbali ambazo nchi inaweza kuviuza katika masoko ya nje na kuleta faida," alisema Sabuni.

Johnson Joseph mmoja kati ya vijana hao, alisema suala la ubunifu kwa vijana linapaswa kuhimizwa na kuhakikisha linaungwa mkono na wadau wa maendeleo, kwa kutenga maeneo ya uzalishaji ili kuwapa fursa ya kubuni bidhaa mbalimbali.

Alisema kwa sasa wameanza kujifunza kuanzisha miradi mbalimbali itakayowasaidia kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini, ikiwamo ufugaji kuku na usindikaji wa bidhaa za nafaka.

# Usimamizi wasaidia kudhibiti makusanyo

**Na Godfrey Mushi,** HAI

USIMAMIZI unaolenga kuwabana watoza ushuru wanaokusanya kodi katika biashara za matunda na mboga katika Soko la kwa Sadala, Wilaya ya Hai, umesaidia kuondoa udanganyifu wa kiwango cha fedha kinachopatikana kwa siku kutoka Sh. 600,000 hadi kufikia Sh. milioni mbili.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amesema mafanikio hayo yanatokana na uamuzi wake wa kufukia mianya ya upigaji wa mapato ya serikali yanayopatikana katika vyanzo mbalimbali yakiwamo masoko.

"Haya ni mafanikio makubwa katika kuongeza mapato ya halmashauri yetu. Katika Soko la matunda na mbogamboga la kwa Sadala, tumeweza kumaliza ujanja ujanja wa watu kupiga hela za umma wakati wa makusanyo ya ushuru, kwa mfano kwa Sadala peke yake mapato yamepanda kutoka Shilingi 600,000 hadi Shilingi milioni mbili kwa siku za soko.

Zaidi aliongeza: "Siyo huko tu, hata ushuru wa mabasi katika stendi ya Bomang'ombe nayo yameongezeka kutoka Shilingi 200,000 hadi Shilingi 400,000 kwa siku moja."

Sabaya alisema mafanikio hayo yanatokana na ushirikiano mzuri, kati ya viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai na vyombo vya usalama, jambo ambalo limeisogeza wilaya hiyo kushika nafasi ya 10 kitaifa kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Wilaya, Hai imefanikiwa kuongeza mapato hayo ya ndani katika robo ya kwanza na ya pili ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mwishoni mwa mwaka jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alisema katika uchambuzi wa mapato ya robo ya kwanza mwaka huo wa fedha unaonyesha kuwa, jumla ya halmashauri 76 zilifanya vizuri kwa kukusanya zaidi ya asilimia 20 ikiwamo Hai.



Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii), Neema Mwanga (kulia), akitoa maelezo kuhusu uzingatiaji wa sheria, taratibu na kanuni katika utekelezaji wa kazi za mashirika yasiyo ya kiserikali, wakati wa kikao cha wadau wa mashirika hayo mkoani Kilimanjaro juzi. Katikati ni Katibu Tawala wa Mkoa huo, Aisha Amour na Katibu Tawala Msaidizi (Mipango), Lydia Liwa. **PICHA: WAMJW**

# Fedha ziara ya madiwani nusura zivunje kikao

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

DAKIKA 30 za mabishano makali kati ya madiwani wa Wilaya ya Siha na wataalamu wa halmashauri hiyo kutokana na kukosekana kipengele cha bajeti ya ziara ya madiwani mikoani, nusura zisababishe wagomee kupitisha bajeti ya maendeleo kwa mwaka mpya wa fedha 2019/2020.

Mabishano hayo yalisababisha kuahirishwa kwa muda kikao hicho cha bajeti na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kulazimika kwenda kuingiza kipengele cha ziara ya madiwani ambacho wamekitengea Sh. milioni 18 katika Bajeti ya Maendeleo ya Wilaya ya Siha ambayo ni Sh. bilioni 23.5

Hoja ya kukosekana kwa kipengele hicho iliibuliwa jana na Diwani wa Viti Maalum (CCM), Claudia Muro, ambaye alisema kitendo cha kutotengwa fedha kwa ajili ya kuwaongezea uelewa madiwani sio kitendo cha kuungwana, kwa vile tangu waingie madarakani mwaka 2015, hawajawahi kwenda kufanya ziara kwa ajili ya kuongeza uelewa.

"Sijui ni kwa nini hatutaipitisha bajeti hii hadi hapo watakapoirekebisha. Toka tuchaguliwe na kuunda baraza hili, hatujawahi kufanya ziara yoyote ya kuongeza uelewa kwa madiwani, hatuwezi kuendelea na kikao hadi mtakapo kwenda kurekebisha na kuweka kipengele hiki," alisema Muro.

Akiunga mkono hoja hiyo, Diwani wa Gararagua (CCM), Zakaria Lukumai, alisema kitendo hicho ni sawa na kuwapa watoto chakula na kumnyima baba, wakati yeye ndiyo mtafutaji wa chakula.

Lukumai alifafanua zaidi akisema, "Ziara kama hizi katika halmashauri nyingine wanafanya na inasaidia kuongeza uelewa kwa madiwani, na jambo hili liko wazi kwamba uelewa ukiwapo hata uchumi nao hupanda katika halmashauri husika."

Baada ya hoja hiyo kuungwa mkono na madiwani, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Valerian Juwal, alikubali kuahirishwa kikao hicho kwa muda ili kwenda kuweka sawa kipengele hicho.

Katika utetezi wake, Juwal alisema hawakuwa wamekiweka awali katika makisio ya bajeti hiyo kutokana na upungufu wa fedha.

Kikao hicho kiliporejea, Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, Aggrey Kiando, alilieleza baraza hilo kwamba wameweka kiasi cha Sh. milioni 18 katika bajeti hiyo kwa ajili ya kufanya ziara kwenye mikoa ya Dodoma au Morogoro.

Awali akiwasilisha bajeti hiyo, Juwal aliwaeleza wajumbe wa baraza hilo kuwa makusanyo ya ndani ya halmashauri yatakuwa Sh. bilioni 1.265, ambapo vyanzo vikuu vya makusanyo hayo vitaendelea kuwa ushuru wa mazao, viwanja, kodi za leseni na huduma mbalimbali pamoja na ada na tozo mbalimbali.

Alieleza kuwa Halmashauri ya Siha imejipanga kuhakikisha inakusanya mapato yake ya ndani kwa kutumia mashine za kielektroniki kwa lengo la kupunguza na kuziba mianya ya upotevu wa fedha zinazokusanywa katika vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani.

Hata hivyo, baraza hilo la madiwani kwa kauli moja walipitisha bajeti hiyo na kutoa ahadi za kutoa ushirikiano wa kutosha kumsaidia Mkurugenzi Mtendaji kufanikisha lengo la kukusanya mapato zaidi ya asilimia 80 hadi 100.

# NGO zakumbushwa kuchangia huduma jamii

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MSAJILI wa asasi za kiraia nchini, Neema Mwanga, ametangaza kiama kwa mashirika yasiyo ya kiserikali yatakayoshindwa kutoa mchango wake wa huduma katika jamii maskini, licha ya kujinasibu kufanya hivyo wakati yakiomba kusajiliwa.

Mwanga alitangaza dhamira hiyo, wakati akizungumza na wadau wa maendeleo wanaoendesha asasi hizo katika mkoa wa Kilimanjaro.

"Mashirika yasiyo ya kiserikali yana dhamana kubwa ya kutoa mchango katika jamii maskini na isiyo na uwezo kuweza kufikia huduma mbalimbali ambazo zinaweza kuwasaidia kuboresha ustawi wa maisha yao hasa kutokana na uhitaji. Tunayo orodha ambayo inaonyesha ziko NGO za mfukoni," alisema.

Ofisi ya msajili huyo ambayo iko katika Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, imetoa angalizo hilo la kuwataka wadau hao kujiandaa kisaikolojia kwa wale walioshindwa kutekeleza vipaumbele vyao kutokana na matakwa ya usajili.

Msajili huyo alisisitiza kwamba atachukua hatua kali dhidi ya shirika lolote litakalokiuka kufanya kazi kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya NGO ya Mwaka 2002 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2005.

Wakati serikali ikitoa ilani hiyo, zipo tuhuma kwamba kuna NGO za mfukoni au hewa ambazo zinatumia vibaya usajili wao kutengeneza faida na kuacha malengo husika ya kusaidia jamii iliyolengwa.

Huenda ukawa mwanzo mzuri kwa serikali kufanya udhibiti, baada ya Mamlaka ya Mapato (TRA) mkoani Kilimanjaro kutangaza pia kuanza kupitisha chujio la kuzibana asasi za kiraia 130 zilizoko katika mkoa huo.

Uamuzi uliotangazwa mwishoni mwa mwaka jana na Meneja wa TRA Mkoa wa Kilimanjaro, Msafiri Mbibo, pamoja na mambo mengine, tayari imeziandikia barua ikitaka ziwasilishe taarifa zao za ritani na mahesabu ya kila mwaka ili iyatathmini kama hayakutengeneza faida au yana tamko la Kamishna Mkuu wa Kodi.

Habari zaidi zinasema, hadi sasa kuna mashirika yasiyo ya kiserikali yapatayo 38, yamebanwa na yanalipa kodi.



Ukurasa 19

Ofisa Biashara: Chukueni mikopo vijana, sharti 'matanuzi' marufuku



Ukurasa 14

Ununuzi wa nazi yako, unakuniwa kwa mashine maalum, wakabidhiwa rojo



## Mkutano wa Marekani Poland wasusiwa

Ukurasa 15

BUFE

Ijumaa Februari 15, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



# Umaskini hadi kulemazwa; sasa atekeleza nadhiri kuhudumia maskini, wanaoteswa

**Na Salome Kitomari,** TURDAco

***IJUMAA iliyopita, katika jarida hili ilikuwapo simulizi ya madhila wanayoyapaya vijana na hasa mabinti, ukiwa na mzizi wa umasikini na uonevu katika jamii. Leo kuna makala nyingine yenye simulizi ya aina hiyo. Fuatilia.***

HISTORIA ya maisha ya mtu inaweza kusaidia kubadili maisha ya wengine, kwa kuhakikisha hawapitii shida na tabu ambazo mwenye historia alipitia katika safari ya maisha yake.

Ndivyo alivyofanya, Consoler Eliya, mwenye simulizi ya kuteseka tangu umri wa miaka saba, kiasi cha kumdhuru kiafya na kushindwa kusoma katika mfano wa watoto wengine.

**INAENDELEA UK.16**

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Takwimu za Biashara Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

**Biashara**

Jumla ya Mauzo (bln) 22,136.24

Mauzo 109,584,255.00
Hisa 58,317

**Kielezo**

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 4,207.58 | +0.00 |
| DSEI | 2,296.50 | -37.11 |

**ZILIZOPANDA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| KA | 180 | -2.70% |
| JHL | 9,500 | +1.06% |
| SWIS | 3,760 | +7.43% |
| EABL | 5,320 | -1.66% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| TCCL | 1,200 | -11.76% |
| ACA | 5,550 | -2.63% |
| NMB | 1400 | -1.41% |
| NMG | 2,510 | -1.57% |
| KCB | 840 | +2.44% |

UCHUMI

ZAMA ZA MAGEUZI

# Unauziwa nazi yako, unakuniw mashine maalum, wakabidhiw

• Chombo cha nusu milioni chatoza Sh. 200 • Nafuu teknolojia yapangish

**Na Beatrice Moses**

NIPO nakatiza katika viunga vya soko dogo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam, nafika hadi eneo walipojipanga wauza nazi, ambako nakutana na msongamano wa watu, kufikia hali inayonilazimu kusimama na kupishana, kufika safari yangu.

Pembezoni mwangu, nawaona wanawake kadhaa waliojipanga kwa muuza nazi mmojawapo. Navutiwa na kusogea karibu zaidi, baada ya kubaini kuna mashine inayotumika kukuna nazi, katika namna ambayo ushuhuda, hisia na mantiki, zinaniekeza kuwa mgeni nayo. Ni kweli kuna ugeni.

Maisha yangu, nimezoea kuona nazi ikikunwa kwa kibao cha mbuzi, lakini hapa kuna kifaa kipya machoni mwangu, kwamba kinatumika kukuna nazi haraka, kuliko ilivyozoeleka.

Nakuwa na subira kwa wateja wahudumiwe, kisha najitambulisha kwa mfanyabiashara huyo, ambaye anaongozwa na msemo wa wahenga wa 'haba na haba hujaza kibaba'.

Shabani Kitogo, ndiyo jina lake, ni mwenyeji wa Kisiju wilayani Mkuranga, mkoa wa Pwani. Anasema tangu aanze kazi ya kuuza nazi, ni takribani miaka 20 sasa.

Huku akitabasamu, Kitogo anasema alianza kukuna nazi kwa mashine mwaka jana, hatua ambayo imemsaidia kuuza nazi nyingi, tofauti na alivyokuwa anauza awali.

"Kabla nilikuwa nauza nazi 100 kwa siku, lakini tangu nianze kuuza na kukuna nazi kwa siku nauza 150 hadi 200 kwa siku," anasema Kitojo.

Anasema mashine hiyo, ameinunua kwa beo ya Sh. 500,000 na wateja wake wanalipa Sh. 200 kwa kila nazi wanayokuniwa.

Anasema, kwa asili kazi ya kukuna nazi iliaminika kuwa ni ya mwanamke, kwa kuwa ndiye mwenye



Muuza nazi wa sokoni Kariakoo jijini Dar es Salaam, anakopatikana Shabani Kitogo, akiendelea na biashara. **PICHA: MTANDAO.**

> **Wateja wangu wengi ni wanawake, wanaume ni wachache ambao hununua na kutaka nazi ikunwe kabisa.**

jukumu la mapishi kwa familia nyingi za Kiafrika.

"Wateja wangu wengi ni wanawake, wanaume ni wachache ambao hununua na kutaka nazi ikunwe kabisa. Wanapenda zikunwe na wake zao," anasema Kitogo.

"Kiutamaduni wapo wanaume wanapenda mkewe akune nazi, naye awe pembezi anazungumza naye. Maana inapaswa kukunwa taratibu ili kupata rojo laini itakayowezesha kupata tui vizuri," anasema.

Anabainisha kuwa, wanaume wengine wanapenda nazi iliyokunwa, ili kumpunguzia kazi mkewe, hivyo anapata muda mzuri wa kupumzika.

Kitojo anasema ni rahisi ku-



UCHUMI

**Umaskini hadi kulemazwa; sasa atekeleza nadhiri kuhudumia maskini, wanaoteswa**

Ukurasa 16

UCHUMI

**Mkutano wa Poland na Marekani wasusiwa kidiplomasia**

Ukurasa 15


BIASHARA


**Ofisa Biashara: Chukueni mikopo vijana, sharti 'matanuzi' marufuku**

Ukurasa 19

# wa kwa a rojo

## na foleni wateja





tumia. Inahitaji kuwa makini, ili kuepuka kupata majeraha. Pia, inatakiwa kuzingatia usafi, kwa kuhakikisha unafuta kwa kitambaa safi, beseni unalokingia rojo ya nazi.

"Pamoja na hayo, kwa matumizi ya kifamilia kwa mashine hii ni gharama. Naamini wengi hawawezi kumudu," anasema Kitojo.

Anasema, kuwa anafurahia hali ya biashara yake ilivyo sasa kwa kuwa, pia wamejitokeza wanunuzi wa vifuu ambao wamemweleza kuwa wanakwenda kutengeneza mkaa.

Kitojo anasema, changamoto inayowakabili ni ufinyu wa eneo wanashindwa kuhifadhi vifuu vyao ili kusubiri kupata wanunuzi husika.

**MWANZILISHI**

Rajab Said, ni mfanyabiashara mwingine wa nazi, anayetajwa kama mwazilishi wa kukuna nazi sokoni hapo, kwa kibao cha mbuzi.

"Kukuna nazi ni kazi ya halali inayoingiza kipato kwa hiyo sikujali wana fikra gani, nilikuna kibao ingawa ukilinganisha ninavyotumia mashine, ninakuna haraka zaidi," anasema Said.

Said anasema, changamoto ambayo wamekuwa wakiipata ni kukatika umeme inapotokea hali hiyo, wanawake wanajikuta wakikosa fedha za kukuna kwa kuwa, mashine wanazotumia ni za nishati hiyo.

Anasema nazi zao wengi wanauza kulingana na ukubwa, hivyo zipo za kuanzia Sh. 500 hadi Sh.1,500 kulingana na mzigo unavyopatikana kutoka shamba.

Loyce Gimonge ni mmoja wa wateja anasema yeye ni mkazi wa Kimara Mbezi ambapo hali ya usafiri haitabiriki, hivyo akinunua nazi iliyokunwa inamrahisishia kazi zake za mapishi.

"Hapa nikifika nyumbani si wazi kutafuta kibao nikune, bali nachuja na kupika, hii inakuwa na radha nzuri kuliko ile ya dukani iliyochujwa na kuwekwa kwenye paketi," anasema Gimonge.

Anabainisha kuwa kununua nazi iliyokunwa kunampa nafasi ya kupika haraka na kupata muda mzuri wa kulala.

Kwa mujibu wa Jarida la Kilimo Endelevu Afrika Mashariki Toleo la 78 la Oktoba 2018, Minazi hulimwa kwa wingi katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Mtwara, Morogoro, Tanga, Unguja na Pemba.

Mimea hiyo pia hulimwa kwa uchache katika mikoa ya Mbeya, Tabora, Kigoma, Rukwa na Mara.

**TUI LINATUMIKAJE?**

Kwa mujibu wa wataalamu wa masuala ya mapishi wanabainisha kuwa chakula kilichopika kwa tui la nazi kina ladha nzuri na harufu inayomvutia mlaji.

Baadhi ya vyakula vinavyotajwa kupikwa kwa tui la nazi ni pamoja na maharage, njegere, kunde, wali, samaki, dagaa, unaweza kutumia kukanda kwenye mikate ya kumimina, vitumbua, maandazi.

Pia, tui la nazi hutumika kuunga mihogo, makande na tambi na baadhi ya mboga, zikiwamo majani ya maboga na kisamvu.

Katika jarida hilo wanabainisha kuwa tui la nazi linasindikwa, ili kupata mafuta na achari (jamu) ambayo inaweza kutumia kuongeza ladha kwenye vyakula mbalimbali, kama chipsi na kachori.

Kwa upande mwingine, tui la nazi linatajwa kutumika kutengenezea mafuta yanaaminika kuwa tiba ya nzuri hasa kwa wanaokabiliwa na matatizo ya ngozi kuwa kavu.

Mafuta hayo yanaelezwa kuwa ni bora kwa ngozi ya watoto wachanga, hivyo wanapozaliwa, inashauriwa kuwapaka mafuta ya nazi kwa sababu hayana kemikali.

Aidha, inaelezwa kuwa mafuta ya nazi yanaongeza kinga mwilini na kukabili shinikizo la chini la damu, huku katika taaluma ya afya ya mwili ya unyooshaji viungo au masaji.



Shabani Kitogo, mjasiriamali wa nazi na kukuna kwa kutumia teknolijia ya kisasa, inayowavuta wateja wengi, akiwa kazini katika picha tofauti. **PICHA ZOTE: BEATRICE MOSES.**

# Mkutano wa Poland, Marekani wasusiwa



Makamu wa Rais wa Marekani, Mike Pence. **PICHA: MTANDAO.**

MKUTANO wa Kimataifa Kuhusu Mashariki ya Kati ulioandaliwa na Poland na Marekani, umefunguliwa huku kukiwako hali ya mashaka ya kutumia malengo yake.

Makamu wa Rais wa Marekani, Mike Pence, ameshawasili Poland, kushiriki mkutano huo wa kimataifa, akiunganisha na ziara ya siku nne barani Ulaya, ambako anatembelea kambi ya maangamizi ya Auschwitz, iliyotumiwa na utawala wa Kinazi.

Baada ya kushiriki katika mkutano huo wa Mashariki ya Kati, alitarajiwa kwenye mkutano wa Usalama utakaofanyika leo mjini Munich, Ujerumani.

Mkutano wa Poland, awali ulipendekezwa na utawala wa Rais Donald Trump, ukijikita zaidi katika mada ya Iran, lakini waandaaji wakaamua kutanua ajenda za kujadiliwa, zikijumuisha mgogoro wa Israel na Palestina; mapambano dhidi ya kundi la Dola la Kiislamu, Syria na mgogoro wa Yemen.

Hata hivyo, hoja zilizotolewa mkutanoni hazionyeshi hatua thabiti za kuchukuliwa, zaidi inalenga kuundwa makundi ya kufuatilia hali ilivyo katika mada hizo.

Pia, kimeshuhudiwa nchi takriban 60 zinazoshiriki mkutano huo, zinawakilishwa na viongozi wa ngazi za chini serikalini mwao.

**EU YASUSA**

Wakati Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu na Makamu Rais wa Marekani, Mike Pence, wakihudhuria mkutano huo, akiandamana na Waziri wa Mambo ya Nje, Mike Pompeo, ila nchi nyingi hazijakipa uzito.

Nchi za kiarabu, Ufaransa na Ujerumani zimeamua kutuma maofisa wa ngazi ya chini, huku Mkuu wa Sera za Nje wa Umoja wa Ulaya (EU), Federica Mogherini amejiweka kando.

Russia na China, hazishiriki mkutano huo na Wapalestina wametoa wito wa kikao hicho kususiwa.

Iran kwa upande mwingine, imeendelea kulaani na kuukosoa mkutano huo, wakiuita ni cha 'sarakasi'.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Javad Zarif, anasema mkutano huo wa siku mbili 'umeshakufa kabla haujaanza."

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alitarajiwa kutumia fursa hiyo ya mkutano wa Poland, kunadi hadharani uhusiano wa nchi yake ulivyoimarika na mataifa kadhaa ya Ghuba ya Arabuni.

Kwa mujibu wa ajenda iliyowekwa, Makamu wa Rais wa Marekani, Mike Pence, alipewa fursa ya kuhutubia masuala mbali mbali ya Kanda ya Mashariki ya Kati.

Pia, waziri wake Pompeo, jukumu lake ni kuzungumzia Mpango wa Marekani Juu ya Syria, kutokaha na uamuzi wa Rais Trump, kuondoa wanajeshi wake. **DW**

**BEI YA MAZAO >>** MCHELE 187045.45/- | ULEZI 142263.16/- **FEDHA >>** RAND 165.50 | KSH 22.85 | USH 0.63

UCHUMI

MAGUMU YA CONSOLER

# Umaskini hadi kulemazwa; sasa atekeleza nadhiri kuhudumia maskini, wanaoteswa

• Alikaa stendi kumwandikia Mola barua • Dhamira ya ubinti aliianza alipopevuka
• Madaktari walimkataza shule, ndoa • Leo ana digirii, watoto, kituo kinacholea

**Inatoka Uk.13**

Licha ya leo kuwa msomi wa elimu ya shahada ya uzamili, ameamua kujitoa awe mama wa mabinti wanaopitia mateso na manyanyaso yanayowakwaza kufikia ndoto zao za maisha.

Mazingira hayo ya kimaisha, ndiyo walimsukuma Consoler, akalazimika kuandika barua kwa Mungu, tendo alilofanya akiwa katika kituo cha basi, baada ya kufukuzwa kwenye chumba cha mtihani wa kidato cha kwanza.

"Ilikuwa siku ngumu sana kwangu, kwa kuwa licha ya kusoma kwa shida kwa kuomba omba fedha, mateso nyumbani, kudharauliwa na kunyanyaswa kwa kila hali, lakini sikuruhusiwa kufanya mitihani ya kidato cha kwanza, kwa kuwa sijamaliza kulipa ada," anasema.

Consoler anasema, barua aliyomwandikia Mungu, aliahidi iwapo angefanikiwa kusoma hadi kidato cha sita, angetumia fursa hiyo kuwasaidia wasichana wanaopitia changamoto za aina yake.

**AITUMIKIA BARUA**

Ni ahadi iliyotimia baada ya kujiunga na chuo kikuu na kupata fedha za Bodi ya Mikopo, aliamua kuishi kwa misingi ya barua aliyoandika, akiishi na wasichana waliotelekezwa.

"Ni maombi yangu kuwa hata siku nikiwa sipo duniani, Tanzania iwe na familia ya watoto wawe na nyumbani, badala ya vituoni. Vituo vibaki vya polisi na daladala na watoto waishi kwenye familia, kwa sababu naamini Mungu ana watu wengi wa kuweza kukaa na watoto," anasema Consoler.

Hiyo ni historia iliyowasilishwa wanaosomea talauma ya Mawasiliano kwa Umma katika Chuo Kikuu cha Tumaini, Tawi la Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya kukamilisha mafunzo yao kwa vitendo, walipotembelea nyumba ya New Hope for Girls, anakopatikana Consoler.

Wanafunzi hao walipika, kushiriki usafi, kupiga pasi nguo, kupaka rangi viatu, kucheza na watoto, kusaidia kufanyakazi za darasani na kuongea nao, kama sehemu ya mafunzo yao, katika dhana ya kurejesha kwa jamii.

Ziara hiyo yenye mvuto, kuna wakati iligeuka uwanja wa simanzi iliyoibua machozi, wakati Consoler alielezea historia yake na jinsi anavyowalea wasichana hao 38.



Wanakikundi wa Kinyerezi Family, walipotembelea makazi yake na wasichana anaowalea katika kikundi chake. **Picha chini;** Consoler Eliya, mwanzilishi wa nyumba ya New Hope for the Girls, akipokea misaada ya kituo chake, kutoka kwa wahisani. **PICHA ZOTE: SALOME KITOMARI.**



> **Nilianza kuzunguka nikiwa na sare za shule nikiomba ada. Wengine waliniita mimi ni 'malaya mdogo' niliyejificha kwenye sare za shule.**

**MAHALI PALIVYO**

Unapofika kituoni hapo, unapokewa na mabinti wenye umri tofauti, dhahiri wakionyesha tofauti wenye adabu, wanaojitambua, salamu zao zimejaa heshima ya mapokezi.

Hawafichi uchangamfu wa majukumu yao kuanzia ukaribishaji, ushiriki wa kazi mbalimbali kama kuandaa mavazi na kusaidiana na dada yao kupika.

Tofauti na matarajio ya vurugu na kutitambua, penye mkusanyiko wa wasichana, mahali hapo ni kinyume. Ni dhahiri mabinti hao ukikutana nao hata nje ya nyumba, wana upendo wa hali ya juu.

Nyumba wanayoishi ni ghorofa inayowatosheleza wote na nje kuna ubao wa taarifa mbalimbali. Sebuleni kuna televisheni na hawatumia kiti, wanakaa chini kuangalia.

Staili yao ya kuishi inabeba sura ya familia na ni vigumu kujua kwa haraka, tofauti ya watoto wa Consoler na anaowalea kituoni hapo, kwani usawa uko juu.

**MAISHA KITUONI**

Nyumba ya New Hope for Gilrs, iliyopo Kimara Stopover, jijini Dar es Salaam, ilianza mwaka 2005. Ni zao la historia ya maisha yake tangu akiwa na umri wa miaka saba.

"Nilikuja Dar es Salaam kutoka Kagera, nikiwa naumwa, ikiwa ni mara ya tatu kufika jijini, katika familia niliyoachwa, baada ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kusema natakiwa kubaki kwa ajili ya matibabu,"anaanza simulizi.

Consoler anaongeza: "Nilibaki kwa ndugu, lakini kwa bahati mbaya katika familia niliyofikia walinitesa sana. Naamini Mungu aliniandaa kunipitisha nilikopitia, ili niweze kupata heshima ya kulea wasichana ninaowalea leo hii."

Anayasimulia maisha hayo, akiyatafsiri yalikuwa magumu na mateso ya kupigwa sana, kila alipopofanya kosa dogo, huku akiachwa bila ya nguo.

Mama huyo anasema, hakupewa nafasi ya kula chakula na watoto wengine nyumbani na nakiita alichopewa kuwa "Cha kuokotewa chakula kutoka majalalani."

Consoler anafafanua kwamba, katika hatua hicho alipewa chakula chenye hali mbaya, muda mrefu alifungiwa ndani na alilala stoo.

"Nikiwa na umri wa miaka 11, mama niliyekuwa naishi naye aliniambia nikiwa kama mtoto wa kike, sitakiwi kuendelea kusoma kwa kuwa najua kusoma na kuandika inatosha, " anasimulia.

Anafafanua: "Akaniambia amenitafutia mwanaume tajiri anauza magazeti, ana baiskeli na yuko tayari kukuoa. Alinichukua akanipeleka kwenye jumba bovu na nilikutana na huyo kaka. Nililia sana, baadaye (muoaji) aliamua kuniacha na kumwambia mama yangu (mlezi) muache tutaongea kesho."

"Maisha hayakuishia hapo. Niliendelea kuishi maisha ya shida sana kwa kosa dogo nilipigwa sana. Aliniamsha asubuhi kwa kunimwagia maji baridi. Nilimaliza darasa la saba nikiwa najua kusoma na kuandika tu, nilikuwa napenda sana shule, baadaye nilipata shule kwa kuhangaika mwenyewe."

Mama huyo anaendeleza simulizi yake kwamba, akiwa na umri wa miaka 15, msomi wa muhula wa kwanza wa kidato cha kwanza, alitolewa kwenye chumba cha mtihani pekee yake, kwa deni la ada. yake na ndipo wazo wa nyumba ya huduma iliyopo leo, ilipozaliwa.

"Nilitoka ndani ya chumba cha mtihani nikiwa pekee yangu nikakaa kituo cha basi, nikakumbuka kulikuwa na baba yangu mdogo anaitwa Baba Mdogo Mlokole, alikuwa ananiambia, ipo siku Mungu atakusaidia.

"Nilimwandikia Mungu barua katikati ya daftari langu huku nikilia sana. Nilimwambia Mungu naomba unipeleke shule nikimaliza kidato cha sita, nitakuwa mama kwa watoto wanaoteseka kama mimi," anasimulia

Consoler anasema, baada ya kumaliza kuandika barua hiyo, alipata wazo kwenda eneo la Posta kuomba kwa kuwa alipafahamu, alipompeleka mtoto wa mlezi wake shuleni.

"Nilianza kuzunguka nikiwa na sare za shule nikiomba ada. Wengine waliniita mimi ni 'malaya mdogo' niliyejificha kwenye sare za shule, lakini mwisho wa

**INAENDELEA UK.18**

# Biashara katika picha



Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Kampuni ya simu ya Zantel , Rukia Mtingwa (kushoto) akimuonyesha Msimamizi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha nchini, Abdallah Mrisho namba ya mshindi wa Droo ya kwanza ya Promosheni ya TUMIA EZYPESA USHINDE iliyofanyika jijini Dar es Salaam ambayo imewezesha wateja 30 kujishindia fedha taslimu na Smartphones, (Katikati) ni Meneja Bidhaa Kitengo cha EZYPESA wa Zantel, Leonard Kameta.Promosheni itadumu kwa kipindi cha miezi 3. **NA MPIGAPICHA WETU**



Wachuuzi wa embe wakisubiri wateja kando ya Barabara ya Morogoro, eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA MIRAJI MSALA**



Wachuuzi wa vitumbua wakivihesabu tayari kwa kuingia mitaani kusaka wateja katika stendi kuu ya mabasi ya Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

**BEI YA MAZAO >> MAHINDI 52130.43/-| MAHARAGE 177272.73/-**

UCHUMI

# Umaskini hadi kulemazwa; sasa atekeleza nadhiri kuhudumia maskini, wanaoteswa

INATOKA UK.17

siku nilipata kiwango cha fedha na niliendelea na masomo," anasema.

Consoler, anakumbuka tukio lingine lililompatia madhara ya kiafya kwenye mgongo wake tangu wakati huo, ni siku mama mlezi alipompiga sana na kumbana kwa mlango, wakati akikazana kujitoa kwenda nje.

Anasema, alijibana na mlango na alianguka chini. Akiwa mahali hapo chini, alimkanyaga mgongoni kwa viatu virefu ana anaongeza:

"Huyu mama hakutosheka, alikuja kuniletea vurugu shuleni. Alilipa baadhi ya walimu, walinipiga sana kwa takribani saa nane. Kile kipigo 'kilipelekea' (kusababisha) nikawa na madhara makubwa ya kiafya na kuanzia hapo ndiyo nilitoroka kurudi Bukoba kwa wazazi wangu."

Aidha, anasema alifika nyumbani alikolala kwa siku moja na akapelekwa Hospitali ya Rufani KCMC, mjini Moshi alikolazwa kwa miezi sita, akiwa haoni kwa miezi mitatu, kwa sababu alipigwa sana kichwani.

"Nimehangaika sana kutibiwa, nimetibiwa nchini India mara mbili, lakini ilionekana madhara niliyoyapata ni makubwa sana, hivyo hawawezi kunihakikishia kutokuwa kwenye maumivu.

"Nina shida kubwa ya mgongo. Nilifanyiwa upasuaji mara mbili na upasuaji mkubwa wa kichwa, lakini mwisho wa siku ilionekana inabidi kukaa na kufuata masharti ya daktari. Ninaishi kwa dawa na kufuata utaratibu wa daktari kama nilivyoshauriwa.

"Kuna wakati ninaweza kuumwa sana na kushindwa kunyanyuka, kwa ajili ya mgongo. Lakini, nina mafuta na vidonge.

"Pia niliambiwa sitaweza kusoma, kwa kuwa mishipa iliumizwa sana na ninatumia jicho moja la kulia, maana la kushoto halina uwezo wa kuona,"anafafanua alichoelekezwa, alichokatazwa na madaktari kunusuru afya yake, akitaja sharti lingine asiolewe wala kuzaa.

**UDSM HADI NDOA**

"Mungu alinionyesha uwezo wangu na uwezo wake, alinisaidia nilisoma katika mazingira magumu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

"Nilisoma sayansi ya jamii nikiwa nakaa bweni la watu wenye ulemavu, kwa kuwa sikuwa naweza vitu vingi na ninadondoka kila ninaposoma, lakini nilimaliza mwaka 2008," anasema.

Consoler anasema, alipojiunga chuoni hapo mwaka 2005, alipata fedha ya mkopo kutoka bodi ya mikopo (HESLB) na ndipo alikumbuka kuishi kwa misingi ya barua yake.




Msichana mkazi wa New Hope For The Girls, Kimara, jijini Dar es Salaam, akizungumza walipotembelewa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tumaini, Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: SALOME KITOMARI.**

> **"Nilimwandikia Mungu barua katikati ya daftari langu huku nikilia sana. Nilimwambia Mungu naomba unipeleke shule nikimaliza kidato cha sita, nitakuwa mama kwa watoto wanaoteseka kama mimi.**



Mmoja wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tumaini, akishiriki kazi, alipotembelea kituo cha New Hope For The Girls, Kimara, jijini Dar es Salaam.

Anasema, hapo ndipo alipoanza kuwatafuta wasichana aliyokutana nao katika sehemu nyingi, aliwaomba wamuombee akifika kidato cha sita atawasomesha na atawasaidia.

"Wengi ni wanaokuja kufanya kazi za ndani na wanaoishi kwenye familia duni. Msichana wa kwanza, nilianza kumhudumia mwaka 2005, ilivyofika 2008 nilikuwa na wasichana saba, watano niliishi nao kwenye chumba kidogo na wawili niliwaombea kwa kaka yangu," anasema Consoler.

Anasimulia kwamba, wasichana hao kwa sasa wameshaolewa na wengine wanajitegemea wakiwa na kazi zao. Anaongeza: "Baada ya kuoana na mume wangu, tulikuwa na nyumba mbili."

" Kipindi hicho tumekaa kwenye mahusiano kwa miaka sita na nilikuwa namwambia hata nisome nifike wapi nataka kuwa mama wa mabinti, aliniambia 'Mungu anisaidie.'

"Niliwachukua watoto wangu saba wakawa wanalala kwenye kisebule kidogo na sisi chumbani, baadaye nilipata watoto wawili wakafika tisa.

"Kuna mama mmoja aliguswa na kunilipia nikasoma sahahada ya uzamili na nilifanya utafiti kwenye familia watoto wanaopitia changamoto gani walio yatima, wanaolelewa na walezi na wazazi," anasema.

Anasema kupitia utafiti huo, alibaini wengi wanateseka ndani ya familia na kwamba ilimpa nafasi ya kurudisha watoto wengi kwenye familia zao hasa waliokuwa wanakuja kufanyakazi za ndani, ambao aliwakusanyia nauli kutoka kwa marafiki na majirani na kuwarudisha kwao.

"Kuna wale waliohitaji sehemu ya kupaita nyumbani, hao ndiyo niliamua kukaa nao baada ya kumuomba mume wangu. Mtoto wetu wa kwanza alizaliwa katikati ya watoto tisa, alikuta ndugu zake ambao Mungu alitupa na mtoto wa pili alikuta ndugu zake 17," anasema.

Anasema, idadi ya watoto wanaohitaji msaada, iliongezeka kila siku na wapo wanaoweza kusaidiwa wakiwa kwenye familia zao, walifika zaidi ya 150, ambao wanahudumiwa na watu mbalimbali kwa kupewa ada na mahitaji.

"Hapa nyumbani tuna mabinti 38 wa kulea na wawili wa kuzaa, jumla 40 na wajukuu watatu. Mume wangu amepanga, lakini amekubali niishi furaha ya moyo wangu ambayo ni kulea watoto wa kike wanaotoka mazingira magumu na hatarishi. Wote wanasoma wako kuanzia darasa la awali hadi chuo kikuu," anaeleza.

Anasema wanawahudumia watoto hao kwa zaidi ya miaka 13,

INAENDELEA UK.20

FEDHA >> USD 2295.12| Pauni 2961.62| Euro 2594.86

UCHUMI

# Ofisa Biashara: Chukueni mikopo vijana, sharti 'matanuzi' marufuku

• Awapa ngazi muhimu za kupitia • Wakufunzi wataja shida iliko

Na Sabato Kasika

HALMASHAURI ya Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam, imetenga asilimia nne ya fedha, kwa ajili mikopo ya vijana, watumie katika kuanzisha miradi yao mbalimbali ya maendeleo.

Hata hivyo, Ofisa Biashara wa Manispaa hiyo, Peter Ngoti, anatoa angalizo kwa wakopaji, kwamba ni lazima wafanye hayo wakiwa na malengo ya maendeleo na siyo fedha zikaelekezwa katika starehe za mitaani.

Ngoti anasema, vijana walioko katika majukwaa waliojiunga wanapaswa kuanzisha biashara mbalimbali, kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi.

Katika kauli yake hiyo ya Februari Mosi mwaka huu, alipokuwa katika mkutano maalum wa kupokea mrejesho wa maendeleo ya biashara za vijana walioko katika majukwaa ya vijana, ndani ya manispaa hiyo.

Ni mkutano uliolenga mafanikio, changamoto na usajili wa vikundi, ili kuwawezesha kuendeleza biashara zao.

"Vijana changamkieni fursa ya mikopo, ili muweze kujishughulisha na ujasiriamali, kwa ajili ya kujikwamua. lakini ni makosa kukopa na kwenda kufanya 'matanuzi' eti muonekane mna pesa," anasisitiza Ngoti.

Anawaambia kwamba, kufanya starehe ni mwanzo wa kujiingiza katika matatizo na wanachopaswa ni kujiwekea malengo sahihi, yatakayowawezesha kufanya shughuli za kuwaingizia kipato, ambayo watarejesha, ili kutoa fursa kwa wengine zaidi nao wakope.

Ngoti anasema, kwa walioko katika vikundi inakuwa rahisi kwao kukopesheka, lakini anaendeleza msisitizio kwamba, jambo la msingi ni kuzingatia malengo ya mkopo kwa kuachana na mengine, yanayoweza kusababisha wakatumia vibaya pesa.

"Fedha za mikopo kwa ajili yenu siyo za rais wala chama, ni kodi zenu wenyewe. Lakini, msiombe mkopo ya uongo na kwenda kutumia pesa kwa mambo mengine, ili muonekane mna pesa," anasema Ngoti.

Ngoti anawafungua macho vijana hao, mbinu ya kuanzisha vikundi bora ni vyenye katibu, kwa maana vinawasaidia kutambulika na wakati huohuo, inawapa malengo yenye mwelekeo.

Katika angalizo lake, ofisa biashara huyo, anawasisitizia waombaji mikopo hao kuhusu katiba, kwamba iwaongoze wajasiriamali katika mafanikio, kuwa mbali na ubabaishaji au mgongano.




Kiongozi wa kikundi cha Vijana Tujikwamue na Umaskini' cha Mbezi Kwa Yusuph, Kata ya Msigani, Rechnold Msaki, akizungunza katika mkutano. Kulia ni Jabir Mahmoud wa jukwaa la vijana Temboni. **PICHA: SABATO KASIKA.**

> **"Baadhi ya vijana tumepata elimu ya kujitambua na kujikwamua kiuchumi, sasa ni vyema manispaa ikatusaidia katika kutangaza au kuonyesha shughuli zetu ambazo tumeanzisha baada ya kupata elimu.**

Ngoti anasema, biashara yenye mafanikio ni ambayo ina wajihi wa unadhifu na mvuto kwa wateja, huku akiwahimiza kwamba inaambatana na mbinu bora za masoko.

Hoja yake ni kwamba, waombaji daima wasianzishe biashara ili mradi wamepata mtaji, bali muhimu ni mwelekeo wa uhakika wa soko.

Mikopo ya kukopesha vijana katika biashara, inatokana na sehemu ya asilimia nne inayotengwa kutoka fungu la bajeti.

### VIJANA WANENA

Kwa upande wao, vijana wanasema manispaa hiyo inatakiwa iwasaidie kutangaza biashara wanazozifanya ili zijulikane zaidi wapate wateja wengi.

Jabir Mahmoud, ambaye ni kiongozi wa jukwaa la vijana la Temboni, anasema vijana wamekuwa wakijishughulisha na biashara mbalimbali, zikiwamo za ubunifu ambazo ni muhimu zikatangazwa.

"Baadhi ya vijana tumepata elimu ya kujitambua na kujikwamua kiuchumi, sasa ni vyema manispaa ikatusaidia katika kutangaza au kuonyesha shughuli zetu ambazo tumeanzisha baada ya kupata elimu," anasema Jabir.

Mafunzo hayo yaliyotolewa na taasisi ya Mpakani Tunaweza, yalisaidia kuibua vipaji vya vijana, katika maeneo kama ya uimbaji, yanayotakiwa kutangazwa, ili iwasaidie wahusika washiriki.

Kiongozi wa Kikundi cha Vijana Tujikwamue na Umaskini' kilichopo Mbezi Kwa Yusuph katika Kata ya Msigani, Rechnold Msaki, anasema wapo vijana 30 waliochanga mtaji wa Sh. milioni tisa.

"Mimi nilifanikiwa kuhudhuria mafunzo hayo na kuwaletea wenzangu elimu niliopata na kuitumia vizuri na sasa tumefanikiwa kupata kiasi hicho cha pesa kutokana na hisa, ada, kiingilio na kukopeshana kwa riba," anasema Msaki.

Kiongozi huyo anasema baada ya kupata mtaji huo, sasa wanajipanga kununua viti, maturubai kwa ajili ya kukodisha na vifaa vya kupikia chakula na mapambo ili wanavitumia katika shughuli mbalimbali ikiwamo harusi.

"Sisi kikundi chetu kina malengo makubwa, hivyo tukipata mkopo tutautumia vizuri, kwasababu tunataka maendeleo, ndio maana tuliamua kuchangishana fedha tangu Mei mwaka jana na sasa tuna Sh. milioni tisa," anasema.

### WAKUFUNZI

Mwenyekiti wa taasisi ya Mpakani Tunaweza, Assi Khalifa, ambao ni wakufunzi, anawataka waombajo hao wasibweteke na badala yake watumie vizuri fursa ya elimu ya biashara wanayopata, ili kuwasaidia katika maendeleo.

Anasema kwa mwaka mmoja na nusu, taasisi hiyo kwa ufadhili wa asasi ya kijamii uya The Foundation for Civil Society, imetoa mafunzo kwa vijana wa kata nne za Mbezi, Kwembe, Msigani na Mabibo.

"Vijana hao tumewahamasisha kuanzisha majukwaa yao, lakini changamoto ni kwamba, baadhi yao wamekuwa wakidhani kwamba baada ya mafunzo tunawapa pesa za kuanzishia biashara," anasema Khalifa.

Anasema taasisi hiyo imetoa elimu ya kuwafanya vijana wasibweteke bali watumie vizuri fursa zilizopo katika maeneo yao, kwa kuanzisha biashara.

"Sisi hatuna fungu la fedha kwa ajili yao ila tunawakumbusha tu kwamba wana asilimia nne ya mikopo, ambayo wanaweza kuandika maombi wakapewa kutoka manispaa yao na kuanzisha biashara," anasema Khalifa.

Anasema, taasisi yake iliamua kuitisha mkutano huo kwa kushirikisha viongozi wa ngazi ya mtaa hadi wilaya hiyo wasikilize changamoto zinazowakabili vijana wao ili wachangie mawazo ni jinsi gani wanaweza kuwasaidia.


# Takwimu za Biashara

Na Edward Ntwale & Elias Samweli

Bei ya Mazao Ya Chakula kwa Sh/kilo 100 Februari 13, 2019

| Mkoa | Arusha | D'Salaam | Dodoma | Kagera | Kilimanjaro | Kigoma | Manyara | Mwanza | Rukwa | Shinyanga |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 43000 | 70000 | 43000 | 60000 | 48000 | 50000 | 54000 | 60000 | 50000 | 61000 |
| Mchele | 200000 | 220000 | 190000 | 185000 | 180000 | 160000 | 200000 | 180000 | 170000 | 130000 |
| Mtama | 40000 | 90000 | 35000 | 100000 | 80000 | 70000 | 42000 | NA | 80000 | 50000 |
| Uwele | 42000 | 70000 | 35000 | 110000 | NA | 60000 | 100000 | 150000 | NA | 50000 |
| Ulezi | 73000 | 140000 | 85000 | 150000 | 180000 | 150000 | 120000 | 160000 | 200000 | 130000 |
| Ngano | 80000 | 150000 | 160000 | NA | 108000 | 150000 | 120000 | NA | 110000 | 140000 |
| Maharage | 150000 | 210000 | 160000 | 150000 | 180000 | 145000 | 150000 | 170000 | 200000 | 200000 |
| Viazi Mviringo | 78000 | 90000 | 63000 | 75000 | 65000 | 90000 | 62500 | 70000 | 90000 | 100000 |

## Mwenendo wa Shilingi




## Mafuta

Bei : Kuanzia Februari 6, 2019

| MKOA | DSM | Arusha | Kibaha | Dodoma | Geita | Katavi | Kigoma | Moshi | Lindi | Mwanza |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Petroli | 2,120 | 2,255 | 2,125 | 2,179 | 2,286 | 2,329 | 2,352 | 2,245 | 2,110 | 2,271 |
| Dizeli | 2,080 | 2,299 | 2,084 | 2,139 | 2,245 | 2,288 | 2,311 | 2,289 | 2,089 | 2,230 |
| M'Taa | 2,046 | 2,286 | 2,050 | 2,105 | 2,211 | 2,254 | 2,277 | 2,276 | 2,105 | 2,196 |

## Soko la Hisa la Dar es Salaam Kikao cha Februari 13, 2019

### Muhtasari

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,533.78 | +0.00 |
| DSEI | 2,154.35 | +3.54 |

| | |
|---|---|
| Thamani za Hisa (bln) | 20,765.64 |
| Mauzo | 246,206,800.00 |
| Hisa | 65,221 |

### Zilizopanda na Zilizoshuka

| Kampuni | Bei | Badiliko |
|---|---|---|
| JHL | 9,700 | -3.00% |
| KA | 200 | -2.44% |
| NMG | 1,580 | +1.28% |
| EABL | 5,100 | +0.99% |
| ACA | 5,700 | +1.79% |

### Viwango vya kubadilisha

| Fedha | Nunua | Uza |
|---|---|---|
| EUR | 2,591.28 | 2,617.65 |
| USD | 2,268.07 | 2,290.76 |
| KES | 22.38 | 22.56 |
| GBP | 2,947.82 | 2,977.52 |

## Bei za hisa hadi kikao cha Februari 13, 2019

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| ACA | 5,700 | 5,600 | +1.79 |
| CRDB | 135 | 135 | +0.00 |
| DCB | 340 | 340 | +0.00 |
| DSE | 1,300 | 1,300 | +0.00 |
| EABL | 5,100 | 5,050 | +0.99 |
| JHL | 9,700 | 10,000 | -3.00 |
| KA | 200 | 205 | -2.44 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| KCB | 1,000 | 1,000 | +0.00 |
| MBP | 490 | 490 | +0.00 |
| MCB | 500 | 500 | +0.00 |
| MKCB | 800 | 800 | +0.00 |
| MUCOB | 400 | 400 | +0.00 |
| NICO | 175 | 175 | +0.00 |
| NMB | 2,340 | 2,340 | +0.00 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| TBL | 11,700 | 11,700 | +0.00 |
| TCC | 17,000 | 17,000 | +0.00 |
| TCCL | 640 | 640 | +0.00 |
| TICL | 385 | 385 | +0.00 |
| TOL | 660 | 660 | +0.00 |
| TPCC | 2,060 | 2,060 | +0.00 |
| TTP | 120 | 120 | +0.00 |

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA

| FEDHA | KUNUNUA | KUUZA |
|---|---|---|
| KENYA SHS | 22.69 | 22.87 |
| UGANDA SHS | 0.58 | 0.63 |
| RWANDAN FRANC | 2.53 | 2.56 |
| BURUNDI FRANC | 2.18 | 2.19 |
| USD | 2272.40 | 2295.12 |
| POUND STG | 2931.39 | 2961.62 |
| EURO | 2568.26 | 2594.86 |
| CANADIAN $ | 1715.92 | 1732.56 |
| SWITZ. FRANC | 2259.74 | 2281.43 |
| JAPANESE YEN | 20.52 | 20.72 |
| SWEDISH KRONOR | 246.89 | 249.25 |
| NORWEG. KRONOR | 263.15 | 265.69 |
| DANISH KRONOR | 344.27 | 347.66 |
| AUSTRALIAN $ | 1615.45 | 1632.75 |
| INDIAN RPS | 32.10 | 32.40 |
| PAKISTAN RPS | 15.55 | 16.28 |
| ZAMBIAN KWACHA | 188.34 | 191.50 |
| MALAWIAN KWACHA | 2.91 | 3.10 |
| MOZAMBIQUE-MET | 36.50 | 36.81 |
| ZIMBABWE $ | 0.43 | 0.43 |
| SDR | 3151.79 | 3183.31 |
| GOLD (T/O) | 2972884.84 | 3004449.79 |
| S. AFRICAN RAND | 163.91 | 165.50 |
| UAE DIRHAM | 618.74 | 624.76 |
| SINGAPORE $ | 1674.94 | 1691.44 |
| HONK KONG $ | 289.54 | 292.43 |
| SAUD ARABIAN RIAL | 605.94 | 611.95 |
| KUWAIT DINAR | 7481.88 | 7554.46 |
| BOTSWANA PULA | 214.51 | 218.50 |
| CHINESE YUAN | 335.98 | 339.26 |
| MALAYSIA RINGGIT | 559.02 | 564.05 |
| SOUTH KOREA WON | 2.03 | 2.04 |
| NEWZEALAND | 1547.50 | 1563.89 |

## Interbank Foreign Exchange Market (IFEM)

| Tarehe | Idadi (Mn USD) | Juu | Chini | Wastani |
|---|---|---|---|---|
| **13/Feb/2019** | **1.55** | **2,305.80** | **2,293.97** | **2,295.12** |
| 12/Feb/2019 | 1.42 | 2,308.15 | 2,293.94 | 2,295.14 |
| 11/Feb/2019 | 1.10 | 2,307.50 | 2,293.95 | 2,295.19 |
| 8/Feb/2019 | 1.65 | 2,307.00 | 2,293.97 | 2,295.16 |

## Inter-bank Local Money Markets

| Tarehe | Kiasi (million-TZS) | Juu | Chini | Wastani (WAR) |
|---|---|---|---|---|
| **13/Feb/2019** | **36,200** | **5.50** | **4.00** | **5.03** |
| 12/Feb/2019 | 2,000 | 5.00 | 5.00 | 5.00 |
| 11/Feb/2019 | 6,350 | 7.50 | 4.50 | 5.04 |
| 8/Feb/2019 | 76,500 | 8.00 | 4.20 | 4.72 |
| 7/Feb/2019 | 51,200 | 6.00 | 3.50 | 4.19 |
| 6/Feb/2019 | 53,200 | 5.00 | 3.50 | 4.14 |

# Umaskini hadi kulemazwa; sasa atekeleza nadhiri kuhudumia masikini

kupitia michango ya watu na mumewe anachokipata kwenye familia siyo kikubwa, bali jamii inayoguswa kusaidia watoto hao kusoma.

"Asilimia 99 ya watoto tunao walea wana changamoto ya kitabia, lakini mara nyingi natumia silaha ya upendo ili nikiupata moyo wake, tunaanza kuongozana kilicho sawa na ambacho siyo sawa, baadaye wanabadilika na kuwa watoto wazuri sana na wanaishi kwa upendo.

"Tumewagawa kwenye makundi manne, kulingana na umri. Kila kundi lina kiongozi wake, lakini wanajua wao ni familia moja na silaha yao nguzo ni Mungu.

"Kwa mwezi tunatumia Shilingi milioni nne, hapo tuna kila kitu ndani. Wakiondoka kwenda shule, kwa siku moja ni Shilingi 61,000. Kuna wakati wanaenda shule kwa tabu sana.

"Kuna wakati hakuna fedha wanakaa nyumbani. Huwa tunawafundisha kuwa Mungu anaruhusu nyakati zote. Huwa nazunguka shuleni, lakini inafika wakati wanachoka barua zangu na watoto wanafukuzwa na kwa sasa wapo wengine hawajaenda shule," anasema.

### WASICHANA KITUONI

Consoler, anasimulia saikolojia iliyopo kuhusu wasichana anaowalea, ni kwamba wajitahidi kuzitafuta familia zao na inapotokea wanapatikana, wanachokuta ni mzazi wa kike aliumizwa kuhusu uhusiano na baba wa mtoto, kwa hiyo akamchukia mtoto kabisa.

Anaeleza picha iliyoko kituoni: "Anamchukia mtoto kiasi kwamba, akimuona anaona kama anamuona yule mwanamume. Wengi ni wanawake na hawawataki kabisa watoto hawa, kwa sababu waliumizwa na baba zao.

" Najitahidi kuongea nao na kuwafundisha kusamehe na kujenga uhusiano na watoto wao, baadhi wameelewa na huwa wanakuja kuwatembelea."

### WANAZUONI TUMAINI

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Tumaini tawi la Dar es Salaam (TUDARCo), Mary Kafyome, anasema kazi anayoifanya Consoler ni kubwa sana na ishara ya kulipwa na Mungu, hivyo ni vyema watu wakamuunga mkono kusaidia kazi yake kuwasaidia watoto watoto hao kupata elimu.

"Tumekuja kimasomo. Kubwa ni kuwafundisha wanafunzi wetu, umuhimu wa kusaidia jamii inayowazunguka. Ni wajibu wetu kama jamii kuwasaidia watoto wa Kitanzania, watoto hawa wanastahili kusaidiwa na sisi," anasema.

Rai yake kwa vijana hao kambini, ni kutumia vyema fursa ya maisha hayo, kwa kusoma kwa bidii zaidi kutimiza kusudi la Mungu kwenye maisha yao.

"Msikate tamaa bali ng'ang'anieni elimu, ili muweze kutimiza lengo la Mungu katika maisha yenu. Mafanikio yoyote yanapatikana kwa kuweka nia na kufanya kwa bidii," anasisitiza.

Aidha, Kaimu Mkuu wa Idara ya Mawasiliano kwa Umma, Richard Ngaiza, anahimiza umuhimu wa jamii kusaidiana, kwani kuna wahitaji wengi nchini wa huduma za elimu, malazi, chakula na upendo.

"Anachokifanya mlezi huyu na mume wake ni kikubwa sana, ambacho kitakwenda kubadilisha maisha ya watoto wa Kitanzania.

"Someni kwa bidii sana, lakini wanafunzi wa Tumaini waone ni jambo muhimu kusaidia watoto hawa na wengine kupata mahitaji ya msingi," anasema.

### MABINTI KAMBINI

Wasichana wakazi wa kambi hiyo, Varediana Galani, ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha sita, huku akishukuru kufadhiliwa masomo, anasema sadaka kubwa kwa kibinadamu ni kuwa mwenye furaha, hivyo wanaowasaidia wanagusa mioyo yao.

"Kundi la wadogo zetu wenye chini ya miaka 18 walikatiwa bima (Bima ya Afya) na mmoja wa wafadhili, ila kwa ambao tumeshavuka umri huo hatuna bima, hivyo tunatumia fedha taslimu kwenye matibabu ambazo wakati mwingine hakuna," anasema.



## HABARI MBEYA

# Mtumishi Tazara mbaroni tuhuma rushwa ya 200,000/-

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Mbeya, inamshikiria mtumishi mmoja wa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (Tazara) kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Shilingi 200,000 kutoka kwa mfugaji.

Kaimu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, alisema mtuhumiwa anayeshikiliwa anajulikana kwa jina la Bahati Selemani au Rashid Mwakipiti.

Matechi alisema mtuhumiwa alikamatwa na maofisa wa Takukuru Februari 12, mwaka huu akipokea rushwa hiyo kutoka kwa mfugaji mmoja wa Kata ya Chimala wilayani Mbarali, baada ya kumkamata akichunga ng'ombe kwenye hifadhi ya reli.

Alisema lengo la mtuhumiwa kupokea rushwa hiyo ilikuwa kuweka mazingira ya kutomchukulia hatua za kisheria mfugaji huyo kutokana na kosa hilo. Alisema mtuhumiwa alimkamata mfugaji huyo ambaye jina lake halijawekwa wazi Februari 11 mwaka huu na kumtaka ampatie rushwa ya Shilingi 400,000 na hivyo wakakubaliana wakutane kesho yake.

"Fedha hizo alizopewa ilikuwa ni sehemu tu ya kiasi alichokuwa ameomba, lakini kitendo alichokifanya ni kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007," alisema Matechi.

Alisema taasisi hiyo inakusudia kumfikisha mtuhumiwa mahakamani wakati wowote baada ya uchunguzi kukamilika kwa ajili ya hatuza zaidi za kisheria.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kuendelea kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa taasisi hiyo, ili kukomeshwa na wananchi kuendelea kupata huduma wanazostahili kwa mujibu.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa kwa kupiga simu ya bure ya taasisi hiyo ama kwenda moja kwa moja katika ofisi za taasisi hiyo au vyombo vingine vya dola ili wahusika wadhibitiwe. Vilevile aliwashukuru wananchi wa mkoa huo kwa kuendelea kutoa taarifa za watu wanaojihusisha na rushwa, hatua ambayo alidai imesaidia kupunguza taarifa za vitendo hivyo.

Alisisitiza kuwa taasisi hiyo itaendelea kushirikiana na wananchi kwa kutoa elimu juu ya madhara ya vitendo hivyo pamoja na kutunza siri za watu wote wanaotoa taarifa za siri juu ya vitendo hivyo vya rushwa.



Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango (wa tatu kulia), akikabidhi sehemu ya madawati 100 na kompyuta 5 vyenye thamani ya shilingi milioni 5, kwa Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Sophia Kizigo, kwa ajili ya shule za sekondari za Narwi na Rwinga wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mauaji ya watoto yawaamsha polisi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAUAJI ya watoto yaliyotokea hivi karibuni mkoani Njombe, yameliamsha Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, ambapo limeamua kuungana na Umoja wa Jamii Tanzania (Mujata) kuweka mikakati ya kudhibiti vitendo hivyo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema wameamua kuanza kujihami kutokana na kuwa jirani na Njombe.

Alisema kutokana na ujirani wa mikoa hiyo, kuna hatari ya mauaji hayo kuingia mkoani Mbeya na hivyo kuuchafua mkoa pamoja na kukwamisha shughuli za maendeleo.

Matei alisema ameshawasiliana na viongozi wa Mjata kwa ajili ya kuanza kutoa elimu kwa wananchi ili waachane na imani za kishirikina kwa madai kuwa asilimia kubwa ya mauaji yaliyotokea Njombe yalikuwa yanahusishwa na imani za kishirikina.

Alisema watazunguka katika wilaya zote za mkoa huo kwa kuanzia na wilaya korofi za Chunya, Mbarali na Kyela, ili kuhakikisha wanaweka mazingira ya wananchi kuepuka vitendo vya rushwa.

"Haya mauaji yaliyowatesa wenzetu Njombe sisi lazima tufanye utaratibu wa kujihami, tumekubaliana na wenzetu wa Mujata kuanza kutoa elimu kwa wananchi ili waachane na hizi imani za kishirikina ambazo hasa ndio zinasababisha mauaji," alisema Matei.

Kamanda Matei alisema kuna baadhi ya matukio ambayo yamekuwa yakitokea mkoani humo ambayo yanatishia uwezekano wa kutokea vitendo kama vilivyotokea Njombe.

Alisema hivi karibuni lilitokea tukio moja wilayani Kyela ambapo mwanamume alimuua mke wake kisha na yeye akajinyonga na kuwaacha watoto wakibaki yatima.

# Tarura yawapunguzia kero ya usafiri jijini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kata ya Ilomba katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wameanza kupata nafuu ya usafiri baada ya Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) kuanza kutengeneza barabara inayounganisha kata hiyo na barabara kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam) ambayo ilikuwa imeharibika vibaya.

Barabara hiyo ambayo inategemewa na wananchi wa kata hiyo, iliharibika kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha jijini hapa na hivyo kukata mawasiliano ya wananchi hao na maeneo mengine ya jiji hilo. Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wananchi hao walisema barabara hiyo ilikuwa imeharibika kiasi kwamba hata pikipiki zilikuwa haziwezi kupita na hivyo kuwafanya wakose huduma muhimu za kijamii ikiwamo wanafunzi kwenda shuleni.

Julius Mwalingo, alisema uharibifu wa barabara hiyo pia ulikuwa unahatarisha makazi ya wananchi hao kutokana na maji yaliyokuwa yanajaa kusababisha mmomonyoko wa ardhi.

Alisema wenye magari walikuwa wanashindwa kuyatumia magari yao na hivyo kulazimika kutembea kwa miguu kwenda kupanda pikipiki za magurudumu matatu (Bajaji) eneo la mwisho wa lami ambako ni mbali.

"Tunashukuru Tarura kwa kusikia kilio chetu haraka na kuja kuturekebishia barabara maana ilikuwa imeanza kutunyima usingizi, uharaka wa wataalamu hawa unaonyesha namna rais wetu Magufuli alivyoona mbali kuunda chombo hiki," alisema Mwalingo.

Naye Tito Laison alisema barabara hiyo ilikuwa imechimbika na kusababisha makazi yao kuwa hatarini kubomoka kutokana na mmomonyoko kuanza kuzisogelea nyumba zao. Alisema wananchi walianza kujihami kwa kujaza mchanga kwenye mifuko na kuziba makorongo yaliyokuwa yamejitokeza ili yasiendelee, lakini bado kutokana na wingi wa maji mifuko hiyo ilikuwa haifui dafu kutokana na kusombwa na maji.

Alisema athari za mafuriko kwenye barabara hiyo ilikuwa kubwa kutokana na eneo hilo kuwa na ardhi yenye asili ya mchanga ambayo ni rahisi kuchimbika endapo maji yakizidi.

Laison alisema baada ya barabara hiyo kuharibika waliwapigia watendaji wa Tarura na wakafika ndani ya muda mfupi kuangalia uharibifu huo na wakaanza kurekebisha ndani ya muda mfupi.


"Tulianza kujihami kwa kuweka mifuko na mawe kwenye korongo lililojitokeza ili lisiendelee, lakini bado ilisombwa, tukaamua kuwapigia Tarura na walikuja haraka sana wakaanza kazi ya kurekebisha," alisema Laison.

Mwakilishi wa Meneja wa Tarura Mkoa wa Mbeya, Jacob Mwamanga, alisema barabara kama hizo zinatengenezwa kwa mfumo wa dharura kwa madai kuwa majanga hayo huwa yanatokea bila kukusudiwa.

Alisema kwa sasa wanafanya matengenezo ya haraka ili wananchi waendelee na shughuli wakati wanajiandaa na mipango ya kuleta suluhu ya kudumu.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, aliwataka Tarura kuendelea kurekebisha barabara zote zinazolalamikiwa na wananchi ili kuendelea kujenga imani kwa wananchi kwa madai kuwa barabara hizo zinajengwa kwa kodi zao.

Alisema kwa sasa wanahangaika kugawa vitambulisho vya wajasiriamali vilivyotolewa na Rais Dk. John Magufuli, hivyo miundombinu ya barabara lazima iwe rafiki kwao ili waweze kusafirisha bidhaa zao kwenda sokoni.





# Diwani kizimbani kisa tuhuma kughushi kiwanja cha Malecela

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATUHUMIWA wa kesi ya kughushi hati ya kiwanja cha Waziri Mkuu wa zamani, John Malecela, wamefikishwa mahakamani na kusomewa mashtaka nane.

Kesi hiyo ilisomwa juzi mchana katika Mahakama ya Wilaya ya Dodoma mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Godfrey Pius.

Katika shauri hilo, Diwani wa Kata ya Makole, Abel Shauri na wenzake watatu wanashtakiwa kwa kughushi nyaraka na kuuza kiwanja cha Malecela namba 26 kitalu J, kilichopo mtaa wa Area D ambapo walijipatia Sh. milioni 35.

Watuhumiwa wengine ni Jackson Ndahani (msaidizi wa Malecela), Shaban Msovela na Elias Stephen.

Wakisoma maelezo ya kesi hiyo mbele ya Hakimu huyo, Waendesha Mashtaka wa Serikali, Lina Magoma na Morisi Sarara, waliiambia mahakama kuwa watuhumiwa hao walitenda kosa hilo kati ya Juni na Agosti mwaka 2018.

Walidai kuwa washtakiwa waligushi nyaraka na kubadili jina katika kiwanja hicho kinachomilikiwa kwa jina la John S. Malecela ambacho kilitolewa kwa ofa namba CDA/ED/LA-15/53243 ya Februari 16, 2010.

Magoma alidai makosa hayo yanaangukia kifungu namba 333 na 335 (b) na 337 vya kanuni ya adhabu sura ya 16 ambapo walimuuzia Godfrey Gao kiwanja walichojua kuwa siyo mali yao.

Wakili Magoma aliyataja baadhi ya makosa yanayowakabili washtakiwa hao ni kutengeneza nyaraka ya uongo, kuandika barua ya uongo kutoka kwa Malecela, kuandika nyaraka za uhamisho za uongo, kubadili nyaraka halisi kuwa za uongo na kujipatia pesa kwa njia ya udanganyifu hivyo akaomba washitakiwa wanyimwe dhamana.

Wakili wa utetezi, Francis Stephen alitaka wateja wake wapatiwe dhamana, na baada ya malumbano ya kisheria, hakimu aliamuru kesi hiyo isikilizwe leo kwa ajili ya uamuzi.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), Elius Mwakalinga (kushoto), akikagua moja ya miradi inayojengwa na Wakala wa Majengo nchini (TBA), kwa kushirikiana na vikosi vya ujenzi na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), mjini Dodoma jana. **PICHA: WUUM**

# Vijana watajwa kuwa nguzo muhimu kufikia uchumi wa kati

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetakiwa kuwatumia vijana kikamilifu ili Tanzania iweze kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Mpango wa Kuendeleza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania(SAGCOT), Geoffrey Kirenga.

Alikuwa akizungumza na vijana walioko kwenye mradi wa vijana wa Feed the Future Tanzania Advancing Youth, unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Misaada la Marekani (USAID).

Alisema hakuna nchi inayoshinda vita kwa kutumia askari wazee bali hutumia kitu cha thamani kushinda ikiwemo vijana.

"Vita yoyote ina gharama zake na gharama ya juu ni kupoteza uhai wa askari ili ushinde unatakiwa kutumia kitu chako cha thamani, sasa tuko kwenye vita ya uchumi katika kufikia uchumi wa kati tunawajibika kuwatumia vijana ili tushinde," alisema.

Alisema kwa sasa serikali inawasikiliza na kuwatambua vijana na biashara nyingi kwasasa zinaongozwa na vijana.

Pamoja na hayo, aliwataka vijana kutumia simu zao kuangalia fursa za kibiashara kwenye mitandao ili waweze kujikwamua kiuchumi.

"Makampuni tunayofanya nayo kazi yanayoongozwa na vijana yana fikra mpya katika kazi, hivyo vijana kuna fursa nyingi lakini mna kazi ya kuzijua na kuzitambua na kuwa focus," alisema.

Mwakilishi wa USAID, Michelle Corzine, alisema kufikia mwaka 2025 Watanzania wa umri wa 15-35 watakuwa zaidi ya asilimia 35 ya idadi ya watu wote hivyo ni muhimu hatua zikachukuliwa kukabiliana na wingi huo wa vijana.

Aidha, alisema ni muhimu kutenga ardhi kwa ajili ya vijana hivyo watendaji wa serikali wahakikishe wanawapatia fursa vijana kuzalisha.

Kadhalika, alisema kuna changamoto ya upatikanaji mdogo wa kifedha inayowakabili vijana.

"Serikali ya Marekani inashirikiana kufanya kazi na serikali ya Tanzania kuimarisha ushiriki wa vijana katika kukuza uchumi kwa kutambua njia za kuwaingiza katika sekta ya kilimo,' alisema.

Naye Rais wa Chama cha Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Octavian Mshio, aliwataka vijana kutumia fursa kujiunga na TCCIA ili waweze kutumia fursa zilizopo.

Alisema vijana wengi wamenufaika kwa kupata mitaji kupitia vikundi walivyojiunga na kuwataka kutumia vizuri nafasi waliyopewa na USAID ili waweze kujikwamua.

"Vijana ndio idadi kubwa ya watu waliopo nchini, ukiongelea uwekezaji wa kilimo bila kuwashirikisha vijana inakuwa ni changamoto kwenye upatikanaji wa ajira," alisema.

Alitoa wito kwa serikali kuhakikisha vijana wanapewa ardhi kwenye maeneo ya vijijini, ili waweze kufanya kilimo cha kisasa kitakachowawezesha kujikwamua kiuchumi.

Kwa upande wake, Mkuu wa kitengo cha kilimo kutoka Taasisi ya kuendeleza huduma za kifedha nchini (FSDT), Mwombeki Baregu, alisema taasisi hiyo inatambua umuhimu wa vijana na kuwashirikisha kwenye mifumo ya kifedha.

# Waziri awakumbuka wazazi watarajiwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIKA jitihada za kuhakikisha wanawake wanajifungua salama jijini Dodoma, Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, ametoa vifaa vya kujifungulia 350 na mashuka 100 ili waweze kupata huduma bora.

Akikabidhi vifaa hivyo katika Kituo cha Afya Makole, Mavunde alisema ametoa vifaa hivyo kwa ajili ya vituo vyote vya afya na zahanati ambazo zinatoa huduma ya wanawake kujifungua.

"Natambua baadhi ya wanawake wamekuwa wakikosa vifaa vya kujifungulia kutokana kukosa fedha, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya sikukuu ya wapendanao nimeona nitoe msaada huu ili kukabiliana na vifo vya akina mama na watoto vinavyotokana na uzazi," alisema.

Mavunde ambaye pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, alisema mifuko hiyo ina aina 10 za vifaa kwa ajili ya wanawake hao.


"Mimi upendo wangu ni kuwajali watu wenye mahitaji maalumu nimewaletea mifuko 350 yenye vifaa vyote vya kujifungulia ambapo mfuko mmoja gharama yake ni Sh. 21,000 pia nimetoa mashuka 100 pamoja na maji kwa ajili ya wagonjwa," alisema.

Aidha, alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa ahadi yake wakati wa kampeni kwamba atahakikisha anaboresha sekta ya afya na ni mwendelezo wa utoaji vifaa kwa sekta hiyo.

Mganga wa Halmashauri ya Jiji hilo, Dk. Gatete Mahava, alisema idadi ya wanawake waliotarajiwa kujifungua mwaka 2018 walikuwa 17,685 ambapo hali halisi jumla ya wanawake 19,496 sawa na asilimia 110 walijifungulia katika vituo vya afya.

Dk. Mahava alisema wanawake 3,462 walifanyiwa upasuaji wa dharura kwenye vituo mbalimbali vya kutolea huduma Jijini humo.

Alisema kwa sasa wanakabiliwa na changamoto za upungufu wa mashine za kupimia msukumo wa damu, mashine ya kupimia wingi wa damu kwa wajawazito pamoja na machela za kubebea wagonjwa.





# Shein aagiza wataalamu afya kupelekwa Kianga

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameiagiza Wizara ya Afya kupeleka wataalamu na huduma zote muhimu katika Kituo cha Afya kilichoko Kianga, mara kitakapoanza kuhudumia wananchi.

Akizungumza baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa kituo hicho, Dk. Shein, alisema haitakuwa vyema kuona kinasitisha huduma kutokana na ukosefu wa wataalamu.

Alisema mpango wa serikali kuongeza vituo vya afya nchini, unalenga kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi.

Rais Shein alisema ni muhimu jamii inapokumbwa na changamoto za kiafya, ipate huduma hizo kwenye maeneo yake.

Kwa kutambua hilo, alisema serikali imeona ni vyema kujenga kituo hicho kupitia Mradi wa Kusaidia Kaya Maskini (Tassaf).

Aliwataka wananchi kujiepusha na uharibifu au hujuma katika kituo hicho ili kitoe huduma kwa muda mrefu bila kuhitaji gharama kubwa za matengenezo ya miundombinu yake.

Alisema pamoja na wananchi kuendelea na utamaduni wa kupata huduma za afya kupitia njia za jadi, kuna umuhimu mkubwa wa kukitumia ipasavyo kituo hicho, ambacho kitaendeshwa kupitia afya ya msingi chini ya mfumo wa ugatuzi.

"Sisemi yale ya asili msifanye, sijasema hivyo, yale fanyeni, lakini pia hospitalini mje, sitaki kuondosha imani za watu," alisema. Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Haji Omar Kheir, aliahidi kushirikiana kikamilifu na Wizara ya Afya kuandaa mkakati kupata wataalamu bora wa kutoa huduma katika kituo hicho.

Katika hatua nyingine, Rais Shein, aliendelea na ziara yake kwa uzinduzi wa kituo cha kukaushia dagaa cha Kihinani.

Akizungumza na wananchi na wajasiriamali baada ya kukagua mashine ya kukaushia dagaa, Rais Shein aliwataka kuendelea kuuza bidhaa zilizo bora ndani na nje ya nchi bila woga.

Alisema Zanzibar imebarikiwa kuwa na bahari yenye rasilimali nyingi, hivyo ni vyema ikatumika kuwakomboa wananchi kiuchumi. Aliitaka Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kubuni njia bora zaidi kuwawezesha wajasiriamali na wafanyabiashara wa dagaa kutumia mbinu bora za ukaushaji ili kuzalisha bidhaa bora na kukidhi soko la nje.




Mkurugenzi Mtendaji wa Khulisa Social Solutions, Lesley Ann Van Selm (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu kuanzisha ushirikiano rasmi na Shirika la Under The Same Sun (UTSS), ili kuwafikiwa watu wenye ualbino na kutoa taarifa ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Ualbino itakayofanyika Februari 18 hadi 20, mwaka huu, jijini Johannesburg, nchini Afrika Kusini. Katikati ni Mkurugenzi wa Miss Albinism Zimbambwe Trust, Brenda Mutzimu na Ofisa Ushauri katika masuala ya ajira wa UTSS, Josephat Igembe. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Asasi zamtaka Lugola achukue hatua polisi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

ASASI za kiraia visiwani Zanzibar, zimemtaka Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, kuchukulia hatua dhidi ya askari polisi wanaodaiwa kuwavamia na kuwapiga maofisa wa Mamlaka ya Kudhibiti Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (Zaeca).

Mkurugenzi wa Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar (Zafela), Jamila Mahmoud, alitoa rai hiyo alipotoa tamko la pamoja la muungano wa asasi za kiraia nchini kwenye Ukumbi wa Babari Maelezo visiwani Zanzibar.

Alisema kitendo kinachodaiwa kufanya na askari hao si cha kiungwana na kinahitaji kufanyiwa uchunguzi na wahusika kuwajibishwa ili haki itendeke.

Alisema asasi za kiraia hawaungi mkono suala la kumalizwa kwa kauli za kukemea vitendo vya aina hiyo, badala yake zichukuliwe hatua za kisheria ili kutoa fundisho kwa askari na watu wengine wanaokiuka misingi iliyowekwa.

"Kwa kuzingatia haki za binadamu na usawa wa binadamu, ni lazima wahusika wadhibitiwe na kuwajibishwa," alisema.

Aliongeza kuwa kitendo kinachodaiwa kufanyika dhidi ya mamlaka hiyo nyeti, kinazitia hofu hata asasi za kiraia ambazo zitakuwa na woga wa kufuatilia kesi zinazowahusu polisi.

"Kama polisi wamethubutu kuingia na kuvamia taasisi ya serikali ambayo ina mamlaka kisheria, je, sisi asasi za kiraia tutakuwa katika hali gani?" Mahmoud alihoji.

"Tunakwazika na kuingia hofu, pindi likitokea tukio linalomhusu askari, turudi nyuma kuripoti kwa kuhisi kuja kuvamiwa." Alisema suala hilo kumalizwa kwa mazungumzo ya mezani, kutasababisha kushuka kwa hadhi ya ZAECA.

Mwanzoni mwa mwezi, askari wa Jeshi la Polisi walidaiwa kuvamia ofisi za mamlaka hiyo na kuwapiga maofisa wake baada ya mmoja wa askari wa jeshi hilo kunaswa akipokea rushwa.

# Mbunge alia wanaoficha watoto wenye ulemavu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MBUNGE wa Jimbo la Dimani, Juma Ali Juma, ameitaka jamii kuacha tabia ya kuwaficha watoto wenye ulemavu wakiwamo wasiiona na wenye ulemavu wa ngozi, kwa kuwa wana haki kama watoto wengine.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na viongozi wa Jumuiya ya Wasiiona Zanzibar (Zanab) Wilaya ya Magharibi B Unguja.

Alisema wananchi wanapaswa kufahamu kuwa wote ni walemavu watarajiwa, hivyo ni vyema kujiweka vizuri na kujiandaa kisaikologia.

Alisema ulemavu si mwisho wa maisha, na watoto wanaozaliwa na ulemavu wana uwezo mkubwa na kufanya mambo mazuri na hata kuwazidi wasio na ulemavu.

"Msiwafiche watoto hawa, tuwaunganishe katika jamii ili nao waweze kutoa mchango wao kwa serikali yetu na hata jamii inayotuzunguka," alisema.

Mbunge huyo alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hazijawaacha watu wenye ulemavu kwa kuwa zimewajengea mazingira mazuri kuhakikisha wanashiriki katika mambo ya maendeleo.

Aliahidi kuwa balozi wa kuwasemea watu wenye ulemavu ili wasadiwe kufikia lengo walilokusudia kwa kuwa wanahitaji uangalizi wa hali ya juu.

Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Wilaya ya Magharibi B, Jamila Borafya Hamza, alisema kukamilika kwa ofisi yao kutarahisisha utendaji wao wa kazi.

Alisema wana mpango wa kuanzisha programu ya kuwafichua watu wenye ulemavu wakiwamo wasioona na wenye ulemavu wa ngozi waliofichwa kwa kupita nyumba kwa nyumba ili wapate haki zao za msingi.

"Kitu kilichotusukuma kufanya hivi, tumegundua kuwa watoto wengi wanafichwa na wanakosa haki zao za msingi ikiwamo elimu bila kufahamu kuwa nao wanahaki ya kupelekwa skuli na wale ambao hawapo skuli, basi wanashiriki katika kazi za kijamii ili waweze kujitegemea wenyewe," alisema.

Kiongozi huyo alisema mzazi yeyote atakayebainika kumficha mtoto wake, atachukuliwa hatua kwa kuwa lengo la jumuiya yao ni kuona inafika wakati wasioona na wenye ulemavu wa ngozi wanajitegemea wenyewe bila ya kutegemea kufanyiwa kila kitu.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 11 Feb**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 12 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 13 Feb**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 14 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 15 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 16 Feb**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Ode To Joy
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Ground Zero
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 17 Feb**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Telenovela: Ode To Joy
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 11 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Shamba shape up
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 12 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 13 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Kipindi Maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 14 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Hatua
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Jungu Kuu
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo rpt: Riziki
18:30 Kipindi Maalum: Ewura
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 15 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: TCRA
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi maalum: Tanesco
13:30 Kipindi Maalum rpt - TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Mapishi
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Uchumi na biashara
19:00 Kipindi maalum: TCRA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 16 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Hatua
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 17 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Green Light
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Green light 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)


EATV




LEO USIKU SAA 3:00



IJUMAA
10:59 Jikoni Na Jane
11:00 DADAZ (live)
13:30 Kali Za Wana
14:00 Radio:PlanetBongo Live
15:00 FUNGUKA
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 Kurasa
18:00 eNewz
18:30 Skonga
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 Friday Night Live

FRIDAY NIGHT LIVE (FNL) ni mlipuko wa burudani unaounganisha EATV na East Africa Radio kukuletea Muziki mnene, burudani ya kupagawisha na mahojiano na wageni wanaoalikwa kutoka ndani na nje ya nchi.

eastafrica RADIO
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise

88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

| TIME | MONDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

| TIME | TUESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | WEDNESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | THURSDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | FRIDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | SATURDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

| TIME | SUNDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
## FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

# 500 wakimbia machafuko DRC, waingia Uganda

**KINSHASA,** Congo

MAPIGANO ya kikabila yaliyotokea mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo-DRC wiki iliyopita, yamesababisha zaidi ya watu 500 kukimbilia usalama nchini Uganda.

Zaidi ya raia 500 kutoka Congo waliwasili Uganda wakikimbia mapigano ya kikabila yaliyozuka wiki iliyopita.

Wakimbizi hao wamewafahamisha maofisa wa Uganda pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa linalowahudumia Wakimbizi (UNHCR) kwamba mapigano hayo yaliyozuka kati ya jamii za Lendu na Bagerere yamesababisha eneo la mashariki mwa Congo kuwa katika hali ya sintofahamu.

Makundi hayo ya wakimbizi kutoka jimbo la Ituri Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia yanafanya safari za hatari kuvuka ziwa Albert lililoko kwenye mpaka wa nchi hizo mbili wakitumia mitumbwi isiyokuwa imara.

**Makundi hayo ya wakimbizi kutoka jimbo la Ituri Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia yanafanya safari za hatari kuvuka ziwa Albert lililoko kwenye mpaka wa nchi hizo mbili wakitumia mitumbwi isiyokuwa imara.**

Wengi wao ambao ni wanawake na watoto wameshuhudiwa wakiwa na mizigo yao hususani magodoro, na kwamba Kwa mujibu wa wakimbizi hao, mapigano hayo ni kati ya kikabila ya jamii ya Lendu na Bagerere.

Kinachowatia hofu na wasiwasi viongozi wa wilaya za Hoima na Kikuube ni uwezekano wa kuzorota kwa hali ya usalama.

Inahofiwa huenda kuna uwezekano wa wakimbizi kuingia Uganda wakiwa wamejihami kwa silaha.

Wasiwasi mwingine ambao wimbi hilo jipya la wakimbizi kutoka DRC ni kuhusiana na jinsi wanavyowasili bila kupitia njia rasmi za mipakani ambako wangepimwa kabla ya kuchangamana na jamii za Uganda.

Wakazi wana wasiwasi kuwa kuna uwezekano wa milipuko ya magonjwa ya ebola na kipindupindu, kwa kuwa wakimbizi hao wanatokea sehemu ambako ugonjwa huo umeripotiwa hivi karibuni mashariki mwa nchi yao.

Uganda imekubaliana na hali hiyo kwa kutuma majeshi kuhakikisha kunakuwapo kwa usalama katika maeneo ya mpakani hasa kwenye fukwe za ziwa Albert, huku makundi ya maofisa wa afya wakipelekwa kuwapima wakimbizi hao kabla ya kuwasafirisha kwenda kwenye kambi rasmi ya wakimbizi ya Kyangwali.

Shirika la Umoja wa Mataifa linalowahudumia wakimbizi limefafanua kuwa hata kabla ya kundi hilo la wakimbizi kuanza kuwasili Uganda, kila siku watu 113 wamekuwa wakiwasili kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo tangu mwanzoni mwa mwaka huu.

Inakisiwa kuwa kuna wakimbizi 240,000 kutoka nchi hiyo jirani walioko Uganda, idadi kubwa ikiwa imetokea majimbo ya Kivu Kaskazini na Kivu Kusini. **DW**



Mojawapo ya ndege za kivita za Marekani zinazotoa msaada kwa ndege za muungano unaoongozwa na Saudia katika vita vya Yemen. **PICHA: DW**

# Polisi Kenya wakutwa na hatia ya mauaji

**NAIROBI,** Kenya

MAKAMANDA watano wa polisi walioongoza operesheni ya mwaka 2017, ambapo mtoto kwa jina la Baby Pendo, aliuawa mjini Nyalenda kaunti ya Kisumu, wamepatikana na hatia ya kifo chake.

Uchunguzi ulioongozwa na hakimu mwandamizi, Beryl Omollo, ulitoa uamuzi huo jana mjini Kisumu.

Makamanda waliokutwa na hatia ni Linah Kosgei, Benjamin Koima, Christopher Mutune Maweu, Titus Yoma na John Thiringi.

Wakati wa operesheni hiyo iliokumbwa na utata, Yoma alikuwa kamanda wa polisi wa kaunti ya Kisumu, Maweu alikuwa OSPD wa Kisumu Mashariki, Thiringi alikuwa OSC wa Kisumu ya Kati, Koima akisimamia Kisumu Magharibi, huku Kosgei akiongoza kituo cha polisi cha Nyalenda.

Mtoto huyo aliyekuwa na miezi sita aliuawa ndani ya nyumba ya babake na maofisa wa polisi wa kitengo cha kukabiliana na ghasia ambao walikuwa wakijaribu kuzima maandamano yalioanza baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi mkuu mwaka 2017.

Katika uamuzi wake, hakimu huyo pia aliagiza mkurugenzi wa mashtaka, Noordin Haji, kuwachunguza maofisa 31 wa kikosi cha GSU ambao aliwataja kuwa washukiwa muhimu.

Maofisa wengine 20 wa polisi ambao walikuwa chini ya usimamizi wa Kosgei mjini Nyalenda pia watachunguzwa na mahakama hiyo. Wazazi wake Joseph Abanja na mkewe Lencer Achieng, walisema kuwa walikuwa wakiomba maajabu ya 'valentines' na ni hicho walichopata.

Wakati wa kusikilizwa kwa kesi hiyo makamanda hao walilaumiana, huku hakuna hata mmoja akitaka kuchukuwa lawama. Wakati mwingine maofisa hao walitaka kushikana mashati mahakamani.

Baby Pendo alifariki Agosti 2017, baada ya kudaiwa kupigwa kichwani na maofisa wa polisi kufuatia ghasia zilizokumba kaunti ya Kisumu baada ya Rais Uhuru Kenyatta kutangazwa mshindi wa uchaguzi huo.

Katika kesi hiyo, maofisa wa polisi hao walishutumiwa kwa kuvunja na kuingia katika nyumba ya Abinja katika Mtaa wa Mabanda wa Nyalenda.

Mtoto huyo alifariki siku tatu baadaye wakati alipokuwa akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Aga Khan mjini Nairobi. **BBC**

## Wafanyakazi waitisha mgomo

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

CHAMA kikuu cha wafanyakazi nchini Afrika Kusini (Cosatu), kimeitisha mgomo wa kitaifa dhidi ya serikali.

Sababu kubwa ya kuitisha mgomo huo ni kutaka kufutwa kwa muswada wa Rais Cyril Ramaphosa, ambao unataka kurekebisha na kubinafsisha baadhi ya kampuni za umma.

Cosatu ni mmoja ya washirika wa kihistoria wa chama tawala ANC, na inashiriki katika muungano serikalini.

Wito huo wa Cosatu ni ishara kwa ANC ikiwa imesalia miezi mitatu kabla ya uchaguzi wa urais.

Akizungumza na waandishi wa habari mweka hazina wa Cosatu, Thabang Sonyathi, alisema kilichosababisha maelfu ya wafanyakazi wa Afrika Kusini kuingia mitaani ni mpango wa urekebishaji wa kampuni ya umeme ya Eskom.

"Tunaona mpango huu kama njia ya kuwezesha ubinafsishaji wa Eskom na hatua za kibaguzi. Na wale ambao watakabiliwa na hali mbaya ya maisha ni wafanyakazi wa kawaida," alisema Sonyathi.

Kwa mujibu wa Thabang Sonyathi, tabia ya ANC imewachosha wanachama wa Cosatu, ambao wanaweza kubadilisha kura zao kwenye uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Mei. **RFI**

## Bunge Marekani lataka misaada kusitishwa

**WASHINGTON,** Marekani

BARAZA la wawakilishi nchini Marekani jana, liliidhinisha azimio litakalofikisha mwisho wa uungaji mkono wa Marekani kwa muungano wa kijeshi unaoongozwa na Saudi Arabia katika vita nchini Yemen.

Hatua hiyo imechukuliwa wakati wabunge wengi wakitaka kumlazimisha Rais Donald Trump wakati yeye akiimarisha sera zake kuelekea nchi hiyo ya kifalme.

Ni mara ya kwanza kwa baraza hilo la wawakilishi kuunga mkono azimio la madaraka ya vita, lakini kura hiyo iliyoungwa mkono na wabunge 248 kwa 177 waliopinga.

Ni wabunge 18 tu wa chama cha Rais Trump cha Republican katika baraza hilo la wawakilishi waliojiunga na wa- Democrat 230 kuunga mkono azimio linalotaka Marekani kuzuia jeshi kujiingiza katika uhasama na Yemen.

Mojawapo ya misaada ambayo wabunge wamekuwa wakiipinga ni pamoja na kujaza mafuta katika ndege zinazofanya mashambulizi katika vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Yemen bila ya idhini ya wabunge.

Wabunge wa Democrat na Republican walilirejesha tena azimio la madaraka ya kivita wiki mbili zilizopita kama njia ya kutuma ujumbe mzito kwa utawala wa Riyadh juu ya maafa ya binadamu na kuishtumu mauaji ya mwandishi wa habari wa Saudia, Jamal Khashoggi. **DW**

# MOI yaanza upasuaji nyonga, uti wa mgongo

**Na Mary Geofrey**

KWA mara ya kwanza Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), imefanya upasuaji wa maungio ya nyonga na uti wa mgongo kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka India.

Upasuaji huo utafanywa kwa siku tatu na madaktari bingwa wa MOI na wataalamu kutoka Hospitali ya Zydus ya India na jumla ya wagonjwa sita wenye matatizo magumu ya nyonga na uti wa mgongo watafanyiwa upasuaji.

Akizungumzia upasuaji huo jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alisema watapandikiza nyonga bandia na upasuaji wa mgongo kwenye eneo la shingoni kupitia upande wa mbele.

Alisema Oktoba mwaka jana, waliingia mkataba wa ushirikiano na hospitali hiyo kwa lengo la kubadilisha uzoefu wa wataalamu na kufanya kambi za upasuaji kwa wagonjwa kama walivyofanya jana.

Alisema pia mkataba huo ulihusu kuwaona wagonjwa wa kliniki na kuwafundisha wataalamu wa nchini kupitia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

"Novemba mwaka jana walikuja madaktari bingwa kutoka India, wakaona wagonjwa wa kliniki na mwaka huu sasa ndio tumeanza kazi rasmi," alisema Dk. Boniface.

Alisema wameanza utekelezaji wa mkataba huo na lengo kubwa ni kuifanya MOI kufikia viwango vya kimataifa vya utoaji huduma kama wanavyofanya India.

Alisema pia lengo ni kuwafanya wagonjwa wote nchini wapate huduma kwa gharama nafuu bila kusafiri kwenda nje.

Akizungumzia tofauti ya upasuaji wa nyonga walizowahi kufanya na wanazofanya kwa siku tatu, alisema hizi zinahusu maeneo magumu ambayo nchini hakuna utaalamu wa kufanya vyema hivyo mgonjwa angelazimika kusafiri nje. Alisema upasuaji wanaofanya ni wa kisasa wa mbinu mpya kutoka kwa wataalamu wengine.

"Huu ni upasuaji mgumu ambao nchini hatukuwa na utaalamu wa kutosha na wanapotupatia mafunzo haya kwa siku tatu, wakiondoka na sisi tutaweza kufanya wenyewe," alisema.

Pia alisema mfumo wanaotumia unatumia muda mfupi tofauti na awali na gharama nazo zinapungua kwa sababu zinategemea na muda anatumia mgonjwa kwenye upasuaji.

Dk. Boniface alisema awali walifanya upasuaji kwa saa nne, lakini sasa wataanza kufanya operesheni kwa saa mbili na nusu hadi saa tatu.

"Gharama za kufanya upasuaji wa mgongo kwa mgonjwa mmoja inatumia Sh. milioni nne hadi tano, lakini kulingana na muda anaokaa katika chumba cha upasuaji," alisema na kuongeza:

"Lakini kwa sasa tunapata utaalamu utakaotuwezesha kutumia muda mfupi kufanya upasuaji na kusaidia gharama kupungua pia."

Kwa upande wake, Daktari Bingwa wa Mifupa wa MOI aliyebobea kwenye upandikizaji wa nyonga bandia, Dk. Violeth Lupondo, alisema mbinu wanazopata zitawasaidia kuendelea kutoa huduma hizo hata baada ya madaktari kutoka Zydus kuondoka.

"Huwa tunafanya kila siku aina hizi za upasuaji, lakini huu wa leo ambao tunafanya na wenzetu kutoka Zydus ni wa tofauti na mgumu," alisema Dk. Lupondo.




Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Mawasiliano), Mhandisi Atashasta Nditiye (wa pili kulia), akizungumza na Menejimenti ya Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), alipotembelea shirika hilo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya TTCL, Mhandisi Omary Nundu na Naibu Katibu Mkuu Wizara hiyo Sekta ya Mawasiliano, Dk. Jim Yonaz. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ekari 42 za polisi zagawiwa wananchi

**Na Munir Shemweta,** MWANZA

SERIKALI imekonga nyoyo za wananchi baada ya kuwapatia ekari 41.67 kati ya 58.4 katika eneo la mgogoro la kambi ya Jeshi la Polisi ya Kigoto iliyoko Kata ya Kurumba jijini Mwanza.

Kutokana na hatua hiyo ya serikali, jeshi hilo sasa litabakiwa na ekari 16.73 katika eneo hilo lililokuwa na mgogoro kati ya wananchi na polisi.

Tamko la kutwaa eneo hilo lilitolewa jana na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, baada ya Rais John Magufuli, kuamua wananchi kupatiwa ekari hizo kutokana na mgogoro uliodumu kwa muda mrefu.

Eneo la kambi ya polisi la Kigoto lenye kaya 461 na nyumba 664 kwa muda mrefu limekuwa na mgogoro baina ya wananchi na jeshi hilo, baada ya wananchi kuvamia na kuliendeleza ikiwamo kujenga nyumba za makazi.

Mabula alisema Rais amesikia kilio cha cha wananchi wa eneo hilo na kuamua kuwapatia umiliki na kusisitiza kuwa mara nyingi Rais amekuwa mtetezi wa wanyonge.

Huku akishangiliwa na wananchi wa eneo hilo ambao walikuwa na furaha isiyo na kifani, Mabula alisema kuanzia sasa wananchi hao watakuwa wamiliki halali na kwamba eneo hilo sasa litapimwa upya kwa kuwa kuna maeneo ndani ya kambi hiyo yalipimwa kimakosa. Pia alisema eneo hilo litarasimishwa na kuwataka wananchi kuonyesha ushirikiano wakati wa mchakato huo ambao utawafanya wananchi hao kuwa na hati zitakazowazesha kukopa fedha benki.

Hata hivyo, Mabula alisema eneo la ekari 16 ambalo halijavamiwa litabakia kuwa mali ya Jeshi la Polisi na wananchi hawaruhusiwi kuendesha shughuli yoyote na kuwataka kutii sheria.

Naibu Waziri alisema Manispaa ya Ilemela italitafutia eneo lingine Jeshi la Polisi kwa ajili ya kuendesha mafunzo ya mbinu za medani na kuimarisha kikosi cha wanamaji na shughuli za chuo cha wanamaji Butimba mkoani Mwanza.

# Serikali yavikumbuka vituo utengemao watoto walemavu

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amesema serikali itahakikisha vituo vyake vya afya 510 vinakuwa na vituo maalum vya utengamao kwa ajili ya watoto wenye ulemavu katika kipindi cha miaka mitatu.

Mwalimu aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua Kituo kipya cha utengamao wa watoto wenye ulemavu, kilichojengwa eneo la Kawe kitakachojulikana kama Community Based Rehabilitation Centre.

Kituo kicho kipya chenye uwezo wa kuchukua watoto 300 kimejengwa chini ya mradi wa Shirika la Comunita Solidali nel Mondo kutoka Italia na Shirika la Ivrea Sisters Congregation lililopo Kawe ambapo hadi sasa jumla ya watoto 175 wameshaandikishwa.

Waziri Mwalimu alisema amevutiwa na suala hilo na kuwaagiza watendaji wake walioongozana naye kwenye uzinduzi huo wahakikishe ndani ya mwezi mmoja wanamwandikia dokezo ambalo litamwezesha kwenda kutafuta fedha za utekelezaji.

Mwalimu aliwaeleza wafadhili hao kuwa hawawezi kujua jinsi gani alivyoguswa na mradi huo walioufanya ili kuwezesha watoto wenye ulemavu kupata huduma zitakazowawezesha kujitegemea na kupunguza mzigo kwa wazazi na walezi wao.

Alisema endapo angelijua miaka miwili iliyopita ambako kulijengwa hoja ya kuboresha vituo vya afya ili vitoe huduma za uzazi wa dharura ikiwemo upasuaji, suala hilo lingekuwa kwenye utekelezaji.

"Wizara tulikaa tukaandika andiko kwa nini wanawake wajawazito wanakufa, moja ya sababu tuliyoiona ni kwamba hakuna huduma ya upasuaji na huduma ya damu salama, hivyo katika vituo 350 kati ya 510 tunavyoviboresha tumejenga chumba cha upasuaji, wodi ya wazazi, maabara ya damu na nyumba moja ya mtumishi," alisema.

"Kwa kufanya hivi tutawafikia wanawake na walezi wengi, ninaahidi na bahati nzuri siogopi kushindwa, tunaweza tusipate 510 lakini tunaweza kuanza na vituo 50 kwanza na baada ya miaka mitatu tukafikia vituo vyote," alisema.

Alisema kama wameweza kuweka jengo kwa ajili ya upasuaji, wodi ya wazazi watahakikisha jengo la utengamao linakuwepo vituoni.

Pia aliwaagiza maofisa Ustawi wa Jamii kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa makao yanayotumika kulelea watoto wenye ulemavu na kutoa ushauri unaotakiwa wafanye. Balozi wa Italia nchini, Roberto Mengoni, alisema kwenye maisha kuna njia mbili za kuishi, moja ni kwa miujiza na nyingine hakuna miujiza.

Alisema kituo hicho kwa ajili ya watoto hao ni miujiza na anaamini watoto wa Tanzania badala ya kufungiwa ndani, watapelekwa hapo kwa ajili ya kupata huduma muhimu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

**KIWANJA KINAUZWA** Kiwanja kizuri kilichopo ITV Mikocheni chenye sq.m 5,262, karibu na benki ya CRDB na Nyumba za Mawaziri kinauzwa. Kinafaa kwa kupaki malori, Yard ya Ujenzi, Jengo la Ofisi, Kiwanda cha Kati nk. Simu 0756 266525.

## NAFASI ZA KAZI

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.

## MAGARI

**MAGARI YANAUZWA,**

1. LEYLAND DAF TANI 4, DIESEL, SAFI SANA, 4200 CC.
2. LEYLAND DAF TANKI YA MAJI LITA 8000 DIESEL 5800 CC. KUBADILISHANA NA GARI NYINGINE, PIGA SIMU NAMBA 0657 370655.

*Uza Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0767 223311*

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**Ernest John Gabriel** anatangaza kupotelewa na kadi ya gar iaina ya Mitsubishi yenye namba Za usajili **T.571 DCZ.** Chasis no. **FE63EEX5600661,** na Engine namba **4M51A81985** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/945/2019**

15063402

Yetu Microfinance Bank PLC

**Wekeza nasi katika akaunti maalum upate faida kubwa.**

**Muda wa uwekezaji:**
Miaka miwili

Kwa mwekezaji mwenye kiasi cha zaidi ya million 50, tafadhali piga simu 0762623062

**Unaweza kuwekeza kuanzia shilingi million moja kwa faida ya hadi 13%**

215048502

## Taarifa ya Kufungwa/ Kufutwa kwa Kampuni

**INATOLEWA TAARIFA KUWA** katika mkutano wa ziada wa **LAC INVESTMENT HOLDING CO. LTD** uliofanyika siku ya 8 ya October 2018, azimio maalum lilipitishwa kwa pamoja na wamiliki/wanahisa wa kampuni la kufunga kampuni kwani haijafanya shughuli zake tangu iliposajiliwa na hakuna mipango ya kuanza shughuli.

Ikiwa mtu ana madai yoyote au maslahi dhidi ya kampuni, wanashauriwa kuwasiliana na kampuni kwenye anwani iliyo chini ndani ya siku 7 za taarifa hii.

**Karimjee Attorneys**
**P.O. Box 76421**
**Dar es Salaam**

115063502

## Taarifa ya Kufungwa/ Kufutwa kwa Kampuni

**INATOLEWA TAARIFA KUWA** katika mkutano wa ziada wa **LAC INVESTORS INC.LTD** uliofanyika siku ya 8 ya October 2018, azimio maalum lilipitishwa kwa pamoja na wamiliki/wanahisa wa kampuni la kufunga kampuni kwani haijafanya shughuli zake tangu iliposajiliwa na hakuna mipango ya kuanza shughuli.

Ikiwa mtu ana madai yoyote au maslahi dhidi ya kampuni, wanashauriwa kuwasiliana na kampuni kwenye anwani iliyo chini ndani ya siku 7 za taarifa hii.

**Karimjee Attorneys**
**P.O. Box 76421**
**Dar es Salaam**

115063502

## KADI YA GARI IMEPOTEA

NIKO BON MWASUMBI ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T. 438 APK AINA YA TOYOTA COROLA RANGI YA KIJIVU. CHASSIS NAMBA AE1100003115.

YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI MB/RB/84/2019.

115063302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO**

**MADAI NA. 183 YA MWAKA 2018**

**BAKARI OMARY MNDEME...........MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**VITALIS PETER.........................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**VITALIS PETER.............MJIBU MAOMBI**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 21/2/2019 mwenyewe binafsi au muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa mkono wangu leo tarehe 17 Mwezi Januari, 2019.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO

115062702

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**HABIBU KASSIM MARENGU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 267 DHJ TOYOTA LITEACE** NOAH. Yenye chassis namba **SRS00006011** na Engine namba **357145673.** Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MOR/TR/RB/136/2019.**

115062302

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TEMEKE**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 160 YA 2018**

**DR. DEOGRATIAS SOKA..........MDAI**

**DHIDI YA**

**MALUGU MAHINDI............MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

**MALUGU MAHINDI – POPOTE ULIPO**
Dr. DEOGRATIAS SOKA wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Temeke (Usalama). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 12 mwezi 03 mwaka 2019. Hivyo basi unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya Tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi Baraza la Ardhi na Nyumba TEMEKE. Endapo hautatekeleza haya Shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.
**AMRI hii imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 05 mwezi 02 mwaka 2019.**

MWENYEKITI,
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA TEMEKE

115062502

## KUPOTEA KWA HATI

Anaitwa **ROMAN M. MKUDE** wa Kihonda amepotelewa na hati ya toleo la kiwanja **No; 278** eneo la Kilakala kilichokuwa cha Marehemu **JOSEPH HALINDOGO.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: Ref: **NO.MOR/PS/B.I/35/VOL: CLXIV/56.**

215063002

## NYUMBA INAUZWA TABATA

NYUMBA INAUZWA ILIYOPO TABATA CHANG'OMBE YENYE VYUMBA 3 IKIWEMO MASTER MOJA, PUBLIC TOILETS, STORE, DINNING, JIKO, PARKING YA MAGARI (BEI NAFUU).

**MAWASILIANO:**
**0788 058343 / 0654 969280 / 0622 096882.**


JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO? Nipashe

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO




# BARCA KUTOMPA MKATABA MPYA RAKITIC

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona haina mpango wa kumpa ofa ya mkataba mpya kiungo wake, Ivan Rakitic licha ya mchezaji huyo raia wa Croatia kusisitiza kuwa anataka kubakia hapo kwenye dimba la Nou Camp.

Rakitic alikataa kujiunga na Paris Saint-Germain kipindi cha majira ya joto kilichopita na kuamua kubakia hapo Barcelona, licha ya kuambiwa kwamba mkataba wake hautaongezwa.

Rakitic amesisitiza kuwa ana furaha kuendelea kucheza hapo Barcelona, lakini bado anaendelea kusubiri kufanya mazungumzo na rais wa Klabu hiyo, Josep Maria Bartomeu kwa ajili ya kuongezewa mkataba mpya.

"Nina furaha zaidi kuwa hapa na sina mpango wa kuondoka," alisema Januari mwaka huu. "Nimezungumza na rais na nimemdokeza uamuzi wangu wa kuongeza mkataba."Hata hivyo, Sky Sports imeripoti kwamba, Bartomeu mwenyewe hana mpango wa kutoa ofa kwa Rakitic na mchezaji huyo anaweza kuondoka akitaka na sasa amebakiwa na miaka miwili kwenye mkataba wake.

Klabu ya Inter Milan imekuwa ikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili Rakitic, huku pia ilionyesha nia ya kumsajili Luka Modric katika kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Rakitic amewachezea mabingwa hao wa La Liga katika kila mchezo msimu huu na ameonekana kuendelea kuwa kwenye kiwango bora.

# Martial, Jesse waipa pigo United

**MANCHESTER,** England

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer yupo kwenye wakati mgumu baada ya kikosi chake kukumbwa na majeruhi, huku Anthony Martial na Jesse Lingard wakiwa shakani kuivaa Chelsea na Liverpool, baada ya kuumia katika mchezo waliopoteza dhidi ya PSG.

Martial alishindwa kuingia katika kipindi cha pili, huku Lingard alitolewa katika kipindi hicho kutokana na kuumia misuli ya nyama za paja, wakati United ikifungwa 2-0 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na sasa wawili hao hawatakuwapo kwenye mchezo dhidi ya Chelsea pale Stamford Bridge, na gazeti la Daily Mail limeripoti kwamba pia wanaweza kuukosa mchezo dhidi ya wapizani wao wakubwa Liverpool.

Ikiwa imecheza mechi 11 bila kufungwa chini ya Solskjaer, klabu hiyo ilikumbana na kipigo chake cha kwanza chini ya kocha huyo wa muda Jumanne wiki hii, lakini sasa kikosi hicho kimekumbwa na pigo la majeruhi.

Matokeo ya mchezo huo wa kwanza wa hatua ya mtoano ya timu 16 bora Ulaya kumewaacha mashetani wekundu hao kwenye hatari ya kutolewa, huku mchezaji wake,Paul Pogba hatacheza mechi ya marudiano kutokana na kupewa kadi nyekundu.

Akizungumza mara baada ya mchezo huo, Solskjaer alikubali kwamba kikosi chake kilikumbwa na majeruhi baada ya kuumia kwa Martial na Lingard.

"Unajua kwamba, ana matatizo ya misuli ya nyama za paja, pamoja na nyonga," alisema kocha huyo mwenye umri wa miaka 45.





# Kompany kuendelea kuula Manchester City




**MANCHESTER,** England

NAHODHA wa Manchester City, Vincent Kompany anatarajiwa kupewa ofa ya mkataba mpya wa mwaka mmoja ili kuendelea kuitumikia klabu hiyo ya hapo Etihad.

Kompany amekuwa na City tangu Agosti mwaka 2008 ambapo alipojiunga akitokea klabu ya Hamburg kwa ada ya thamani ya euro milioni 8.5, kabla Klabu hiyo haijanunuliwa na Sheikh Mansour.

Tangu hapo ameichezea timu hiyo jumla ya mechi 348, akifunga mabao 19 na kutoa pasi za wmsiho 11, na kutwaa mara tatu taji la Ligi Kuu England, mataji matatu ya Ligi na moja la FA.

Kwa mujibu wa Goal.com, Klabu hiyo itampa mkataba huo wa mwaka mmoja mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji mwishoni mwa msimu huu wakati mkataba wake wa sasa utakapokuwa unafikia mwisho.

Na hiyo imekuja baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kusumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara na kumfanya muda mwingi akiwa nje ya dimba. Amecheza mechi tisa za Ligi Kuu msimu huu, na hajacheza tangu wakati timu yake ikiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Liverpool Januari mwaka huu.

Kompany kwa sasa anapokea mshahara wa pauni 120,000 kwa wiki, lakini amekubali kupunguziwa mshahara ili aendelee kubakia na timu hiyo kwa ajili ya msimu ujao.

## HABARI MICHEZO

# Chelsea, Utd zamwania Zidane

**LONDON,** England

IMERIPOTIWA kuwa, klabu ya Chelsea ipo mbioni kutafuta saini ya aliyekuwa Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane ili kuchukua mikoba ya Maurizio Sarri.

Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 46, Zidane amekuwa nje ya kazi yake kwa muda kidogo tangu alipoachana na Real Madrid baada ya kuipatia mataji matatu mfululizo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Sarri amekuwa kwenye wakati mgumu tangu alipopokea kichapo cha mabao 6 - 0 kutoka kwa Manchester City wiki iliyopita huku wakimpendekeza, Zidane kuchukua nafasi yake.

Taarifa kutoka kwenye vyombo mbalimbali vya habari zinaeleza kuwa wiki hii kumekuwa na vikao ambavyo vikiendelea baina ya klabu hiyo na watu wa karibu wa Zidane ili kuhakikisha suala hilo linatimia.

Kutua kwa gwiji huyo wa Ufaransa ambaye amewahi kutwaa Kombe la Dunia akiwa na Les Bleus, kutamfanya nyota wa klabu ya Chelsea, Eden Hazard kuongeza mkataba mpya wa kuendelea kusalia kwenye viunga hivyo vya Stamford Bridge.

Hata hivyo, Chelsea huenda ikakumbana na vikwazo kutoka Manchester United ambao bado wapo mbioni kuhitaji huduma ya Zidane atakayechukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer ambaye alirithi mikoba ya Jose Mourinho aliyetimuliwa kazi katikati ya Desemba mwaka jana.





# KLOPP ASHTAKIWA NA FA

**LONDON,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp ameshtakiwa na Chama cha Soka cha England (FA) kwa matamshi yake aliyoyatoa dhidi ya mwamuzi, Kevin Friend wakati timu yake ikitoka sare na West Ham kwenye dimba la London.

Katika mchezo huo, bao la Liverpool lilionekana ni la kuotea, lakini mwamuzi hakuweza kuliona, na baada ya mchezo huo Klopp alidai kwamba, maamuzi ya mwamuzi huyo yaliathiri matokeo kwenye mchezo huo.

Kwa mujibu wa taarifa ya FA imeeleza kuwa: "Jurgen Klopp ameshtakiwa kwa kuhoji uwezo wa mwamuzi, Kevin Friend baada ya sare ya 1-1 dhidi ya West Ham.

Klopp amepewa hadi Februari 18 mwaka huu kuweza kujitetea na kama atapatikana na hatia atakumbana na faini.

Kauli ya Klopp kwenye mchezo huo ilisema: "Nimesikia goli letu lilikuwa la kuotea, nina uhakika kabisa kwamba mwamuzi alijua hilo. Katika hali ya 50-50 ilikuwa ni adhabu ndogo kwa timu nyingine, kitu ambacho hakifanyi maisha yakawa rahisi."

Na akizungumza na Sky Sports, kocha huyo raia wa Ujerumani aliongeza: "Kama binadamu, kama ningejua nimefanya makosa kwenye kipindi cha kwanza, singependa kuongeza gepu jingine. "Waamuzi ni binadamu, na nalielewa hilo, lakini goli letu halikuwa baya."

# *Pochettino awaita wachezaji mashujaa*

**LONDON,** England

KOCHA Mauricio Pochettino amewapongeza wachezaji wake kwa kuwa mashujaa baada ya Jumatano usiku kuifunga Borussia Dortmund na kuiweka Tottenham mguu mmoja ndani kuelekea hatua ya Robo Fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Spurs iliwafunga vinara hao wa Ligi ya Bundesliga katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Wembley Stadium, mabao 3-0 baada ya kurejea kutoka mapumziko.

Pochettino sasa atawaruhusu nyota wake kupata mapumziko ya siku chache baada ya kuondoka na ushindi huo mnono lakini akiwakumbusha kujiandaa kwenda Ujerumani katika mechi ya marudiano kumalizia kazi waliyoianza.

"Ninajisikia furaha sana," alisema Pochettino. "Wachezaji wangu ni mashujaa. Unapokutana na timu kama Borussia Dortmund, unatakiwa uonyeshe nidhamu. Tunahitaji kwenda Dortmund tukiwa na malengo ya kuishinda mechi.

"Ni kweli, tuna furaha sasa kwa sababu tumepata matokeo mazuri lakini bado tunatakiwa kufanya kazi zaidi. Kwa upande wangu, nina furaha. Ninataka kuwapongeza wachezaji wangu. Kwa kuonyesha kiwango bora.


"Kwangu, ni mchezo wa raundi ya kwanza, ni nusu tu ya kwanza ya mchezo.

"Tunahitaji kufikiria kwamba tunatakiwa kumalizia kazi tuliyoianza. Kila siku, pale unapocheza na timu nzuri kama Dortmund, ni ngumu na bado tuna kazi ya kufanya mbele yetu."

Son Heung-min aliendeleza wimbi lake la kufunga akichukua nafasi ya kutokuwapo kwa Harry Kane kwa kuunganisha mpira wa krosi uliopigwa na Jan Vertonghen na kufunga bao la utangulizi dakika ya 47.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# JUVENTUS YAJIPANGA KUMSAJILI MO SALAH

Vigogo hao wa Italia wajiandaa kutoa dau nono pamoja na mshambuliaji wake Dybala ili...

**LONDON,** England

KLABU ya Juventus imeripotiwa kuwa inajipanga kutoa ofa kwa mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, pamoja na kumtoa Paulo Dybala pamoja na euro milioni 50.

**Kwa mujibu wa Sky Sports, mpango huo thamani yake ya jumla itakuwa ni euro milioni 125 kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya Misri.**

Kwa mujibu wa gazeti la Tuttosport, Liverpool itapokea ofa ya Salah kutoka Juventus pamoja na euro milioni 50 na Dybala, ambapo thamani yake ya jumla itafikia kuwa ni euro milioni 125.

Miamba hao wa soka la Italia wanapanga kumsajili mchezaji huyo kwa ajili ya kukiimarisha zaidi kikosi chake ili kiweze kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Tayari Juventus imemsajili Cristiano Ronaldo kutoka Real Madrid, lakini bado wanaona kwamba, kikosi chao kinahitaji kuongezewa nguvu na Salah ndiye anayeonekana kuwa chaguo lao sahihi.

Dyabala ambae ni mchezaji wa kimataifa wa Argentina, msimu huu kiwango chake kinaonekana kushuka hasa baada ya ujio wa Ronaldo na hivyo wanapanga kumtumia kama chambo kwenye usajili huo.

Taarifa nyingine zinasema kuwa beki wa kushoto wa Real Madrid, Marcelo anajiandaa kuondoka katika klabu hiyo ya Hispania na kumfuata mshambuliaji, Cristiano Ronaldo.

Inaelezwa kuwa, Marcelo ambaye ana umri wa miaka 32, amesema ataondoka Real Madrid katika kipindi cha majira ya joto na kutua Juventus kuungana na Ronaldo ambaye kwa pamoja walikuwa na kipindi kizuri kwenye klabu hiyo inayoshikilia taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## ZISIKUPITE

### KOMPANY KUAGWA AGOSTI

NAHODHA wa Manchester City, Vincent Kompany anajiandaa kusaini mkataba mpya wa mwaka mmoja na klabu hiyo lakini ukionyesha mshahara wake atakaolipwa utapungua. Beki huyo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji (32), ataagwa rasmi ifikapo Agosti mwaka huu. ***(Mail)***

### FELIX AKARIBIA UNITED

KLABU ya Manchester United inatarajia kumsajili kiungo wa Benfica ya Ureno, Joao Felix (19) katika kipindi cha majira ya joto. ***(Sun)***

### MESSI KUZEEKEA BARCA

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu amesema kuwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi (31), atasaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Nou Camp. Mkataba wake wa sasa na klabu hiyo utamalizika katika kipindi cha majira ya joto ifikapo mwaka 2021. ***(RKB, via Marca)***

### WERNER AITWA LIVERPOOL

WACHEZAJI wa Liverpool, Naby Keita na Sadio Mane wamemweleza straika wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner (22) atue Anfield kama nyota huyo ataamua kuondoka RB Leipzig katika kipindi cha majira ya joto. ***(ESPN)***

### MANE ALITAKIWA BAYERN

WINGA wa Timu ya Taifa ya Senegal, Sadio Mane (26), amesema kuwa alikuwa akiwindwa na Bayern Munich wakati Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola alipokuwa akiwafundisha vigogo hao wa Bundesliga. ***(Bild, via Goal)***

### JUVE: DYBALA HAUZWI

JUVENTUS imesitisha uamuzi wake wa kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Argentina, Paulo Dybala (25), katika kipindi cha majira ya joto na kuzima ndoto za Chelsea na Manchester United ambao walionyesha nia ya kumsajili. ***(Sun)***

### WENGER ALIMTAMANI SANCHO

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger ameweka wazi kuwa alijaribu kufanya mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho alipokuwa na umri wa miaka 18 na akiichezea Manchester City. ***(beIN Sports)***

### UNITED KUNASA WANNE

MANCHESTER United imewataja mabeki, Kalidou Koulibaly (27) wa Napoli, Lucas Hernandez (22) wa Atletico Madrid na Nikola Milenkovic (21) wa Fiorentina pamoja na winga wa Juventus, Douglas Costa (28) ni kati ya wachezaji wapya inaotaka kuwasajili katika kipindi cha majira ya joto. ***(Mirror)***

### MARCELO KUMFUATA RONALDO

BEKI wa kushoto wa Real Madrid, Marcelo (30) anatarajia kujiunga na mchezaji mwenzake wa zamani wa timu hiyo, Cristiano Ronaldo katika klabu ya Juventus ifikapo majira ya joto mwaka huu. ***(Mail)***

### SARRI PRESHA JUU

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri yuko katika presha ya kuhakikisha anachukua taji la Ligi ya Europa League msimu huu ili kunusuru ajira yake. ***(Telegraph)***

## Mkwabi: Tunasubiri wakati tuwamalize

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU homa ya pambano la watani wa jadi ilizidi kupanda, Mwenyekiti wa Simba, Swedi Mkwabi, amesema kuwa kwa upande wake anasubiri muda ufike ili timu yake iweze kutimiza mpango wa kuondoka na pointi tatu dhidi ya Yanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkwabi alisema kuwa awali mawazo na nguvu zao walizielekeza katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Misri ambao walishinda bao 1-0 na sasa zamu na nguvu za maandalizi zimeelekea kuisubiri Yanga.

"Jukumu la mchezo na Al Ahly limepita, sasa tunaelekeza nguvu katika mchezo wa Jumamosi, tunakiamini kikosi chetu kina uwezo mkubwa wa kuondoka na ushindi mbele ya Yanga, ni jambo muda tu kulitimiza hili," alisema Mkwabi.

Aliongeza kuwa anawataka mashabiki wajitokeze kwa wingi kuishangilia timu yao kama walivyofanya katika mchezo dhidi ya Al Ahly.

" Hakuna shaka mashabiki wetu walichangia kwa kiasi kikubwa sana kwenye ushindi dhidi ya Waarabu kutokana na wingi wao uwanjani, tungependa kuona Jumamosi tunajaa kwa wingi kuwasapoti na kuwapa hamasa wachezaji wetu," alisema Mkwabi.

## KVZ kuwakaribisha New Star Amaan

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MZUNGUKO wa lala salama wa Ligi KUU Zanzibar kwa vinara wa ligi hiyo "Maafande" wa KVZ kuwakaribisha New Star kutoka Pemba katika mchezo utakaochezwa kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KVZ, Shekha Khamis, alisema kuwa ameiandaa vyema timu yake kuendelea kupambana lakini akaongeza kwamba ni mapema kueleza kwamba timu yake itachukua ubingwa wa ligi hiyo.

Shekha alisema mara nyingi ushindani huongezeka katika mzunguko wa pili baada ya timu kujiimarisha baada ya kuimarisha vikosi vyao katika dirisha dogo la usajili ikilinganishwa na mzunguko wa kwanza unavyokuwa.

Kocha huyo alisema pia anaamini timu yake ipo katika klabu zinazopewa nafasi ya kutwaa ubingwa endapo wachezaji wake watajituma uwanjani na kutoruhusu kufanya makosa ambayo yatawafaidisha wapinzani wao.

Mechi nyingine itakayochezwa kwenye Uwanja wa Amaan leo kuanzia saa 8:00 mchana itakuwa ni kati ya JKU ambayo iko katika nafasi ya pili katika msimo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 38 dhidi ya Chipukizi kutoka Pemba ambayo nayo ipo nafasi ya 11 ikiwa na pointi 18.

Kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba timu ya Opec itavaana na Malindi kuanzia saa 8:00 mchana na jioni Mbuyuni itawakabili Muhustadhi wa Chuoni.

# DANTE AFUNGUKA NAMNA ATAKAVYOMKABA KAGERE

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI ikiwa imebaki siku moja tu kabla ya mchezo wa watani wa jadi nchini, beki wa kati wa Yanga, Andrew Vincent 'Dante' amesema kuwa amejiandaa "kula sahani moja" na mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere.

Dante ameliambia gazeti hili kuwa licha ya kuwa mchezo huo kutarajiwa kuwa mgumu, mahesabu yake anayapanga namna ya kumdhibiti mshambuliaji huyo raia wa Rwanda ambaye alijiunga na Simba akitokea Gor Mahia ya Kenya.

Beki huyo alisema kuwa anafahamu ubora wa Kagere lakini hatishiki naye na amejipanga kumdhibiti endapo atapata nafasi ya kucheza.

> **"Mchezo utakuwa mgumu na ndio maana kila timu inafanya maandalizi kuhakikisha inaibuka na ushindi, hakuna mchezaji ninayemuogopa Simba, najua wanawashambuliaji wazuri kama Kagere lakini tutawadhibiti," alisema Dante.**

Aidha, alisema kama kocha wake, Mwinyi Zahera atampa nafasi ya kucheza katika mchezo huo, atahakikisha anamkaba vema mshambuliaji huyo ambaye mapema wiki hii aliifungia timu yake bao pekee katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Misri.

Aliongeza kuwa hamasa katika kikosi ipo juu na kila mchezaji anasubiri kufanya kazi yake uwanjani siku ya mchezo huo.

Kikosi cha Yanga kinatarajia kurejea jijini Dar es Salaam leo kikitokea Morogoro ambapo waliweka kambi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo huo.

Yanga ndio mwenyeji wa mechi hiyo ambayo itaanza kuchezwa kuanzia saa 11:00 jioni na watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0 waliopata dhidi ya JKT Tanzania wakati Simba yenyewe iliwaduwaza Waarabu wa Misri kwa kuwafunga goli 1-0 mapema wiki hii.



Wachezaji wa Timu ya Simba Queens ya jijini Dar es Salaam wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi za Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania, ambayo inatarajia kuingia katika mzunguko wa pili hivi karibuni. **PICHA: SSC**

# *Serengeti Boys kujiwinda Arusha*

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys) kinatarajia kwenda jijini Arusha ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kuelekea Fainali za Afrika kwa umri huo (AFCON U-17) zinazotarajiwa kufanyika hapa nchini Aprili mwaka huu, imeelezwa.

Kambi hiyo ya Arusha inatarajiwa kuwa ya muda mfupi na baada ya hapo itaelekea Uturuki kwa ajili ya kushiriki mashindano ya kimataifa yaliyoandaliwa na Shirikisho la Soka Ulaya (UEFA) ambayo yatashirikisha timu kadhaa za Afrika na nyingine kutoka Ulaya.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema hayo jana wakati akizindua nembo maalum ya Fainali za Afrika ambazo zinafanyika Tanzania kwa mara ya kwanza.

Mwakyembe alisema kuwa uamuzi wa kuipeleka Serengeti Boys Arusha ni kutaka kuwaandaa wachezaji wa timu hiyo kuizoea hali ya hewa ya baridi ambayo watakutana nayo Uturuki.

Alisema kuwa Serikali inaimani na kikosi hicho kutokana na viwango vinavyoonyeshwa na wachezaji wake katika mechi mbalimbali za kirafiki wanazocheza huku akiwaomba Watanzania kujiandaa kuwaunga mkono wakati fainali hizo zitakapoanza.

"Timu yetu itacheza mechi na mataifa makubwa, itapata uzoefu zaidi, itacheza na timu mbalimbali kama Hispania, Australia, Cameroon, tumepangwa na Nigeria, ni jina kubwa, lakini wakifuatilia rekodi zetu wanapata homa," alisema Mwakyembe.

Alisema pia wizara yake inaendelea kumpongeza mlezi wa timu hiyo, Dkt. Reginald Mengi kwa dhamira yake ya kutaka kuona Serengeti Boys inapata mafanikio pamoja na uongozi wa Azam FC kwa kukamilisha maandalizi kwenye Uwanja wa Azam Complex ambao utatumika kwenye michuano hiyo.

Tujitolee kwa sababu tunataka kuona tunabadilisha rekodi ya soka na michuano hii iwe chachu ya kushinda na kuirejesha Tanzania katika ramani ya michezo duniani," aliongeza Mwakyembe ambaye alisema kamati yake imejipanga kuhakikisha michuano hiyo inakuwa bora.

Aliongeza kuwa, anahitaji kuona mchakato wa kuuza tiketi kwa ajili ya kuingia uwanjani kushuhudia mechi za AFCON U-17 unaanza mapema ikiwezekana iwe wiki mbili kabla ya siku ya ufunguzi ili kuondoa usumbufu wa mashabiki kupanga foleni siku ya mchezo.

Michezo

Ijumaa Februari 15, 2019

Nipashe




Juve yajipanga kumsajili Mo Salah

HABARI UK. 30




Golikipa wa Tottenham, Hugo Lloris, akiokoa mpira uliopigwa kwa kichwa na straika wa Borussia Dortmund, Dan-Axel Zagadou (mbele yake) na kuwanyima nafasi ya kufunga vigogo hao wa Bundesliga katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi usiku. Spurs ilishinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

## Azam yazidi kupotea Bara

**Na Nebert Msoka,** MBEYA

MABINGWA wa Kombe la Kagame, Azam FC wameendelea kujiweka katika nafasi ngumu ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kukubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Tanzania Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Sokoine jijini hapa.

Kwa matokeo hayo, Azam FC ambayo ilishuka uwanjani jana ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 na Lipuli FC ya Iringa, itaendelea kubaki kwenye nafasi ya pili na pointi 49 wakati Tanzania Prisons wamefikisha pointi 29 na kuanza kujinasua kwenye janga la kushuka daraja.

Goli la dakika ya 35 lililofungwa na Jumanne Elfadhili kwa mkwaju wa penalti lilitosha kuwapatia Maafande hao pointi tatu muhimu na kuwatuliza mabingwa hao wa Kombe la Mapinduzi Zanzibar.

Tanzania Prisons walipata tuta hilo kufuatia beki wa Azam FC, Yakubu Mohamed kuunawa mpira akiwa ndani ya eneo la hatari na hivyo mwamuzi wa mchezo, Hussein Athuman kutoka mkoani Katavi kuamuru adhabu hiyo.

Beki huyo mahiri wa Tanzania Prisons, Elfadhili alipiga tuta hilo kiufundi na kumpoteza kipa wa Azam, Benedict Haule ambaye alianguka kulia na mpira ukapita upande wa kushoto na kutinga wavuni moja kwa moja katika mchezo huo ambao ulishuhudiwa na mashabiki wachache.

Ushindi ilioupata Tanzania Prisons ni wa tano tangu timu hiyo ilipomtimua aliyekuwa Kocha Mkuu, Abdallah Mohamed.

# Aussems, Zahera watambiana

**Na Mwandishi Wetu**

### ●●● Kila mmoja amejipanga kuondoka na pointi katika mchezo huo utakaochezeshwa...

IKIWA imebakia siku moja ya kumaliza ubishi kati ya watani wa jadi, Yanga na Simba, makocha wa timu hizo, Mwinyi Zahera na Patrick Aussems kila mmoja anatamba kuwa kikosi chake kitaibuka na matokeo mazuri katika mchezo huo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara

**Katika kujiandaa na mchezo huo, Yanga iliweka kambi yake mkoani Morogoro wakati Simba iliyokuwa na mechi ya kimataifa ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ilibakia jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera alisema kuwa mchezo wa kesho watawashangaza Simba kwa kuingia uwanjani "kivingine" na kuwaonya wapinzani wao hao wasitarajie mteremko baada ya kupata ushindi katika mechi yao iliyopita dhidi ya Al Ahly kutoka Misri.

Zahera alisema kuwa anayafahamu mapungufu yaliyopo katika kikosi cha wapinzani wake ambayo amejipanga kuyatumia vema ili kupata ushindi katika mechi ya kesho.

Kocha huyo alisema pia kila mchezo una mipango yake hivyo watu wasitegemee kucheza kwa namna ambayo walicheza kwenye mchezo wao wa kwanza uliochezwa Septemba 30 mwaka jana ambao ulimalizika kwa sare ya bila kufungana.

"Hautakuwa mchezo mwepesi kwao wala kwetu, hatutacheza kama tulivyocheza awali, kila mchezo una mipango yake, hata huu wa Jumamosi una mipango yake, nashukuru sina majeruhi wengi kwenye kikosi, hii inanipa nafasi pana ya kupanga kikosi kitakachoikabili Simba, nimetumia siku hizi tulizokaa Morogoro kuwapa mbinu wachezaji wangu kupitia mapungufu ya wapinzani wetu," alisema kocha huyo.

Aussems alisema kuwa amekiandaa kikosi chake kuendeleza kasi waliyoionyesha katika mechi iliyopita ingawa ni ya mashindano tofauti.

"Tulifanikiwa kushinda mechi ile ya Ligi ya Mabingwa Afrika, sasa ni zamu ya kuchukua pointi tatu tena za Ligi Kuu Tanzania Bara, tunafahamiana na wachezaji wanafahamiana, nasisitiza kuwaheshimu wapinzani wetu, wanaongoza ligi, sisi tuko nyuma, lakini ushindi utatufanya tupige hatua mbele," alisema Mbelgiji huyo.

Kikosi hicho cha Yanga kilitarajiwa kurejea Dar es Salaam jana jioni ambapo wachezaji wake watawekwa kambini mpaka baada ya mchezo huo wa kesho.

Katika mchezo wa mzunguko wa kwanza ambao Simba walikuwa nyumbani, licha ya kuutawala mpira lakini walishindwa kuondoka na ushindi.

Taarifa kutoka katika Kamati ya Waamuzi inasema kuwa refa, Hans Mabena kutoka Tanga ndiye atapuliza filimbi ya kati kwenye mchezo huo akisaidiwa na Mohammed Mkono na Kassim Mpanga, wakati Heri Sassi atakuwa mezani.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >